# USAWIRI WA UGONJWA, UUGUZI NA TIBA KATIKA METHALI ZA KISWAHILI

**JOSEPH GIKONYO MWANGI**

**MAKI/2022/44670**

**Tasnifu Iliyowasilishwa Katika Shule Kuu ya Mafuzu ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili (MA) katika Kiswahili ya Chuo kikuu cha Mount Kenya**

**CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**JULAI, 2025**

Mount Kenya University

**UNGAMO NA DHINI**

**UNGAMO LA MTAHINIWA**

Tasnifu hili ni kazi yangu asilia na wala haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine chochote.

**Saini:** ...... **Tarehe:** *Julai 1, 2025*

**Joseph Gikonyo Mwangi**

MAKI/2022/44670

**IDHINI YA MSIMAMIZI**

Tasnifu hii iliwasilishwa katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

**Saini:** ............................................................ **Tarehe:** 01/07/2025

**Dkt. Stanley Adika Kevogo**

Idara ya Lugha, Taaluma za Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga cha Sayansi na Teknolojia

Mount Kenya University

# TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu kwa kuniwekea msingi bora wa malezi bora. Na pia kwa familia yangu kwa himizo ambalo wamenipa kila wakati kuendelea na kisomo changu.

Mount Kenya University

## SHUKRANI

Kazi hii ya utafiti wangu ni zao la michango na maelekezo ya watu wengi. Nachukua fursa hii kuwashukuru wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine kufika hapa nilipo katika kisomo changu. Nimetaka kuwataja wote lakini naomba radhi niwataje wachache tu ambao michango yao kwa kazi hii kamwe haiwezi fichika.

Nimpe shukurani zangu Maulana kwa kunineemesha, kunipa uwezo na stahamala katika kuifanya kazi hii ya kiutafiti ambayo imenigharimu nguvu na muda mwingi. Pasi yeye singeweza.

Natoa shukrani zangu kwa msimamizi wangu, Dkt. Adika Stanley Kevogo, kwa uelekezi na ushauri wake kutoka mwanzo hadi hatima ya kazi hii bila kuchoka. Kila wakati nilipohitaji uelekezi hakuchelea kunielekeza, hakuchoka kunipa ushauri na kuirekebisha kazi hii hatua baada ya nyingine hadi nilipoweza kuikamisha. Ahsante sana, Mola akubariki sana na siha njema akujalie Daktari.

Pia na washukuru Bw. Samuel Kamau mwanafunzi wa Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Leibniz katika mji wa Hannover, Ujerumani na Bw. Benson Wahiu Mwangi mwandani wangu wa karibu kwa kunipa moyo na motisha ya kuendelea na utafiti huu kila wakati.

Mount Kenya University

## IKISIRI

Tangu jadi, binadamu amekumbwa na magonjwa hatari yaliyokuwa changamoto katika maisha yake. Kwa hivyo, wanajamii wamekuwa wakitafuta njia za kuuguza na kutibu magonjwa ya kila aina. Utafiti huu unahusu nafasi ya methali za Kiswahili katika kusawiri ugonjwa, uuguzi na tiba yake. Methali ni kipera muhimu cha utanzu wa semi katika fasihi simulizi. Methali ni hazina kubwa katika maisha ya wanajamii kwani zinasheheni dhima mbalimbali katika jamii inayohusika. Mojawapo ya dhima hizo ni kusawiri hali mbalimbali zinazowazunguka wanajamii, yakiwemo magonjwa yanayowakumba, uuguzi na jitihada za kutafuta tiba mujarabu ya magonjwa haya. Utafiti huu umechochewa na uhalisi kwamba, ingawa methali za Kiswahili zimechunguzwa, kuorodheshwa na kuainishwa kwa kategoria mbalimbali kwa mujibu wa miktadha na dhima zake, bado kuna pengo la maarifa katika uchunguzi wa usawiri wa magonjwa, uuguzi na tiba katika kuwasilisha ujumbe wa methali hizi. Utafiti huu unajikita katika malengo matatu mahususi: kwanza, kufafanua matumizi ya vipengele vya fani kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Pili, kudadavua matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili na tatu kutathmini athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe wa methali za Kiswahili. Uchunguzi huu uliokitwa katika muundo wa kimaelezo unaongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Ferdnand De Saussure na Charles Pierce. Vyanzo vya methali zinazochambuliwa ni kamusi 3 za methali - *Maelezo ya Methali za Kiswahili*, *Kamusi ya Methali* na *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi*. Sababu ya kuteuliwa kwa kamusi hizi ni kuwa zinaafikiana na azma kuu, malengo na nadharia ya utafiti. Usampulishaji lengwa ndio uliotumiwa kuteua kamusi pamoja na methali zinazohusu ugonjwa, uuguzi na tiba katika kamusi teule. Idadi lengwa ni methali 5,856 kwenye kamusi teule. Kati ya methali hizi, 90 ndizo zilizoteuliwa kwa sababu zinaakisi malengo ya utafiti. Njia za ukusanyaji wa data maktabani ambazo ni kusoma tasnifu mbalimbali, vitabu na makala mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu, ndizo zinazotumiwa kuufanikisha utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba, methali za Kiswhili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumia vipengele vya fani kama vile takriri, kinaya, taswira, kejeli, tashihisi na sitiari kuwasilishia ujumbe wake. Vipengele hivi vya fani ndivyo vitumikavyo kuufumba na kuukoleza ujumbe wake. Pia imethibitika kwamba methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumika kuwasilisha ujumbe maalum kama vile jumbe zilizoza matumaini, utamaushi, tahadhari, subira pamoja na kuhamasisha upendo, umoja na ushikamano katika jamii. Hatimaye, athari chanya na hasi zinazotokana na ufasiri wa ujumbe katika methali hizi zinajitokeza vyema kama vile: umuhimu wa kufanya mambo kwa utaratibu, uhusiano wa karibu uletwao na ugonjwa, ukataji shauri, usiri mtu anapougua, ustahamilivu, ubaguzi na unyanyapaa, makovu ya ugonjwa maishani, msaada, matumaini pamoja na uchungu uletwao na baaadhi ya magonjwa unadhihirishwa. Kutokana na dhima yake kuadilisha vijana na jamii nzima, inapendekezwa methali zihifadhiwe ili kudumisha ujumbe ulio kwenye methali hizi. Ili kuelewa ujumbe wake, muundo wa tungo na maneno ya methali uzingatiwe kwa kina. Utafiti huu una tija kwa wasomi wa fasihi, hususan wenye raghba ya methali kwa sababu umefafanua jinsi ugonjwa, uuguzi na tiba unafanikisha na/kuathiri ufasiri na welewa wa methali za Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatawawezesha watunzi wa kazi za fasihi kuelewa jinsi ya kuutambua ujumbe wa ndani uliofumbatwa kwenye methali hizi ili kuzitumia ifaavyo. Kwa watafiti, matokeo ya utafiti huu ni msingi na chachu ya uchunguzi wa baadaye.

Mount Kenya University

## ABSTRACT

Since time immemorial, human societies have suffered from a myriad of dangerous diseases and their attendant challenges. Community members have been looking for different ways to nurse and treat all kinds of diseases. This study focuses on the place of Kiswahili proverbs in depicting diseases, nursing and their treatment. A proverb is a very important subgenre in the short form genre of Oral Literature. Proverbs are a great treasure in the lives of the members of the community as they accomplish various functions in the concerned society. One of those functions is to portray the various situations that surround the members of the community including the diseases that afflict them, nursing and efforts to find a panacea for these diseases. This study is inspired by the fact that even though researchers of Kiswahili proverbs have identified, collected, listed and classified proverbs in different categories according to their contexts of use and functions, there still exists a lacuna in exploring the depiction of diseases, nursing and treatment in these proverbs. The main goal of this study is to investigate the portrayal of illness, nursing and its treatment in Kiswahili proverbs. This study is based on three specific objectives which are: first, to describe the use of aspects of styles in delineating illness, nursing and treatment in Kiswahili proverbs. Second, to analyse the use of disease, nursing and treatment in conveying messages in Kiswahili proverbs; and thirdly, to evaluate the effects of the depiction of illness, nursing and treatment on the interpretation of messages in Kiswahili Proverbs. The study is guided by Semiotics theory propounded by Ferdinand Saussure and Charles Pierce. The sources of proverbs to be analysed are 3 Kiswahili proverb dictionaries - *Maelezo ya Methali za Kiswahili*, *Kamusi ya Methali* na *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi*. The dictionaries were selected for their consistency with the aim, objectives and tenets of theory of study. Library methods of data collection such as a close reading various texts, dissertations, and various articles related to the research topic were utilised. The dictionaries with proverbs depicting illness, nursing and treatment were purposively sampled. The study's target population comprised the 5,856 proverbs in the 3 dictionaries. Of these proverbs, 90 are analysed in this study as they depict or reflect the objectives of the study. The study's findings demonstrate that Kiswahili proverbs depicting illness, nursing and treatment are used to convey special messages in the community. Such messages include hope, motivation, and warning, patience, unity and solidarity. Similarly, the research results show that Kiswahili proverbs depicting illness, nursing and treatment are made up of aspects of style such as repetition, irony, imagery, satire, alliteration and metaphor which serve to delineate the illness, nursing and treatment. These stylistic features help in deciphering the profound meaning hidden in these proverbs. Finally, it is revealed that the effects of the portrayal of illness, nursing and treatment on the interpretation of messages includes the importance of doing things in an orderly manner, closer relationships brought by illness, decisiveness, confidentiality, tolerance, stigma, trauma, hope and despair in face of incurable diseases. Since proverbs are one of the literary genres that play a significant role in instilling societal values in the youth, it is imperative that they ought to be conserved in order to sustain their valued deep meaning. This study's findings are beneficial to academics, oral and written literature enthusiasts, especially paremiologists because it fosters the understanding of Kiswahili proverbs depicting illness, nursing and treatment. For literary critiques and writers, it enables them understand and utilize the deeper messages carried by the proverbs. Moreover, to multidisciplinary researchers this study provides useful insights on nexus of literature, language and medicine thus laying the foundation for further research.

Mount Kenya University

**YALIYOMO**

**UNGAMO NA DHINI** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKRANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ v

**ABSTRACT** ........ vi

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ xii

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ xiii

**FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA** ........ xiv

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**MISINGI YA UTAFITI** ........ 1

**1.0 Utangulizi** ........ 1

**1.1 Usuli wa Mada** ........ 1

**1.2 Suala la Utafiti** ........ 4

**1.3 Malengo ya Utafiti** ........ 5

**1.4 Maswali ya Utafiti** ........ 6

**1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada** ........ 6

**1.6 Umuhimu wa Utafiti** ........ 7

**1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti** ........ 8

**1.8 Hitimisho** ........ 9

**SURA YA PILI** ........ 10

**MAPITIO YA MAANDISHI** ........ 10



Mount Kenya University

**2.0 Utangulizi** ........ 10
**2.1 Matumizi ya Vipengele vya Fani katika Methali** ........ 10
**2.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Maana** ........ 18
**2.3 Ufasiri wa Maana katika Methali** ........ 22
**2.4 Misingi ya Nadharia** ........ 27
**2.5 Hitimisho** ........ 31
**SURA YA TATU** ........ 32
**MBINU ZA UTAFITI** ........ 32
**3.0 Utangulizi** ........ 32
**3.1 Muundo wa Utafiti** ........ 32
**3.2 Eneo la Utafiti** ........ 33
**3.3 Idadi Lengwa** ........ 34
**3.4 Sampuli na Usampulishaji** ........ 34
**3.5 Njia za Kukusanya Data** ........ 36
**3.5.1 Usomaji wa Kina** ........ 36
**3.5.2 Uchanganuzi wa Matini** ........ 36
**3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data** ........ 36
**3.7 Uchanganuzi wa Data** ........ 37
**3.8 Maadili ya Utafiti** ........ 38
**3.9 Hitimisho** ........ 39
**SURA YA NNE** ........ 40
**UGONJWA, UUGUZI NA TIBA KATIKA METHALI ZA KISWAHILI** ........ 40
**4.0 Utangulizi** ........ 40
**4.1 Vipengele vya Fani Vibainishavyo Ugonjwa, Uuguzi na Tiba** ........ 40

Mount Kenya University

4.1.1 Takriri ........ 42
4.1.2 Tashihisi ........ 47
4.1.3 Taswira ........ 51
4.1.4 Sitiari ........ 65
4.1.5 Kinaya ........ 74
4.1.6 Kejeli ........ Error! Bookmark not defined.
4.1.7 Kwelikinzani ........ 79
4.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Ujumbe ........ 81
4.2.1 Ugonjwa Kuwasilishia Ujumbe ........ 82
4.2.1.1 Kutahadhari kabla ya Hatari ........ 85
4.2.1.2 Dhima ya Uzazi ........ 86
4.2.1.3 Ugonjwa kama Kiashiria cha Tatizo ........ 87
4.2.1.4 Matumaini ........ 87
4.2.1.5 Kudhubutu Kutenda Mambo Hatari ........ 88
4.2.1.6 Umuhimu wa Uvumilivu Maishani ........ 89
4.2.1.7 Utendaji Mambo kwa Utaratibu ........ 90
4.2.1.8 Utendaji Mambo kwa Wakati ........ 90
4.2.1.9 Kuhamasisha Ushirikiano ........ 91
4.2.2 Uuguzi Kuwasilishia Ujumbe ........ 91
4.2.2.1 Matumaini ........ 93
4.2.2.1 Kuuguza ni Tendo la Utu ........ 94
4.2.2.2 Kuuguza ni Kutamauka ........ 95
4.2.2.3 Tahadhari ........ 95
4.2.2.4 Subira ........ 96
4.2.2.5 Uuguzi ni Kikoa ........ 96

Mount Kenya University

4.2.2.6 **Umuhimu wa Ujuzi katika Jamii** ........ 97

4.2.3 **Tiba Kuwasilishia Ujumbe** ........ 98

4.2.3.1 **Tiba ni Suluhisho** ........ 98

4.2.3.2 **Tiba ni Hali Fulani** ........ 101

4.3 **Athari za Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba katika Ufasiri wa Ujumbe** ........ 103

4.3.1 **Athari za Matumizi ya Ugonjwa kwa Ufasiri wa Ujumbe** ........ 104

4.3.1.1 **Utaratibu katika Utendaji wa Mambo** ........ 106

4.3.1.2 **Hadhari na Umakinifu Maishani** ........ 106

4.3.1.3 **Jihadhari na Usemacho** ........ 107

**haya4.3.1.4** ........ **Mahusiano ya Karibu** 108

4.3.1.5 **Maamuzi ya Haraka** ........ 109

4.3.1.6 **Ukuzaji wa Ustahamilivu** ........ 110

4.3.1.7 **Ukarimu na Msaada kwa Wahitaji** ........ 111

4.3.1.8 **Hadaa ya Vitu Vipya** ........ 111

4.3.1.9 **Hila ya Kukurupuka** ........ 112

4.3.1.10 **Ubaguzi na Unyanyapaa** ........ 113

4.3.2 **Athari za Matumizi ya Uuguzi kwa Ufasiri wa Ujumbe** ........ 114

4.3.2.1 **Ukuzaji wa Matumaini** ........ 115

4.3.2.2 **Uwajibikaji** ........ 116

4.3.2.3 **Utamaushi** ........ 117

4.3.2.4 **Ushirikiano na Umoja** ........ 117

4.3.2.5 **Kiwewe nu Makovu Yasiyosahaulika** ........ 118

4.3.3 **Athari za Matumizi ya Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe** ........ 119

4.3.3.1 **Mapenzi ya Dhati** ........ 120

4.3.3.2 Unyumbukaji au Mnepo Maishani ........ 121
4.3.3.3 Uwezo na Maarifa ya Kibinadamu ........ 121
4.3.3.4 Utamaushi ........ 122
4.4 Hitimisho ........ 125
SURA YA TANO ........ 127
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 127
5.0 Utangulizi ........ 127
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ........ 127
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 128
5.2.1 Vipengele vya Fani Vitumikavyo Kubainishia Ugonjwa, Uuguzi na Tiba ........ 129
5.2.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Ujumbe ........ 130
5.2.3 Athari ya Usawiri wa Ugonjwa, Uuguzi na Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe ........ 130
5.3 Hitimisho ........ 130
5.4 Mapendekezo ........ 132
5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti ........ 132
5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadaye ........ 133
MAREJELEO ........ 134
VIAMBATISHO ........ 142
KIAMBATISHO I: METHALI ZIHUSUZO UGONJWA, UUGUZI NA TIBA ........ 142
KIAMBATISHO II: CHETI CHA UZINGATIFU WA MAADILI ........ 146
KIAMBATISHO III: BARUA YA UTAMBULISHO KWA NACOSTI ........ 147
KIAMBATISHO IV: KIBALI CHA CHA UTAFITI NACOSTI ........ 148

Mount Kenya University

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 4.1: Vipengele vya Fani katika Methali Zihusuzo Ugonjwa, Uuguzi na Tiba** .......... 41

**Jedwali 4.2: Maudhui ya Methali za Kiswahili Zinazochambuliwa**...................................... 81

**Jedwali 4.3: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Ugonjwa** ................................................. 83

**Jedwali 4.4: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Uuguzi** ..................................................... 91

**Jedwali 4.5: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Tiba**.......................................................... 98

**Jedwali 4.6: Athari za Matumizi ya Ugonjwa Kusawiria Ujumbe**....................................... 105

**Jedwali 4.7: Athari za Matumizi ya Uuguzi kwa Ufasiri wa Ujumbe**.................................. 114

**Jedwali 4.8: Athari za Matumizi ya Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe**...................................... 120

Mount Kenya University

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| k.h.j | keshatajwa |
| n.w | na wengine |
| Taz. | Tazama |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| uk. | Ukurasa |

Mount Kenya University

## FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

**Ugonjwa** Maradhi, hali inayompata mtu na kuathiri afya yake.

**Uuguzi** Kazi ya kufanya aliye na maradhi kupata nafuu au apone

**Tiba** Kinachotumiwa kuponya maradhi; yaweza kuwa ni dawa za miti ya kiasilia, miungu, maroho au maneno/mawaidha yanayotelewa na muuguzi ama anayechukuwa nafasi ya kuuguza.

Mount Kenya University

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura ya kwanza ya uchunguzi huu inautanguliza kwa kuweka misingi itakayouongoza utafiti huu. Vipengele muhimu vya utafiti vinajadiliwa ili kuvidhihirisha vigeu na kuliibua suala la utafiti linalochunguzwa. Vipengele vyenyewe ni usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, umuhimu wa utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti. Hatimaye, muhtasari wa yaliyomo umewasilishwa kama hitimisho la sura.

## 1.1 Usuli wa Mada

Kazi yoyote ya fasihi huwa na majukumu ya kubadilisha, kuburudisha na kustarehesha, kuchora au kusawiri mazingira ya binadamu, kukuza na kujenga tabia chanya, kukuza lugha ya jamii, kutoa elimu na kuionya jamii. Hii ina maana kwamba kazi ya fasihi huwasilisha hali kamili au halisi kuhusiana na maisha ya jamii ambayo imeizaa, imeilea na kumkuza mwanajamii anayehusika. Methali za Kiswahili ni zao la jamii ya Waswahili ambao eneo lao kuu la makazi ni mwambao wa pwani ya nchi za Afrika masharika ambazo ni pamoja na Kenya, Tanzania, Jamuhuri ya Kongo na Uganda.

Wamitila (2003) na Mauya (2008) wana maoni yanayofanana wanapoeleza methali kuwa ni usemi mfupi wenye maana iliyopanuka na yenye busara au hekima na huwa na mizizi katika jamii fulani na hutoa elimu, kuasa au kukejeli watu au matendo fulani katika jamii kwa njia inayofumba na kuweka tasfida. Hili lina maana kuwa katika ufupisho huu wa methali, bado huhifadhi na kudumisha ujumbe wa mwanajamii. Methali ni semi fupi ambazo ni za kimapokeo na kwa kawaida husheheni pande mbili kimuundo ambapo sehemu moja,

iliyotangulia, hudokeza wazo, nayo sehemu ya pili au fuatilizi, hulikamilisha wazo lile (Mulokozi, 1996).

Kwa mujibu wa M'Ngaruthi (2008) methali ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii, kwa njia iliyofumba na kutolea jambo fulani mfano. Naye Simiyu (2013) anafafanua methali kuwa ni semi fupi zinazosheheni fumbo juu yake, ya ukweli wa maisha ya binadamu na huwa na umbo maalumu. Anaendelea kusema kuwa mafumbo haya huwa yanalenga kufikisha ukweli bila kukwaza walengwa au wanajamii.

Methali katika jamii ya Waswahili, kama ilivyo katika jamii zingine, huwa zinatumika sana katika shughuli mbalimbali za kila siku zinazohusiana na maisha ya wanajamii. Methali ni kipera katika utanzu wa semi na kimekuwapo tangu jadi hadi wa sasa. Hiki ni kipera hai kwani kutokana na mabadiliko katika maisha ya binadamu ambako mambo mapya huzuka kila uchao (Madumulla, 2005).

Mbonde (2005) anasema kuwa methali ni njia ya mkato ya kuelekeza jamii, kuielemisha, kuiadilisha na kuikosoa haswa vijana ili waweze kuzingatia tunu za jadi kwa kina, ndani ya mazingira ya uasili wa jamii. Katika jamii zote ulimwenguni, methali ni kipera cha sanaa ambacho kutambuliwa kwake huwa ni rahisi kutokana na lugha ambayo hutumiwa na muundo wa yaliyomo katika methali. Muundo wa methali huweza kutumia mbinu maalumu za lugha au kishairi kama vile uradidi, kinaya, taswira au sitiari. Mbinu au fani hizi huchangia kwa kiwango kikuu katika kukumbukika kwake. Methali kwa kiwango kikubwa ni kipera kinachotegemea fani nyingine ili kiweze kuenea na kukua kama vile fani ya maongezi, soga, malumbano ya utani, hotuba na majadiliano mazito. Kipera hiki huwa ni sanaa elekezi kwa kuwa hutumiwa kukazia jambo linalozungumziwa au kulifafanua ili liweze kueleweka vyema.

Kimsingi, methali ni kipera ambacho hutumika mno katika lugha ya masimulizi kuliko katika lugha ya maandishi kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi zilizo katika maandishi. Hili laweza kutokana na kuwa methali huchochea kwa urahisi kuendelea kwa mazungumzo au mjadala baina ya watu walio katika maongezi na wanaoonana uso kwa uso kuliko uhusiano uliopo baina ya mwandishi na msomaji katika fasihi andishi. Matumizi ya methali huleta mawasiliano yaliyo na umuhimu wa kipekee kuhusu mamboo maalumu (Nsookwa, 2011)

Maneno katika methali huteuliwa kwa uangalifu mkubwa ili kutimiza mambo makubwa wawili; kwanza ni kuchora picha au taswira ya hali halisi ya jambo na pili ni kupatanisha hali hiyo na maadili au funzo fulani linalokusudiwa katika jamii husika. Mfano; *Ngoja ngoja huumiza matumbo.* Katika hali hii ni wazi kusema kuwa, methali hutegemea mno uteuzi wa maneno na ujuzi wa kuyapanga vizuri ili yaweze kupatana na kufungamana bara'bara. Lugha teuzi inapotumika hulazimu kuchapua na kuyahusisha mazungumzo. Kwa anayezungumza, methali huakisi vyema mawazo yake na kumwezesha kuyatoa kwa busara wazi wazi. Kwa anayesikiliza, methali humzamisha katika mawazo ya kupima na kuchambua maana iliyokusudiwa na msemaji kutokana na kuyapatanisha maneno ya methali na ukweli ulio katika maisha.

Methali nazo huibuka kutokana na mawasiliano na mtagusano wa kila siku wa wanajamii kama vile katika shuguli za ibada, kazini, maeneo ya michezo na budrudani, harusi, usafiri na hata nyakati za huzuni na maombolezo. Kwa mfano; *Buyu kali ni dawa ya mwana mimba*. Methali kama zao la fasihi, hudhihirisha uhalisia ulio ndani ya jamii na kwa kiwango kikubwa hueleza maisha ya jamii husika.

Methali zimebeba majukumu tofauti katika jamii. Baadhi ya majukumu haya ni pamoja na kuelimisha wanajamii kama vile kwenye tamasha za jandoni na arusi kupitisha ujumbe na

maarifa ya kijamii kwa vijana. Pia methali husawiri mitazamo na falsafa za jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile jamii ina thamini nini, inachukia nini na kadhalika. Vile vile methali hutambulisha jamii kwani kila jamii ina methali zake. Kupitia kwa methali binadamu anaweza kueleza hisia zake, fikra na mawazo yake.

Katika taaluma ya Paremiolojia, kuna vigezo ambavyo hutumiwa katika uainishaji au upangaji wa methali katika vikundi vinavyohusiana. Kulingana na Wamitila(2003) anasema kuwa uainishaji ni ule upangaji wa makundi huku ukizingatia sifa fulani zinazolandana na zinazoweza kuwa mbinu za lugha zilizotumiwa au pia sifa fulani za kimtindo. Vigezo vinavyotumiwa kuainisha methali ni kama vile; kigezo cha kiuamilifu, kimuktadha, kimaana, kimuundo au kimtindo na kialfabeti.

## 1.2 Suala la Utafiti

Tafiti mbalimbali na hakiki nyingi zimefanywa katika methali na wataalamu wengi lakini kutokana na uchunguzi wangu wa tafiti za wataalamu hawa, hakuna mtaalamu yeyote ameshughulikia kipengele cha usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za lugha ya Kiswahili. Khatibu (2017) akichunguza methali katika jamii ya Wapemba aliangazia fani ya taswira pekee katika ujenzi wa dhamira katika methali za jamii hiyo na kwa hivyo akaacha mwanya wa uchunguzi wa fani zingine zinazounda methali hizo na uhusianao wa methali hizo na ugonjwa, uuguzi na tiba katika jamii hiyo. Oyaro(2019) akiangazia tasfiri za methali na misemao katika *Mshale wa Mungu* ameangazia methali kwa ujumla wake kama zinavyotumika katika kazi teule bila kuzingatia methali zinazolenga ugonjwa, uuguzi na tiba na kwa hivyo kuacha pengo tunaloshughulikia katika uchunguzi huu. Kwa hivyo, mwanya huu ulioachwa na wataalamu hawa kuhuzu usawiri wa ugonjwa uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili ndio unaotoa mshawasha na hamasa ya kufanya uchunguzi huu. Uchunguzi

huu anaangazia kwa kina vipengele vya fani vinatumika kwa njia gani kubainisha ujumbe ulio katika methali teule. Pili, ugonjwa, uuguzi na tiba hutumika kwa namna gani kuwasilishia ujumbe na athari zipi zinazoibuzwa na tatu, dhana ugonjwa uuguzi na tiba inaleta athari gani katika kuufasiri ujumbe wa methali teule. Utafiti huu una maana kubwa kwani utaongeza uhai katika methali za Kiswahili haswa zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Kwa kuwa methali ni mojawepo ya vipera vya fasihi ambacho ni muhimu kwa kutoa maadili kwa vijana na jamii nzima kwa ujumla, ni muhimu kuzilinda ili kudumisha maana yake muhimu. Hivyo basi methali zinafaa kutumiwa kwa kuangalia mjengo wake wa maneno kwa undani ili kuelewa ujumbe wake kwa kina. Utafiti huu ni wa manufaa mno kwa wasomi na wapenzi wa fasihi simulizi na andishi haswa wanopenda methali kwa kuwa umetoa mwanga wa kuzielewa na kuzielezea methali haswa za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Kwa waandishi wa fasihi, utafiti huu unawafaa pia kwa kuwa unawawezesha kuelewa jinsi ya kuutambua ujumbe wa ndani uliobebwa na methali hizi ili kuweza kuzitumia vifaavyo. Aidha utafiti huu ni wa manufaa kwa watafiti kwani wanapousoma wanakuwa katika nafasi bora ya kuwawekea msingi bora kwa kazi zao.

**1.3 Lengo kuu**

Azma kuu ya utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba yake katika methali za Kiswahili.

**1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu unajikita katika kuyafikia malengo mahsusi yafuatayo:

i) Kufafanua matumizi ya vipengele vya fani kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili.

Mount Kenya University

ii) Kudadavua matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili.

iii) Kutathmini athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu unadhamiriwa kuyatafutia majibu maswali ya utafiti yafuatayo:

i) Je, vipengele vya fani vinatumikaje kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili.

ii) Ugonjwa, uuguzi na tiba hutumikaje kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili?

iii) Je, usawiri wa magonjwa, uuguzi na tiba una athari gani kwa ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili?

**1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada**

Lugha ya binadamu huwa hai, kwa hivyo inaweza kukua, kudidimia na mwishowe kufa ama hata kubaki palepale bila mabadiliko mengi yanayoweza kudhihirika. Mabadililko hayo hutegemea mwingiliano wa wanadamu. Mabadiliko haya katika lugha huathiri muonolugha wa matumizi ya lugha fulani. Kwa msingi huu wa mabadiliko ya lugha haswa yanayoletwa na utandawazi ambao umeufanya ulimwengu kuwa kijiji, ni mawazo yetu kuwa methali za Kiswahili haswa zile zinazohusu usawiri wa ugonjwa, tiba na uuguzi zimeathirika vilevile. Lengo la utafiti huu ni kubaini methali hizi za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, tiba na uuguzi nazo zimechukua mkondo upi.

Mount Kenya University

Tafiti nyingi ambazo zimefanywa na wataalamu tofauti, zinabainisha waziwazi kuwa Kiswahili ni lugha inayokuwa na kupanuka katika matumizi yake kila kuchao. Baadhi ya watafiti waliofanya utafiti zao katika methali za kiswahili ni pamoja na Ndalu (1989), Andambi (2005), Wamitila (2001), Karama na Said (1983), King'ei na Ndalu (2008), Arege ( 2011). Linalobainika wazi katika kazi hizi za utafiti ni kwamba idadi ya methali za kiswahili inazidi kuongezeka kila kuchao. Mfano mwema ukiwa ule wa Wamitila (2001) aliyekusanya methali elfu mbili mia tisa na sitini na nne (2964) naye Arege (2011) akakusanya methali elfu tatu mia tano thelethini na tisa (3539). Kazi hizi zinaashiria kuwa methali za Kiswahili zinazidi kuongezeka. Hili linaashiria kuwa methali za Kiswahili zina umuhimu tosha katika maisha ya kila siku na matumizi yake bado yangalipo.

Utafiti huu ni wa manufaa kwa kuwa ni nyongeza bora juu ya tafiti nyingine zilizofanywa na wataalamu wengine hapo awali katika methali za Kiswahili hususan ambazo zinarejelea usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba. Kazi hii imechukua mkondo tofauti na uliochukuliwa na watafiti wa awali, kwani wao walichunguza methali zote katika ujumla wake. Utafiti huu unaangazia na kuchunguza kwa kina methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za lugha ya Kiswahili.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni ongezo la maana katika taaluma ya kielimu na taaluma zinginezo, haswa kwa walimu na wanafunzi vyuoni. Utafiti huu mfano mwema wa kielelezo cha kisingi kwa watafiti wengineo wanaonuia kuendeleza juhudi zao za kutafiti dhana za methali za Kiswahili. Wahadhiri na walimu wa vyuo vikuu na shule, wa fasihi simulizi wanaweza kuutumia utafiti huu kuandaa maalumati ya masomo yao.

Pia,  kukamilika kwa utafiti huu kunawajulisha vijana umuhimu wa methali ambao wanaona kama methali zimepitwa na wakati na  kuanza au kuzidi kuzitilia maanani. Baada ya kusoma machapisho kama haya ya kiutafiti watagundua methali za Kiswahili zinabeba ukwasi mkubwa wa amali za jamii kama busara na maadili. Kwa waandishi wa fasihi, utafiti huu unawafaa pia kwa kuwa unawawezesha kuelewa jinsi ya kuutambua ujumbe wa ndani unaobebwa na methali hizi ili kuweza kuzitumia vifaavyo. Aidha utafiti huu ni wa manufaa kwa watafiti kwani wanapousoma wanakuwa katika nafasi bora ya kuwawekea msingi bora kwa kazi zao.

Utafiti huu bado utakuwa rejeleo linalowafaa wadau wa taaluma ya fasihi ya Kiswahili haswa kipengee cha methali kulingana na utajiri mwingi  wa maarifa ulio katika methali hizi. Utafiti huu unatoa nafasi ya kuongeza maarifa ambayo inasongesha mbele taaluma ya fasihi kwa watafiti wengine , wanafunzi na walimu

Vile vile kukamilishwa kwa uchunguzi huu kunatarajiwa kuwafanya Waswahili na wapenzi wa Kiswahili kutambua kuwa methali zao ni tunu hata zinafanyiwa uchunguzi wa kina na wanafunzi wa vyuo vikuu. Hii italeta dhana ya kuzitambua na kuzithamini methali hizi na zilizofungamana na utamaduni wao.

## 1.7  Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Methali za kiswhili pekee ndizo zinazozingatiwa katika utafiti huu. Kwa kuwa mtafiti anaelewa upana na mipaka ya Kiswahili, anatumia tu vielelezo vya methali za Kiswahili vinazorejelea usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba. Utafiti huu unajikita katika msamiati unaorejelea ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiuswahili.

Baadhi wa methali ni visawe vya methali ambazo zitakuwa zishafafanuliwa kulingana na mpangilio wa kiabjadi( kialfabeti), kwa hivyo hazifafanuliwa tena ili kuepukana na hali ya kujirudiarudia. Pia kuna methali zaidi ya moja ambazo zinarejelea dhana moja kwa kutumia msamiati tofauti. Hili linapotokea maelezo ya msamiati ule hayarudiwi bali msomaji anaelekezwa katika methali inayotumia msamiati huo huo na tayari imeshashughulikiwa.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii inashughulikia misingi ya utafiti huu kwa kufafanua usuli wa mada ya utafiti ambayo ni usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, msingi wa uteuzi wa mada, umuhimu wa utafiti na hatimaye upeo wa mipaka ya utafiti huu. Sura ifuatayo inawasilisha mapitio ya maandishi.

Mount Kenya University

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Uhakiki wa maandishi pamoja na misingi ya kinadharia inayoongoza utafiti huu inawasilishwa katika sura hii ya pili. Kimsingi, mapitio ya maandishi yawasilishwayo yanatalii maandiko na taafiti zilizofanywa kuhusiana mada ya utafiti huu ambayo ni usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika kipera cha methali kwa jumla. Kwa hivyo, uhakiki wa mandishi unatekelezwa kwa mujibu wa matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani katika methali, matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilishia maana pamoja na kutathmini athari ya usawiri wa magonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili. Hatimaye, misingi ya kinadharia inafafanuliwa na hitimisho kuwasilishwa kama muhtasari wa yaliyomo katika sura. Hitimisho lenyewe linadhihirisha mianya, upungufu na/au mapengo katika maarifa yanayofidiwa na uchunguzi huu.

## 2.1 Matumizi ya Vipengele vya Fani katika Methali

Jilala (2008) anachunguza matumizi ya kipengele cha sitiari kwa kurejelea sitiari za Ukimwi na mapenzi katika mashairi ya Bongo Fleva nchini Tanzania. Uchunguzi wake unahusu kuchambua sitiari zinazotumika kumchora mwanamke katika mashairi haya, kujadili jinsi sitiari zinavyoakisi nafasi ya mwanamke katika jamii na kubainisha tofauti iliyopo baina ya mwanamke na mwanamume katika uteuzi na matumizi ya sitiari. Utafiti huu unabainisha au kumchora mwanamke kama chombo dhaifu cha kutumiwa na mwanamume katika starehe na mwanamke kama chombo tegemezi. Wanawake wanaonekana kudhalilishwa, kuonewa na kudunishwa kwa ujumla. Mwanamke anaonekana kama chanzo cha Ukimwi na anayetuimika

Mount Kenya University

kusambaza ugonjwa huu. Sitiari katika mashairi au muziki wa kisasa huakisi mielekeo duni ya jamii kumhusu mwanamke kwani katika jamii mwanamke huchorwa kitaswira na hupewa majukumu na nafasi inayomdunisha na kumdhalilisha. Uchunguzi huu unasaidia kumulika kipengele cha sitiari na jinsi kinavyojengwa katika kazi za mashairi ya kisasa. Utafiti huu unasaidia kuelewa kwa kina jinsi ya kuchunguza isitiari katika methali teule katika utafiti wetu.

Katika ujumla wake, fani ni ufundi wa sanaa inayotumika katika kazi za kifasihi. Vipengele vya fani vinavyoijenga kazi yoyote ya kifasihi ni kwa mfano lugha, tamathali za usemi, mandhari, wahusika, mtindo na muundo wa kazi inayohusika (Senkoro, 2011). Kwa hivyo, uchunguzi na uchanganuzi wa methali za Kiswahili unanuiwa kuonyesha namna ambavyo vipengele vya fani vinatumika kuwasilisha maana zake kwa kuurejelea ugonjwa, uuguzi na matibabu.

Naye Nsookwa (2011) analinganisha dokezo la sitiari zilizo katika methali za Kiswahili na zilizo katika methali za Kiganda. Mtaalamu huyu anaangazia sitiari kwa kina kwa urejelezi wa methali za Kiswahili na methali za Kiganda. Anachambua na kubainisha ishara zitokanazo na matumizi ya sitiari katika methali hizo. Matokeao ya uchunguzi wake yanadhihirisha kuwa methali za sitiari katika lugha mbili zilizo na mazingira yanayofanana, ishara zake hukita katika miktadha ya aina moja. Pili anagundua kuwa uchunguzi wa ishara hufuatilia utamaduni wa jamii husika na hatimaye methali za sitiari huwa na pande mbili. Hata hivyo, uchunguzi wake unahusu sitiari katika methali kwa ujumla wake bila kuzihusisha na ugonjwa, uuguzi wala tiba katika lugha mbili zinazochunguzwa - Kiswahili na Kiganda. Utafiti huu unasaidia kujaza pengo la maarifa linaloachwa kwa kuchunguza jinsi sitiari

pamoja na vipengele vingine vya fani vinavyotumika kudokeza, kuashiria na kuwasilisha maana na ujumbe unaohusu ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili.

Akichunguza mfanano na tofauti zilizo kwenye fani na pia kwenye maudhui katika methali za Kitanzania na Kilibya, El-jetlawiy (2013) anachukua mtazamo jumla wa kitaifa kuhusu mada hii. Ugunduzi wake ni kuwa, ingawa methali hizi zinatofautiana kimaudhui, zinafanana sana katika matumizi mbalimbali ya vipengele vya fani. Mtafiti huyu pia anazamia vipengele mbalimbali vya fani vinavyozijenga methali za mataifa yanayochunguzwa. Kwa kuitalii kazi hii, mtafiti anafaidi ujuzi mwingi unaohusu uchambuzi wa vipengele vya fani katika methali kwa jumla. Maarifa haya yanasaidia katika utafiti wetu kwa kuweka msingi na ufahamu wa jinsi vipengele vinavyochunguzwa vinavyooana na utafiti wetu kuhusu usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili zinazochunguzwa.

Akizamia katika uchunguzi wa usawiri wa ujinsia katika filamu haswa matumizi ya lugha katika filamu za Steve Kanumba, Suwed (2013), anabaini kuwa filamu za msanii huyu(k.s.t) zinatumia vipengele vya kejeli na dhihaka kwa kiwango kikubwa kuliko vipengele vingine katika kuchora na kusawiri suala la ujinsia katika jamii. Mtafiti huyu anagundua kuwa, kejeli inatumika katika kujenga tamathali zingine za semi  na kwa hivyo kejeli inatumika mno kama mbinu ya kisanii kuwasilishia ujumbe. Anasema kejeli huchangia hadhira katika kufikiria kwa kina juu ya yale yasemwayo, hadhira hupata nafasi ya kushiriki katika kazi za sanaa kwa kushangilia, kucheka, kupiga makofi na kukataa au kuitikia kwa kutumia masolugha na viziada lugha. Hili linatoa maana bainifu kwa mbinu ya kejeli na dhihaka husaidia kuonyesha hisia na mitazamo ya hadhira kuhusu kazi ya sanaa. Kazi hii inatupa mfano mwema wa matumizi ya kejeli katika kazi za kifasihi na ina tusaidia kuelewa kejeli na jinsi ya kuiangazia katika utafiti wetu.

Kombo (2014) anachunguza matumizi ya tamathali za usemi katika mashairi yanayohusu ugonjwa wa Ukimwi katika magazeti ya Kiswahili. Amebainisha kuwa tamathali za usemi zimetumika kuwasilisha dhamira tofauti tofauti. Aidha, anafafanua dhima za kifani na za kimaudhui zinazotekelezwa na tamathali mbalimbali za usemi. Ingawa uchunguzi wa Kombo haugusii methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa,uuguzi na tiba, ufafanuzi wake unaangazia matumizi ya vipengele vya tamathali za usemi katika kazi ya fasihi. Hata hivyo, unauelekeza uchunguzi wetu kwa mbinu zinazoufaa uchanganuzi wa vipengele vya tamathali mbalimbali za usemi katika methali za Kiswahili zinazohusu ugonjwa, uuguzi na tiba.

Kimambo(2015) akichunguza matumizi ya lugha katika riwaya za *Siri ya Maisha* na *Vipuli vya Figo*, anabaini mwandishi wa riwaya hizi ametumia vipengele vya fani kama tashibiha, kinaya, dhihaka sitiari, mshabaha na tashihisi kuchomoza dhamira katika kazi hizi. Dhamira kwa mfano elimu, siasa, biashara haramu, malezi katika jamii, na uchumi zinafungamanishwa na vipengele hivyo na hili linafanya zijitokeze kwa nama inayovutia na hili linampatia msomaji wa kazi hizi motisha wa kuzisoma. Ingawa utafiti wetu sio wa riwaya, uchunguzi huu unasaidia kuelewa mtagusano wa vipengele vya fani katika kazi za riwaya.

Kwa kurejelea methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe ambao huishi majini, Sito (2015) anachunguza athari zinazotokana na mazingira katika uteuzi wa msamiati kwa kurejelea methali za Kiswahili zirejeleazo viumbe wa majini. Anaonyesha jinsi mazingira yavyoathiri matumizi ya msamiati. Miktadha ya kijamii na mazingira asili yamethibitika kuwa muhimu katika uchambuzi na ufasiri wa maana na ujumbe uwasilishwao na methali inayohusika. Hata hivyo, utafiti wa Sito (keshatajwa) unaacha pengo la maarifa katika ufafanuzi wa athari ya

Mount Kenya University

mazingira katika ufasiri wa methali za Kiswahili zinazosawiri magonjwa, uuguzi na tiba. Mwanya ambao unanuiwa kuzibwa na utafiti wetu.

Oyinda (2016) anachunguza tasfida katika matibabu kwa kurejelea lugha ya Kiswahili na Kimarachi. Anaangazia tasfida kwa kuzingatia tiba, uasaji, ushauri nasaha na uhamasishaji. Tasfida imejitokeza kwa mapana katika lugha mbili zinazochunguzwa wanajamii wanaporejelea magonjwa, takamwili, sehemu za siri, kile kitendo cha uavyaji mimba, baadhi ya dawa zinazotumika kuwapa wagonjwa tiba na tendo la kuzini. Kazi hii ni kielelezo bora cha uchunguzi wa kipengele hiki cha fani. Isitoshe, tasfida ni mojawapo ya tamathali za usemi zinazoangaziwa katika kazi hii. Pamoja na kuchunguza lugha ya matibabu pia, Oyinda (k.s.t) anachunguza kwa kulinganisha kipera cha methali kwa ujumla katika jamiilugha ya Kiswahili na ya Kimarachi. Hata hivyo, uchunguzi wetu unaangazia usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili pekee.

Oyinda(2016) anatafiti jinsi kipengele cha tasfida kinavyojitokeza katika matibabu huku akilinganisha lugha mbili ambazo ni Kimarachi na Kiswahili. Anachunguza namna tasfida inavyotumika katika msamiati unaorejelea tiba, uasaji, uhamasishaji na katika kutoa ushauri nasaha. Matumizi ya kipengele cha tasfida hutumika zaidi na wanajamii katika lugha hizi mbili zinazochunguzwa wanaporejelea kitendo cha kuavya mimba, takamwili, majina ya sehemu nyeti, tendo la kuzini, baadhi ya magonjwa na katika baadhi ya dawa zinazotumiwa kuwauguza wagonjwa. Uchunguzi huu unatusaidia japo kwa kiwango kidogo kwa kuwa kipengele cha tasfida hakichunguzwa katika uchunguzi wetu.

Katika uchunguzi wake kuhusu usawiri wa mhusika wa kiume katika methali za Kimeru, Raymond (2016) anabainisha jinsi mwanaume ana

vyochorwa na kuchukuliwa katika jamii ya Wameru. Kwa kuwa jamii ya Wameru imeegemea upande wa kuumeni, methali nyingi anazochambua zinamtaja mwanamume kwa kumpa hadhi ya juu alinganishwapo na mwanamke. Anaendelea kufafanua dhima ya asasi mbalimbali katika jamii ya Wameru kama vile ndoa, utawala, tohara na kazi. Pamoja na tofauti dhahiri kati ya mifumo ya lugha ya Kimeru na Kiswahili, Njue (k.s.t) hajazamia suala la methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba bali masuala ya kijinsia. Hata hivyo, masuala ya kijinsia katika methali kwa ujumla yanaweza kuathiri uainishaji na mielekeo kuhusu ufasiri wa maana au ujumbe katika methali za Kiswahili zinazohusu magonjwa, uuguzi wake na namna yanavyotibiwa. Ingawa utafiti watu haujaangalia jinsi wahusika na uhusika wao unaathiri ufasiri wa maana katika methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba, umetoa mwanga wa jinsi ya kuchunguza malengo ya methali teule tunazochunguza.

Ali (2016) anachunguza vipengele vya fani pamoja na dhamira katika nyimbo za uganga za jamii ya Waswahili. Anafafanu jinsi ambavyo vipengele vya kifani viundavyo nyimbo hizo vinavyowezesha kuchomoza dhamira ambazo zinajitokeza katika nyimbo tofauti za uganga. Baadhi ya viepengele vya kifani anavyoangazia ni wahusika, lugha, tamathali za usemi na mazingira. Ijapokuwa utafiti huu haukujishughulisha moja kwa moja na utanzu wa methali za Kiswahili, unahitajika katika uchunguzi wetu kwa vile uonaonyesha jinsi vipengele mbalimbali vya fani hutumika kuuwasilisha ujumbe wa kazi za fasihi kwa ujumla.

Khatibu (2017) anaangazia matumizi ya taswira kama kipengele cha fani katika methali za Wapemba. Anadhihirisha taswira tofautitofauti zinazosaidia kujenga dhamira katika methali za Wapemba. Mbali na tofauti za kijamii, uchambuzi wa kipengele cha taswira ni muhimu kwa utafiti wetu. Ingawa mtafiti huyu anachunguza taswira kama kipengele cha fani katika methali, pengo la maarifa lingali lipo katika ufasiri wa taswira zinazosawiri ugonjwa, uuguzi

na tiba katika methali za Kiswahili. Hata hivyo, uchunguzi wetu umefaidi kwa kufahamu njia za kutambua, kuchumbua na kufasiri kipengele cha taswira katika kipera cha methali kwa ujumla.

Kitundu na Malangwa (2018) wakijikita katika uwanja wa semantiki, wanachunguza jinsi maana inavyojengeka katika vipengele vya sitiari na tashibiha. Wakichunguza mwingiliano wa elementi mbalimbali zinazojenga isitiari na tashibihi wanagudua kuwa kila kipengele kina maana yake tofauti. Isitiari hujengeka katika mwingiliano wa elementi tatu ambazo ni mada, kibebeo na sifabia ilhali tashbihi hujengwa kutokana na mwingiliano wa elementi tano ambazo ni mada, kibebeo, sifa au sifabia, kilinganishi pamoja na tendo. Utafiti huu uligundua kuwa elementi hizi husaidia katika ujenzi wa maana katika vipengele hivi husika. Utafiti huu umesaidia uelewa wa kina wa jinsi isitiari na tashbihi hujengwa kisemantiki. Hata hivyo utafiti huu haukutoa msaada katika utafiti wetu kwani utafiti wetu unazingatia isitiari zinazojitokeza katika methali teule bila kuzingatia semantiki ya isitiari zilizotumika katika methali teule.

Farida (2018) anachunguza sanaa na dhima katika methali za Wahaya. Anashughulikia matumizi ya lugha ya mafumbo, muundo, takriri, sitiari, tasfida na taswira katika methali mbalimbali za jamii ya Wahaya. Katika utalii wa kazi yake, anaonyesha jinsi anazishughulikia na kuziorodhesha dhima za methali za Wahaya kulingana na majukumu yake mbalimbali kama vile dhima ya kukuza lugha, kupatanisha jamii, malezi ya watoto, kuhimiza umoja, kuonya, kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii, kuburudisha pamoja na dhima nyinginezo. Pamoja na hayo, mtafiti anafanikiwa kuchunguza vipengele vya kifani na kugundua kuwa kuna matumizi mengi ya vipengele mbalimbali vya fani vinavyotumika katika methali za Wahaya. Mataalamu huyu (k.s.t) anaweza kubainisha takriri ya maneno

katika methali ambayo hutumika huleta msisitizo wa jambo. Pia kuna matumizi ya tashbiha au mshabaha ili kulinganisha dhana mbili zinazobebwa na methali fulani. Tashihsi , isitiari, kejeli na tasfida pia zinatumika kwa wingi katika methali hizi za Wahaya. Matumizi ya taswira pia yanaangaziwa kwa kina kirefu kwani mtafiti huyu( k.s.t) anachunguza taswira zinazojitokeza katika methali hizi kama vile; taswira za wanyama, taswira za matunda, taswira zinazazotokana na mazimwi, nyoni, wadudu, makao, silaha na hatimaye taswira za viungo mbalimbali vya mwili. Kwa kuwa utafiti huu unaangazia fani mbalimbali zitumikazo katika methali za Wahaya, kazi hii inamsaidia sana mtafiti kuweka msingi dhabiti wa utafiti wake katika kuangalia vipengele vya fani ambavyo vinatumika katika methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Ibrahim, Nyandiba na Mohochi (2021) wanashirikiana kuchunguza nafasi ya fani katika fasihi ya watoto ili kufanikisha maudhui wakiongozwa na riwaya mbalimbali za Kiswahili. Lengo lao lilikuwa ni kuangazia kwa kina na kuainisha vipengele vya fani vitumikavyo katika fasihi ya watoto. Watafiti hawa walichunguza mbinu ya picha kama kipengele cha fani katika fasihi ya watoto na mwingiliano uliopo baina ya picha na vipengele vingine vya kifani. Watafiti hawa (k.s.t) waligundua kuwa vipengele vya fani kama vile tashbihi, misemo,nahau, methali na taswira jinsi zinavyofungamanishwa na picha ili kutoa maana inayokusudiwa na kufanya maana katika riwaya za watoto kueleweka kwa urahisi na hadhira lengwa ambayo ni watoto. Kazi hii haikumpa mtafiti usaidizi tosha kwani inaangalia fani katika riwaya za watoto, uzito wa uchunguzi wake ukiegemea sana katika picha na muoano uliopo baina ya picha na fani nyinginezo za kifasihi. Hata hivyo mtafiti alipata mwanga wa jinsi vipengele hivi vya kifani vinavyofaa kuchunguzwa kati utafiti wake haswa kipengele cha taswira kinavyojengeka katika picha.

Mount Kenya University

Awhida (2021) akichunguza jinsi lugha ilivyotumika katika tamthiliya ya *Sadaka ya Okello* anaangazia matumizi ya tamathali za semi zilizotumika kuijenga tamthiliya hiyo. Ameangazia tamathali za usemi mbalimbali zinazojitokeza katika tamthiliya hiyo na kuonyesha uhusiano wake katika ujenzi wa dhamira ya kazi nzima. Ingawa kuna tofauti za kitanzu kati ya uchunguzi wa Awhida na wetu, methali ni kipera cha semi kitumiacho lugha banifu ambayo aghalabu huwasilishwa kwa matumizi ya tamathali hizo za usemi. Uchambuzi na uchanganuzi wa tamathali za usemi mbambali umeelekeza utambuzi na udadavuzi wa tamathali za usemi zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili.

Hamad (2022) akichunguza dhamira na matumizi ya lugha akirejelea nyimbo za ngoma ya msewe wa kambini kichokochwe, anabaini kuwa nyimbo hizi zinatumia vipengele vya fani kama vile tashihisi, kejeli, balagha, taswira na takriri katika kusuka ujumbe wa nyimbo hizo.

## 2.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Maana

Methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zimesheheni jumbe tofauti ambazo huibua maana mbalimbali. Akichunguza nyimbo za matambiko ya uponyaji katika jamii ya Watumbuka nchini Malawi, Waterman (2009) anagundua kuwa waganga wa jamii hiyo hutumia ngoma na uchezaji kama njia mojawapo ya kuuguza na kutibu magojwa tofauti tofauti. Mganga au mponyaji hucheza ngoma kwa madhumuni ya kutuliza mizimu ili iweze kuwajulisha chanzo cha ugonjwa unaomwathiri mtu na hivyo kufanikisha matibabu. Mizimu nao hutumia ishara fulani kuwasiliana na mganga. Hatimaye, mgonjwa anaweza kuponywa ugonjwa aliougua. Maelezo haya kuhusu nyimbo za matambiko yanaashiria kwamba nyimbo, ngoma na uchezaji zinaweza kutumika katika utambuzi, uuguzi na matibabu ya magonjwa yanayoinukia. Pamoja na kutalii uhusiano uliopo baina ya nyimbo, ugonjwa, uuguzi na tiba, Waterman (k.s.t) pia anaonyesha matumizi ya ishara za kimawasiliano baina ya waganga na

mizimu. Methali pia hutumia vipengele vya fani na ishara za kiisimu kuwasilisha maana na ujumbe wake. Uchunguzi huu unadhihirisha ya kuwa nyimbo hubeba maana ya ndani ambayo husaidia katika kutoa matibabu kwa wawele. Uchunguzi huu umefaidi uchunguzi wetu kwa kuwa unatoa mwanga ya kwamba kunao ujumbe maalum uliyobebwa na methali teule zinazochunguzwa.

Mutembei (2009) anaangazia ugonjwa wa Ukimwi katika mashairi ya Kiswahili. Anaeleza kwamba ugonjwa huu umesababisha vifo vya watu wengi nchini Tanzania. Anachambua mashairi ya Kiswahili yaliyotungwa na kuchapishwa tangu kuzuka kwa ugonjwa huu barani Afrika 1986 hadi 2006. Utafiti huu unadhihirisha kuwa ushairi wa magazetini una uwezo mkubwa katika kueleza na kuweka wazi mambo mengi yanayohusiana na ugonjwa wa Ukimwi. Mashairi haya ambayo ni machapisho katika magazeti ya wakati ule yaliangazia jinsi jamii ilivyoambukizwa ugonjwa huo, njia mbalimbali za kujikinga na unyanyapaa kwa wagonjwa na jinsi au njia za kujikinga na ugonjwa ule kwa binadamu. Kwa hakika machapisho hayo yana mchango tosha katika kutoa maelezo yahusianayo na ugonjwa huu wa Ukimwi. Kazi hii inaashiria usawiri wa ugonjwa na tiba yake katika mashairi ambayo ni kazi moja ya kifasihi.

Anapochambua jamii ya Waswahili na itikadi zilizo katika jamii hiyo, Sengo (2011) anaeleza kuwa uganga wa kale ni taasisi iliyo hai katika maisha yao. Akigusia ngoma mojawapo inayoitwa *Pungwa*, anasema haikuwa ngoma ya kawaida bali ilikuwa kama uganga wa kishetani. Wimbo huu ulikuwa unachezwa na waganga mara nyingi wanapofanya matambiko ya uuguzi ili kutoa tiba kwa wanajamii waliouugua. Anaendelea kusema kuwa wawele huweza kuimbiwa nyimbo kama sehemu ya tiba ili wapone. Sengo (k.t.j) amegundua jinsi ngoma za Waswahili hutekeleza dhima za kimawasiliano kuhusiana na ugonjwa, uuguzi na

tiba. Hili linatujengea uelewa wa uhusiano uliopo kati ya nyimbo kama vile *Pungwa* na methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Isitoshe, baadhi ya methali hizi hutumika kama nakshi katika mashairi ya nyimbo.

Akitafitia nyimbo za uganga pia, Haji (2011) anaeleza kwamba nyimbo za uganga hutumika kupandisha mizimu kichwani mwa muwele. Mizimu inapopandishwa kichwani kwa nyimbo, huweza kuongea na mganga. Kupitia mawasiliano haya muuguzi hutambua ugonjwa wa mhusika na kuweza kumtibu. Uganga ulikuwa ni taaluma ambayo ilikuwa inafanywa na wazee katika jamii ambao wako na tajriba ya kutosha kuwasiliana na mizimu ili waweze kutoa matibabu yao. Matibabu haya hufanywa kwa njia ya siri na hutendeka katika mandhari maalumu, hasusan sehemu iliyo na giza ili mizimu wasionekane wanapowasilisha ujumbe. Yamkini, usiri unaozingira mawasiliano haya ndio unaopelekea ufumbaji wa maana zinazowasilishwa na methali za Kiswahili zinahusu ugonjwa, uuguzi na tiba pia. Uchunguzi huu unatoa mwanga pia katika uchunguzi wetu kuwa methali teule zimesheheni ujumbe maalum kwa jamii ya Waswahili.

Asha na Fatma (2012) wametazama athari zinazoletwa na uchawi katika jamii ya Wazanzibari. Madhumuni ya utafiti huu ni kutoa tiba inayoweza kuuguza magonjwa yanayosababishwa na uchawi. Wawili hawa wanasema ili kuuguza waliougua kutokana na athari za uchawi huhitaji kuuguzwa kwa nguvu zile zile za mizimu. Mgonjwa anahitaji kufanyiwa matambiko na mganga ili mizimu inayosababisha magojwa iweze kutolewa katika mwili wa mgonjwa na basi akapata nafuu. Kazi hii inaashiria zaidi tiba zinazotokana na uchawi katika jamii zinazojihusisha na tamaduni hizi. Kazi hii imefanikisha uelewa wa ishara na uashiriaji unaohusiana na ugonjwa, uuguzi pamoja na tiba katika jamii ya Pwani kwa ujumla.

Shemweta (2015) anafanya utafiti ambao ni ulinganishi wa ngoma mbili ambazo ni ya *Ng'wanamalundi* na ya *Fumo Liongo* kwa kurejelea tamthiliya ya Mbogo, huku akizingatia itikadi zinazojitokeza katika kazi hiyo. Chidama ayelikuwa mwenye itikadi za uchawi na ushirikina, aliaminika kukadamiza watu kwa uchawi kwa kuwafanya misukule huku akiwatumikisha. Mtafiti huyu anasema kuwa uchawi hutumika katika kuuguza watu ama kuwafanya wafe.

Ali (2016) anawasilisha maelezo kuhusu nyimbo za uganga za Wazigua na Wazaramo. Anafafanua umuhimu wa nyimbo katika matambiko na uganga wa jamii hizi. Wawele wanapopewa huduma za uuguzi na tiba huhitajika kurudia maneno ya nyimbo mbalimbali ziibwazo na muuguzi. Nyimbo hizi hutuliza mizimu na wagonjwa hutibiwa kutokana nazo. Kazi hii inaashiria dhima ya nyimbo katika uuguzi na matibabu ya wagonjwa katika utamaduni wa Wazigua na Wazaramo. Mbali na kusawiriwa katika nyimbo za matibabu, yawezekana pia hali hizi hutekeleza dhima za kimawasiliano katika tanzu na vipera vingine vya fasihi, methali za Kiswahili zikiwemo. Ingawa uchunguzi wetu hauhusu nyimbo, utafiti huu unatoa mfano mwema wa jinsi kazi za fasihi husheheni ujumbe ambao hueleweka na jamii husika.

Katika utafiti wake wa nyimbo za uganga katika jamii ya Waswahili wa Pemba, Ali(2016) aneleza kuwa nyimbo za uganga huwa na siri kubwa katika jamii. Siri yenyewe inahusu utoaji wa tiba. Mganga husaidiwa na watumishi wake kutekeleza kazi ya kumpa muwele tiba. Mganga hutumia majani yakishirikishwa na fani ya kilinge ambayo hutoa mchango katika kumsaka jini aliyesababisha magonjwa kwa muwele ili kushirikiana kutoa tiba. Maleba huwa ni ya muhimu katika kuuguza na mganga huvalia maleba meupe, na watumishi wake vilevile ilhali mgonjwa anayehitaji kupewa tiba huvalia maleba ambayo ni mchanganyiko wa

Mount Kenya University

wekundu na weupe. Usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba unajitokeza katika utamaduni wa Wapemba kupitia kwa nyimbo zilizoshirikishwa katika kutoa uuguzi na tiba na waganga katika jamii hiyo. Kazi hii inaweza kutoa ithibati tosha kuwa ugonjwa, uuguzi wake na hata tiba zinaweza kutumiwa kuashiria dhana tofauti. Isitoshe hata maleba yaliyovaliwa na mganga na mgonjwa yalibeba ujumbe fulani unaohusiana na ugonjwa, uuguzi na tiba.

Naye Natalia (2019) katika utafiti wake wenye mada ya Tiba ya muziki, anaangazia jinsi ya kupunguza mafadhaiko kwa watoto kwa kutumia tiba ya muziki. Anashauri matumizi ya muziki kama njia bora ya kutoa matibabu ya magonjwa ya kisaikolojia, kupotoka kwa tabia na hata kurekebisha upotovu wa kihemko. Anafafanua kuwa Hippocrates na Pythagoras walitumia muziki kuponya nafsi na miili yao. Mtafiti huyu ameangalia jinsi muziki huathiri mwili wa mwanadamu kwa kuzingatia vipengele vya muziki kama vile mdundo. Amezungumzia njia halisi na mbinu mbalimbali za tiba kwa magonjwa mbalimbali kama vile mbinu ya tiba ya mchezo, mafunzo na mazoezi, tiba ya rangi, tiba ya sanaa, mbinu ya matibabu ya sauti (*vocalotherapy*). Kazi hii inasawiri ugonjwa, uuguzi na tiba katika muziki wa watoto.

## 2.3 Ufasiri wa Maana katika Methali

Karama & Saidi (1983) wanazitalii methali za Kiswahili kwa kuzikusanya na kuzichanganua kimaana na matumizi yake. Hata kama zimepangwa kwa kufuatilia mkondo wa kialfabeti, kazi hii haijazitolea methali hizo maelezo ya kina kwa kuzingatia methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi, na tiba. Vile vile vipengele vya fani vinavyotumika kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili havijashughulikiwa.

Methali huwa na sifa bainifu kama vipera vingine vya fasihi simulizi. Methali ni usemi mfupi ambao unaurari wa silabi au maneno na hutumia maneno yaliyomepesi na ya kawaida ili iwe rahisi kwa wanajamii kuielewa kwa urahisi ili usemi huu ukubalike na kundi la watumiaji wa lugha husika au wanajamii. Maneno yanayotumiwa humtia msikilizaji katika hali ya kufikiria baada ya kusikiliza, kuchambua na kwa hivyo kupata ukweli au maana ya ndani inayokusudiwa na jamii inayohusika (Mtesigwa, 1989).

Katika uchunguzi wao, Njogu & Chimerah (1999) wanabaini kuwa kwa mujibu wa muundo na msamiati teule unaotumiwa kuunda methali, mtu anawezadhani ya kwamba methali ziliundwa na wasomi na kumbe ziliundwa na wazee wa kawaida. Hili linadhihirisha uwezo walionao wazee na ujuzi mkubwa walionao na unaofaa kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Wamitila (2001) anazingatia sifa nyingine ambayo hujenga methali ambayo ni mbinu ya ushairi. Anasema kuwa baadhi ya methali huchukua mizani inayotoshana katika pande mbili za methali na methali zingine huuundwa kwa vina vinavyofanana vya katikati na vya mwisho kwa kila upande wa methali. Kwa mfano, *Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*. Mpangilio huu wa vina huleta mdundo katika methali ambayo huvutia na kutia radha katika methali. Matumizi mbalimbali ya tamathali za usemi katika methali za lugha ya Kiswahili pia yameshughulikiwa na mtaalamu huyu(k.s.t) ambapo anaangazia matumizi ya tamathali hizi kama vile sitiari, chuku, taswira, uradidi na zinginezo. Tamathali hizi za usemi hujitokeza kwa mno katika methali zote za Kiswahili. Kwa mfano, *Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini* (uradidi) pamoja na *Hapana jeraha bila silaha; Hapana uchungu usiotulia; Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi; Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha* na *Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda* (taswira).

Mphande (2001) anayezitafiti methali za jamii ya Tonga nchini Malawi, anasema kuwa methali ni kipera kinachopewa nafasi kubwa na wanajamii ili kutoa elimu kwao. Anabaini kuwa methali katika jamii hii hutumiwa zaidi na wazee kuliko vijana na hili linaweza kuleta hatari ya kufifia kwa kipera hiki. Hili linadhihirisha umuhimu wa methali kwa jamii kwani ni bayana kuwa methali katika jamii zote hutumika katika kutoa elimu kwa wanajamii kuhusu mambo tofauti katika jamii husika. Maitaria (2012) anashandidia hili kwa kusema kuwa methali ni kipera katika utanzu mkuu wa semi katika fasihi simulizi ambacho hubeba masuala tofautitofauti yanayohusiana na jamii fulani bali na kuwa huandikwa katika sentensi moja fupi.

Wamitila (2004) anasema kuwa kipera hiki cha methali ni kati ya vipera ambavyo hujitokeza sana katika jamii nyingi duniani na hutambulika kwa urahisi kutokana na muundo wake, lugha inayotumika kuziunda na maudhui yake. Muundo wa methali huweza kutumia mbinu mbalimbali za lugha kama vile taswira, ishara, uhuishi na vinginevyo. Pia hutumia muundo wa kishairi ambapo sauti au maneno fulani katika methali huimbua mudundo fulani wa kishairi kwa kurudiwarudiwa. Muundo huu husaidia kukumbukika kwa methali hizi kwa urahisi na upesi. Taaluma inayohusika na uchunguzi wa methali huitwa paremiolojia.

Nao King'ei & Ndalu (2008) katika kamusi yao ya methali za Kiswahili wanatoa kijelezi cha methali kuwa ni usemi mfupi uliosheheni maana iliyopana, uliobeba busara na hukita mizizi katika jamii inayohusishwa nazo. Wataalamu hawa wanazidi kuangalia umuhimu wa methali katika fasili yao kwa kusema kuwa methali huelimisha, huasa au hukebehi watu katika jamii au vitendo fulani visivyoendana na madili katika jamii kwa njia iliyo na tasfida au

Mount Kenya University

iliyofumbwa. Azma yetu ni kuchunguza namna ambavyo methali za kiswahili zinazohusuhu ugonjwa, uuguzi na tiba hutekeleza dhima hizi.

Katika kazi yake nyingine, Wamitila (2008:204) anaangazia sifa za methali. Anaeleza kuwa methali huwa na sifa ya wingi-hali yaani muundo wa methali huonekana kuwa na hali ya wingi ambao kimantiki unajitosheleza na pia methali huwa na wingi wa dhamira. Hii ina maana kuwa methali moja huweza kusheheni au kubeba dhamira tofauti tofauti. Sifa ya tatu ambayo mtaalamu huyu ameshughulikia ni sifa ya matumizi ya fomyula. Methali huwa na fomula maalum ambayo hutanguliza kabla ya methali yenyewe kutolewa kama vile "Wasawahili hawakukosea waliposema kuwa ...", au "wahenga walisema kuwa ...". fomyula hii huwezesha kuleta umakini na mvuto wa hisia za anayesoma ama kusikiliza kipera hiki cha methali.

Akimnukuu Simiyu (2013), anasema kuwa methali ni semi fupi ambazo huwa na umbo maalum na husheheni fumbo fulani linalohusu ukweli wa maisha ya binadamu. Mafumbo haya ya methali lengo kuu ni kufikisha ujumbe kwa walengwa bila ya kuwakwaza. Azma yetu ni kudadavua mafumbo yanayotumia ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilisha maana katika methali za Kiswahili zinazochambuliwa

Sito (2015) anachunguza methali kwa kuzingatia athari za mazingira katika uteuzi wa msamiati. Mtafiti huyu anaangazia sifa mbalimbali za methali za kiswahili kwa ujumla wake. Kwanza anaangazia sifa ya uwili. Hii ina maana ya kwamba kila methali hubeba maana ambayo ni rahisi kuielewa na ambayo hueleweka kutokana na maneno yaliotumika katika methali hiyo. Maana ya pili huwa ni batini au ya ndani. Ili kuelewa maana batini, msikilizaji huhitajika kufikiria zaidi ndipo aweze kupata maana ya ndani ambayo huwa na uzito na funzo linalotarajiwa kupashwa msikilizaji. Wamitila (2001) anazungumzia sifa hii ambayo

hujitokeza aghalabu katika methali zote za Kiswahili. Mifano ni pamoja na: *Kuzuia - ni bora kuliko kuponya; Maneno mengi - maradhi; Mapenzi kikohozi- hayawezi fichika; Mkimbilia sheria - hujiponya* na *Mwana kidonda- mjukuu kovu.*

Hatibu (2017) akichunguza dhima za methali zinavyoendeleza elimu ya jadi anasema kuwa, methali hupokezanwa katika jamii kutoka kwa kizazi kimoja hadi kizazi kile kingine. Hii ina maana kuwa methali nyingi zina ukale wa maana na maneno yaliyotumika katika kuziunda methali hizi. Hili hujitokeza kwa sababu, zimekuwa zikitumika kwa kipindi kirefu sana bila mabadiliko yoyote ya miundo yake na mpangilio wa msamiati wake. Sifa hii bado hujitokeza katika methali nyingi za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Mathalan, *Maradhi huja shoti yakitoka, ni mtambao wa kinyonga.* Katika methali hii, neno 'shoti' lina maana 'haraka' ilihali neno 'mtambao' wa kinyonga lina maana ya 'polepole'. Haya ni maneno ya kikale na kwa kuwa methali hupashwa kizazi kimoja hadi kingine bila kubadilisha msamiati wake basi maneno haya yanabaki pale bila kuyabadilisha kwa kutumia msamiati wa kisasa.

TATAKI (2019) wanaeleza methali kuwa ni usemi ambao ni wa kisanii na ulio wa wakimapokeo na unaofikiriwa na jamii husika kuwa wa ukweli na mara nyingi jamii hutumia semi hizi kufumba jambo fulani ama kulitolea mfano na husheheni maana iliyopana zaidi yale maneno yanayotumika kuiunda methali yenyewe.

Sifa nyingine inayoshughulikiwa na mtaalamu Wamitila (k.t.j) ni mkato na ufupisho wa muundo wa methali. Anasema kuwa, methali hutumia maneno machache ambayo husaidia kurahisisha maelezo. Sifa hii huokoa muda kwani maneno machache hutumiwa kuwasilisha ujumbe mrefu ambao ungewasilishwa kwa muda mrefu na kwa maneno mengi kama ingetumiwa maneno ya kawaida. Mifano ni kama vile: *Daawa si dawa; Dawa ya moto ni moto; Mganga hajigangi* na *Tabibu hakingi ajali.*

Wamitila akiendeleza utafiti wake anashughulikia sifa ya uchache wa maneno katika methali. Ingawa methali huwa na maneno machache kama mafumbo, methali hueleza maana kikamilifu kwa kufafanua hoja fulani na kuitolea jawabu au suluhisho hoja hiyo. Sehemu hizi mbili huwa zinajitokeza kama swali na jibu katika methali. Kwa mfano,

1) *Kipya kinyemi - ingawa kidonda*
2) *Kiendacho kwa mganga - hakina marejeo*
3) *Kidole kimoja kikiumia - chenzake chapwita.*

Methali hizi zina sehemu mbili kila methali. Methali ya 1 imegawika katika sehemu ya (a) ambayo ni *kipya kinyemi* na sehemu ya (b) ambayo ni *ingawa kidonda.* Baadhi ya methali pia huwa na sifa ya kuuliza swali lisilohitaji jawabu la papo kwa hapo. Sifa hii katika methali humwacha msikilizaji katika hali ya taharuki na huhitaji kufikiria ili ajue maana ya ndani ya methali husika. Mifano; *mavi usioyala wayawingiani kuku?* au *Pilipili usioila yakuwashiani?*

Kwa mujibu wa mapitio ya kazi za wataalamu hawa wote, imethibitika kwamba wanaafikiana kuwa methali ni usemi mfupi ulio na fumbo ambalo huhitaji weledi wa msikilizaji katika jamii inayohusika ili kuelewa maana ya fumbo la methali. Wataalamu hawa pia amekubaliana kuwa baadhi ya umuhimu wa methali katika jamii ni kuonya, kuelekeza, kuadilisha kufunza au kuelemisha jamii.

### 2.4 Misingi ya Nadharia

Steiner na Bailey hutoa maelezo kuwa semiotiki ni mchakato ambao hutambulisha matukio au vitu kama ishara au viumbe hai na vilivyo na hisia za kibinadamu. Mwanafalsafa kutoka Italia, Umberto Eco, anasema semiotiki huhusishwa na vitu vyote vinavyoweza kuchukuliwa kuwa ishara. Semiotiki kama taaluma ya kisayansi hushugulika katika kuchunguza na kuchanganua mfumo wa ishara tofauti tofauti huku ikizingatia mno uhusiano uliopo baina ya kile kinachotumika kama kiwakilishwa na kinachotumika kuwakilisha (Massamba, 2004).

Mount Kenya University

Njogu & Wafula (2007) wanasema semiotiki ni taaluma ambayo humsaidia binadamu ili aone hali mbalimbali na vitu tofauti kama ishara zilizo na maana kutokana na mpangilio wa ishara zinazorejelewa. Nadharia hii iliasisiwa na Ferdnand De Saussure na Charles Pierce katika miaka ya 1970 pamoja na wataalamu wengine akiwemo Noam Chomsiky ambapo wataalamu hawa walikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuwa nadharia ya umuundo ilikuwa imetumika kuhakiki kazi za fasihi miaka ya hapo awali.

Sengo (2009) anasema nadharia ni mwelekeo mkuu anaoutumia mtu binafsi au wa jamii fulani wa mahala na wakati au pia laweza kuwa ni wazo kuu la kumwongoza mtu. Mtafiti katika kazi hii anaongozwa na nadharia moja ambayo ni nadharia ya semiotiki inayomwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake. John Selden anasema *'semeion'* ambalo ni neno la Kigiriki ndilo msingi wa neno *semiotiki* linalomaanisha ishara na ambalo huwakilisha makundi ya wafuasi wa mielekeo fulani katika kazi ya uhakiki. Maana hii haina tofauti kubwa na iliyotolewa na Wamitila (2003) anaposema neno '*semeotiki'* ni neno lililo na msingi wake katika lugha ya Kiyunani na linalomaanisha ishara na ambalo hutumiwa kueleza misimamo ya makundi fulani katika uhakiki.

Nadharia hii huhusika katika kuchunguza lugha ya ishara, taswira, picha na mafumbo inayojengeka katika fasihi. Saussure katika nadharia hii anaeleza nafasi inayochukuliwa na ishara kwa jamii naye Pierce anaelezea uhalisia wa maana unaotokana na lugha ya ishara na inavyohusiana kidhamira kulingana na utamaduni wa jamii lengwa kwa makusudi ya kutoa maana lengwa.

Nadharia hii inauhusiano wa kiasi cha juu na nadharia ya umuundo. Semiotiki inarejelea vipashio vya lugha na ishara zake ilhali nadharia ya umuundo hujihusisha na jinsi utaratibu wa ishara unavyowekwa ambao huziwezesha ishara zenyewe kueleweka na wanajamii.

Semeotiki ni nadharia ya kimuundo ambayo hujishughulisha na ishara na kisha maana zinazobebwa na ishara hizo katika fasihi (Wamitila, 2003)

Wamitila (2002) anaeleza kuwa nadharia hii hutumika zaidi katika kuchambua kazi za kifasihi, ambapo hushughulikia ishara za lugha na uashiriaji wake. Katika lugha yoyote kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja, ambalo ni umbo ambalo alama inachukua na kitajwa au kirejelee yaani maana inayowakilishwa na alama hiyo. Hii inamaanisha ya kwamba hakuna uhusiano ulioko wa moja kwa moja kati ya kitaja na kinachotajwa/kirejelee bali uhusiano uliopo baina ya vitu hivi viwili ni wa kubuni hutegemea utamaduni wa jamii rejelewa. Kunauwezekano mkubwa kuwa hakuna uhusiano uliopo kabisa baina ya kitaja na kitajwa lakini kama matumizi yake wamekubalianwa na wanajamii basi hutumika na hilo huleta malewano miongoni mwa wanajamii hao. Wamitila (k.s.t) anaelezea zaidi ya kwamba, matumizi ya ishara yanayoundwa na mtunzi wa kazi ya fasihi ni lazima yalingane na mazingira ya jamii ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni.

Nadharia ya semiotiki hujengeka katika mihimili mitano kimsingi. Nayo ni muktadha, ujumbe, msemaji, mpokeaji na lugha na ndio hutumika katika kuzielewa ishara zilizotumika katika fasihi. Nadharia hii imejengeka katika misimbo ya aina tano ambayo ni Kihemenitiki, Kiseme, Kirejelezi, Kimatukio na Kiutamaduni/kiishara (Barthes, 1994). Misimbo hii iliyoasisiwa na mtaalamu huyu huwa ni baadhi ya nguzo imara za nadharia hii ya semiotiki. Barthes aligawanya kazi ya fasihi katika leksi, ambavyo ni vitengo vidogovidogo vilivyo na urefu unaotoshana. Kila leksia ilionyesha kaida yake muhimu inapofasiriwa. Barthes alifafanua aina tano za misimbo kama vifuatavyo:

Msimbo wa Kiutamaduni/Kiishara. Huu huhusishwa na jinsi wasomaji wa kazi ya fahisi wanavyofumbua maana za ishara. Anayetunga kazi ya fasihi huimarisha dhamira yake kutokana na vionyeshi vya kiutamaduni.

Msimbo wa Kiseme. Msimbo huu pia unasaidia katika kujenga nadharia ya semiotiki. Nao huu msingi wake uko katika tawi la kiisimu lijulikanalo kama semantiki ambalo hushughulikia maana zinazobebwa na maneno katika lugha (Mark, 1995). Elementi nasibishi za kisemantiki katika msimbo huu huelezwa ambapo picha ya mhusika fulani hutolewa katika kazi ya fasihi. Maneno fulani yanatumiwa lakini yanarejelea maana tofauti na ile ya kisemantiki.

Msimbo wa Kihemenitiki. Unahusu taharuki na usimulizi na unaweza kuonekana wazi wazi katika anwani ya kazi ya fasihi kama vile jina la wimbo, shairi, jina la sura katika tamthilia na hadithi, onyesho katika tamthilia na maigizo (Nazarova, 1996)

Msimbo wa Kiurejelezi. Msimbo huu hujengeka katika kazi ya kifasihi wakati ambapo viashiria vya kiutamaduni hurejelewa. Uelewa wa ujumbe huwa rahisi wakati ambapo vitu fulani vinavyoeleweka na watu wenye utamaduni fulani kuelezea jambo fulani kutoka katika fasihi.

Msimbo wa Kimatukio. Huu msimbo unahusu namna matukio ya hadithi yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyoyaunda na kuelewa ploti ya kazi ya fasihi.

Nadharia hii inaendana na mada ya utafiti huu kwani methali nyingi zinatumia lugha yenye taswira, mafumbo, ishara na picha ili kufikisha ujumbe fulani wa jamii husika. Hii ina maana kuwa kinachosemwa katika methali fulani chaweza kuwa sio kile kinachojitokeza wazi wazi katika msamiati uliotumiwa ila chaweza kuwe kitu au jambo lingine tofauti mno na

Mount Kenya University

kinachorejelewa. Kuna uwezekano wa anayetoa methali akatumia usawiri wa maradhi fulani lakini kirejelewa kikawa ni kitu tofauti na yale maradhi yanayorejelewa katika methali husika. Methali nyingi kwa kuwa zimefubwa na misimbo inayojenga nadharia ya semiotiki, basi imesaidia mtafiti kwenye uchambuzi wa methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Sababu kuu ya kuteua nadharia hii ya simiotiki ni kwa kuwa itasaidia katika kutosheleza malengo ya utafiti huu. Nadharia hii inafaa zaidi katika kuchanganua ishara za lugha zinazojitokeza katika methali teule. Misimbo ya nadharia hii inayotumika ni msimbo wa kiseme, msimbo wa kimatukio, pia msimbo wa kiishara na hatimaye msimbo wa kitamaduni unahusishwa. Misimbo hii minne inasaidi kubainisha tamathali za lugha kupitia viashiria vya kitamaduni, tukio na vionjo. Msimbo wa kihemenitiki hautashusishwa katika utafiti huu kwa kuwa unaenda kinyume na malengo ya tasnifu hii. Hili linatokana na sababu kuwa msimbo huu umejikita mno kwa kuangazia anwani za kazi za kifasihi kama vile jina la sura katika riwaya, jina la onyesho au sehemu katika tamthilia au mada ya ushairi.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii dhana mbalimbali zilizo na umuhimu mkubwa kwenye utafiti huu zimeelezewa. Umuhimu wa methali na matumizi yake na watu unabainika wazi kutokana na tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa na wanaparemiolijia mbalimbali waliokusanya methali na kuziainisha kwa njia tofauti tofauti na wengine kuzieleza kwa kina kimatumizi na sifa zake mbalimbali. Mapitio ya kazi tangulizi yanaonyesha kuwa hakuna mtafiti mwingine aliyefanyia utafiti kipengele hiki cha usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Utafiti huu umeangazia methali mbalimbali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua mbinu zinazotumika wakati wa kukusanya data ya utafiti. Muundo, eneo la utafiti na pia vifaa vinavyotumika katika utafiti vinabainishwa. Pamoja na hayo, sampuli na usampulishaji, changamoto katika utafiti na uchanganuzi wa data inayokusanywa ni vipengele vinavyoangaziwa.

### 3.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti unarejelea maelezo yanayojenga picha ya jinsi uchunguzi unavyofanyika kuanzia ukusanyaji hadi uchanganuzi wa data (Robson, 2007). Kimsingi, muundo wa utafiti unafananishwa na ramani au dira ya kuelekeza jinsi utafiti unaorejelewa unavyotekelezwa. Utafiti huu wa kitaamuli (kithamano) unatumia muundo wa kimaelezo (Mugenda & Mugenda, 2003). Mkabala huu wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data za utafiti kwa kutoa maelezo ya kina ya data zinazokusanywa kwa njia ambayo inaauni kujibu maswali ya malengo mahususi ya utafiti. Data za methali za Kiswahili zinazokusanywa zinachambuliwa kimaelezo wala si kwa mkabala wa kitakwimu. Mkabala wa kimaelezo unasaidia wasomaji wa matokeo kuyaelewa haraka na kwa urahisi (Kombo & Tromph, 2006).

Methali zinazohusika zinadondolewa kutoka kwa kamusi za methali zinazoteuliwa kwa minajiri ya utafiti huu, kisha kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo. Mtafiti anatumia mbinu iliyo ya maelezo kwa kuwa utafiti huu wenyewe asilimia kubwa unajengeka katika maelezo. Pia data kiwango kikubwa inayokusanywa maktabani inahakikiwa na baadaye inawasilishwa kwa njia ya maelezo. Mbinu hii ya maelezo ni bora na inawezesha kufikia

Mount Kenya University

malengo ya utafiti huu. Hili ni kutokana na ukweli kuwa maelezo yanayotolewa kuhusiana na data za utafiti yanatiwa nguvu imara na nadharia inayotumika ambayo ni nadharia ya Semiotiki.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Uchunguzi huu unajitika maktabani ambapo kazi zozote zinazohusiana kwa njia moja au nyingine na mada ya utafiti, zinasomwa na kuhakikiwa. Tasnifu, vitabu pamoja na makala mbalimbali kwenye intaneti yanasomwa ili kufanikisha maelezo muhimu kuhusu kipera cha methali katika fasihi simulizi. Tasnifu mbalimbali za watafiti wengine zinazohusiana na methali zinaangaliwa ili kutupa mwongozo na mwelekeo katika utafiti huu.

Kitaaluma, eneo la utafiti huu ni fasihi simulizi katika utanzu wa semi na kipera cha methali za Kiswahili. Vyanzo vya methali zinazochambuliwa ni kamusi 3 za methali za Kiswahili: *Maelezo ya Methali za Kiswahili* (Karama & Said, 1983), *Kamusi ya Methali* (Wamitila, 2001) na *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi* (Mkota, 2009). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TATAKI, 2019) inatumika kupata maelezo yanayohusiana na msamiati unaotumika katika methali teule. Kila methali inafafanuliwa kivyake ili ieleweke vyema na ujumbe usawiri wa magonjwa uuguzi na tiba uliopo ueleweke vyema.

Kamusi 3 za methali zinateuliwa kwa sababu zinaendana na lengo, madhumuni na nadharia ya utafiti huu. Kamusi teule za Kiswahili ni matini zenye upekee wa kuwasilisha fasili tendeti, mifano na matumizi ya methali zinazoorodheshwa humo. Uchambuzi wa fasili, mifano na miktadha ya matumizi ya kila methali ya Kiswahili katika matini hizi, unafanikisha uchambuzi chimbuko, maana na hata maudhui ya kila methali inayohusika. Haya ni

machapisho thabiti yanayojumuisha fasili, mifano na matumizi ya methali zinazoorodheshwa humo.

### 3.3 Idadi Lengwa

Walengwa katika utafiti kwa mijibu wa TATAKI (2019) ni jumla ya watu au vitu vinavyoweza kutumiwa kama sampuli ya utafiti. Kothari (2009) anasema kuwa idadi lengwa ya utafiti inaweza ikawa watu katika kijiji au vitu vyenye sifa sawa vinavyopatikana kwenye eneo mahsusi la kijiografia. Idadi lengwa ya utafiti huu ni jumla ya methali zote 5,856 zilizoorodheshwa katika kamusi zilizoteuliwa ili kuchunguzwa. Utafiti huu unahusu dhima ya methali za Kiswahili katika usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba yake. Kwa hivyo, jumla ya methali 5,856 zinachunguzwa kwa kina ili kudondoa tu methali ambazo zinasawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Methali ni kipera muhimu sana katika semi, ambao ni utanzu mkuu mojawepo katika tanzu za fasihi simulizi. Methali zina hazina kubwa katika maisha ya wanajamii kwani zinabeba dhima mbalimbali katika jamii inayohusika. Mojawepo ya dhima hizo ni kusawiri hali mbalimbali zinazowazunguka wanajamii yakiwemo magonjwa yanayowakumba, uuguzi na jitihada za kutafuta tiba mujarabu ya magonjwa haya. Mtafiti anachochewa na ukweli kuwa hata kama wachunguzi wa methali za Kiswahili wamefanya kazi kubwa ya kuorodhesha methali na kuziweka katika makundi mbalimbali kwa mujibu wa miktadha na majukumu yake, bado waliacha pengo katika kuangalia usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali hizi.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli huelezewa kuwa ni kundi la wateule wachache kutoka kundi kubwa au la jumla la watafitiwa wanaotokana na idadi lengwa (Yin, 1994). Kundi hilo ndogo linaloteuliwa ndilo linatumiwa kutoa data kama kiwalikishi cha idadi lengwa. Neuman (2014) anaifasili sampuli kuwa ni seti ya vitu ambavyo mtafiti anachagua kutoka kapu kuu na inayoweza kujumuisha sifa zake kwenye walengwa. Kinadharia, sampuli inafaa kuwa na sifa ya ulinganifu na uwakilishaji wa walengwa wanaohusika (Baker, 2010).

Usampulishaji ni ule mchakato unaofanikisha uteuzi wa kundi au sehemu ndogo kuchaguliwa kutoka kwa kundi kubwa (Kothari 2008). Kundi hili ndogo hutumika kuokota data kwa kuwakilisha kundi kubwa. Sampuli dhamirifu ni mbinu ambayo mtafiti huteua sampuli kimakusudi kwa matarajio na imani kuwa sampuli anayoteua inamsaidia katika kupata data za utafiti unaolenga kuufanya. Mugenda & Mugenda (1999) wanasema kuwa aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudia kupata habari za kina na bila kujumlisha.

Sampuli inayonuiwa kutumika katika utafiti huu ni methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, tiba na uuguzi. Hii ina maana kuwa utafiti huu unateua methali hizo kwa usampulishaji dhamirifu (lengwa). Kwa hivyo, methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinachunguzwa kimakusudi kwa kuwa zina uzito kamili katika suala la uteuzi. Yaani, methali zinazolengwa zinatufaa kwa kutoa habari muhimu na kwa kina kuhusu suala tunalolichunguza la usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Hii ina maana kuwa utafiti huu unakusudia kupata habari za kina kuhusu methali teule bila kuzijumlisha. Kwa marejeleo haya methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinachunguzwa kimakusudi kwa kuwa zina uzito kamili katika suala la uteuzi. Jumla ya methali 90 zinazosawiri magonjwa, uuguzi na tiba zinasampulishwa na kuchambuliwa na kuchanganuliwa kwa kina.

### 3.5 Njia za Kukusanya Data

Njia mbalimbali zinatumiwa kukusanyia data ya utafiti. Njia zenyewe ni pamoja na: Usomaji wa kina na makini wa kamusi teule, tasnifu mbalimbali za watafiti zinazohusiana na mada ya uchunguzi wetu, majarida, magazeti na uchanaganuzi wa matini mbalimbali zinazoweza faidi uchunguzi huu.

#### 3.5.1 Usomaji wa Kina

Usomaji wa Kina (*close reading*) ni njia ya uchanganuzi wa kifasihi inayolenga utondoti mahususi wa kifungu au matini ili kubaini maana ya ndani zaidi iliyomo (Smith, 2016). Maana itokanayo na usomaji makini ni fasiri ya msomaji wa kifungu au matini inayohusika. Usomaji wa machapisho anuwai maktabani unasaidia kupata maudhui ya methali teule na maelezo ya jumla kuhusu ugonjwa, uuguzi na tiba katika jamii ya Waswahili. Usomaji huo unafuatiwa na usomaji makini wa methali teule kabla ya uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

#### 3.5.2 Uchanganuzi wa Matini

Uchanganuzi matini unahusisha kamusi teule 3 za methali za Kiswahili. Njia hii inaazimiwa kubainisha methali mahususi zinazozungumzia ugonjwa, uuguzi na tiba. Pamoja na kuwa machapisho thabiti, Kamusi teule za Kiswahili ni matini zenye upekee wa kuwasilisha fasili tendeti, mifano na matumizi ya methali zinazoorodheshwa humo. Uchambuzi wa fasili, mifano na miktadha ya matumizi ya kila methali ya Kiswahili katika matini hizi, unafanikisha utambuzi chimbuko, maana na hata maudhui ya kila methali inayohusika.

### 3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data

Mount Kenya University

Nyezo zinazotumiwa kukusanyia data zinajumuisha kuorodhesha na kuainisha. Mbinu hizi zinasaidia katika kukusanya data kutoka kwa kamusi tatu teule. Upekuzi wa methali kutoka kwa kamusi unafanikishwa kwa usomaji wa Kina na uchanganuzi wa matini.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kipengele muhimu sana katika utafiti kwani huhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanapatikana na kutolewa ili utafiti uweze kukamilika. Mbinu ya maelezo inatumika katika hatua ya ukusanyaji wa data ya utafiti na pia katika kuchambua data inayokusanywa. Katika kukusanya data, malengo ya utafiti yanatiliwa maanani zaidi ili kujibu suala zima la utafiti huu.

Kothari (2004) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data, ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni au malengo ya utafiti wake. Mbinu hii hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi, kwa kuwa fasihi ni taaluma ya maneno, aidha ya kuandikwa au kuzungumzwa. Methali zinazopatikana vitabuni na kwenye Kamusi za Methali zinasaidia katika ufafanuzi wa utafiti huu.

Uchanganuzi wa methali hizi unafanywa kwa utaratibu na kutayarisha matokeo kulingana na malengo ya utafiti na nadharia inayoongoza utafiti huu. Orodha ya methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba na kuzichambua kila methali kivyake. Msamiati ambao unatumiwa katika methali hizi unaelezwa kwa kina na kutoa maelezo ya ziada na kuonyesha uhusiano uliopo wa msamiati unaotumiwa katika methali hizi. Kisha fani mbalimbali zinazotumika katika methali hizi zinachanganuliwa ili kutoa maelezo zaidi na kutoa maana ya ndani yanayobebwa na methali hizi. Mbinu ya maelezo inatumiwa kwa kuwa utafiti wenyewe

Mount Kenya University

unajikita na kujengwa na maelezo kwa kiwango kikubwa sana na pia data inayokusanywa maktabani inawasilishwa kwa njia ya maelezo.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Maadili ni miiko ambayo huzingatiwa jambo fulani linapofanyika. Katika utafiti maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote mtafiti anatangamana na wao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu.

Lengo la kuzingatia maadili ya utafiti ni kuona kwamba mkondo wa utafiti, shughuli nzima ya utafiti na hatua zote hazikubwi na madhara yoyote ama kuwe na udhalilishaji wa watafitiwa wote wanaoshirikishwa katika mchakato mzima wa utafiti. Kitetu (2003) anasisitiza kwamba masuala ya maadili hayawezi kuepukika katika utafiti wa masuala ya kijamii kwa sababu ni binadamu wanoshirikishwa.

Kwa hivyo, mchakato wa utafiti unapaswa kuzingatia miiko na maadili ili kufanikisha malengo yake. Kwanza, ridhaa ya kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya inaombwa na waraka rasmi wa utambulisho kutolewa. Mtafiti anaanza utafiti baada ya kupewa ruhusa na Chuo Kikuu cha Mount Kenya. Aidha na kupewa ridhaa ya mashirika yanayochapisha kamusi teule.

Pia hazina yoyote ya kazi binafsi ya wataalamu wengine ambayo inasaidia na kurejelewa au kunukuliwa katika kuandaa kazi hii ya utafiti inaorodheshwa katika nafasi ya marejeleo kwa kuzingatia, jina la mwandishi wa kazi ile (kitabu, jarida au tasnifu), anwani ya kazi yake, mwaka wa kuchapishwa kwa kazi ile iliyorejelewa, jina ya matbaa ya uchapishi na sehemu au ukurasa wa kuchapishwa.

Mount Kenya University

Waaidha, kibali cha kufanya utafiti kutoka kitengo cha kutoa vibali vya utafiti nchini, NACOSTI kiliombwa miezi miwili kabla ya kuanza utafiti huu ili kuendana na maadili ya kitaifa kuhusiana na utafiti katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti nchini.

### 3.9 Hitimisho

Ili kufikia malengo ya utafiti huu, vipengele mbalimbali vinavyohusiana na ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti vinaelezewa katika sura hii. Vipengele vyenyewe ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa ya utafiti, sampuli na usampulishaji, njia za kukusanyia data, vifaa vinavyotumika katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data inayokusanywa na hatimaye mazingatio ya maadili na miiko ya utafiti. Sura ya nne inachanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba yake katika methali za Kiswahili.

# SURA YA NNE

## UGONJWA, UUGUZI NA TIBA KATIKA METHALI ZA KISWAHILI

### 4.0 Utangulizi

Utafiti huu unachunguza usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba yake katika methali za Kiswahili. Ili kufanikisha madhumuni mahususi ya utafiti huu, sura hii ya nne inajadili uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya uchunguzi uliofanywa. Kimsingi, uwasilishaji, uchambuzi pamoja na mjadala kuhusu matokeo ya utafiti unatekelezwa kwa mujibu wa malengo pamoja mihimili ya nadharia ya utafiti. Sehemu ya kwanza inaangazia matumizi ya vipengele vya fani kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Sehemu ya pili inajishughulisha na matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kama nyenzo za kuwasilishia ujumbe katika methali teule za Kiswahili. Sehemu ya tatu inaangazia athari zitokanazo na usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili. Mwishowe, hitimisho linawasilishwa kama muhtasari wa yaliyomo katika sura hii.

### 4.1 Vipengele vya Fani Vibainishavyo Ugonjwa, Uuguzi na Tiba

Fani ni kiungo muhimu katika utunzi na hata uwasilishaji wa tungo za kifasihi. Hutumiwa ili kutia ladha katika lugha ya fasihi. Vipengele vya fani hutumiwa pia kuweka nguvu au msisitizo katika maneno yanayotumiwa kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa na msanii. Madumulla (2009) anaeleza vipengele vya fani kuwa ni fungu au kifungu cha maneno ambacho kinageuzwa maana ili kuleta maana tofauti na ile inayoletwa na maneno yanayotumika katika hali ya kawaida. Katika methali za Kiswahili zinazohusu ugonjwa,

uuguzi na tiba zinazochambuliwa, vipengele mbalimbali vya fani vinajitokeza. Vipengele vyenyewe vimewasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali 4.1 hapa chini:

**Jedwali 4.1: Vipengele vya Fani katika Methali Zihusuzo Ugonjwa, Uuguzi na Tiba**

| Na | Kipengele cha Fani | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1) | Taswira | 32 | 35.6% |
| 2) | Sitiari | 37 | 41.2% |
| 3) | Kinaya | 12 | 13.3% |
| 4) | Takriri | 5 | 5.5% |
| 5) | Tashihisi | 3 | 3.3% |
| 6) | Kweli Kinzani | 1 | 1.1 |
| | **Jumla** | **90** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kwa mujibu wa Jedwali 4.1 linalowasilisha data kuhusu vipengele vya fani katika methali zinazohusu ugonjwa, uuguzi na tiba, imebainika kuwa taswira inayo asilimia kubwa (35.6%) ya vipengele saba vya fani ambavyo vinajitokeza katika data ya methali teule zinazochambuliwa. Kipengele cha sitiari kinachukua nafasi ya pili kwa 41.2%. Kinafuatwa na kipengele na kinaya (13.3%), takriri (5.5%), tashihisi (3.3%), na kweli kinzani zinasheheni 1.1% kila kipengele mtawalia. Taswira inajitokeza kwa asilimia kubwa kwa kuwa methali nyingi zinazotumiwa na wanajamii huwa na neno moja au zaidi yanayojenga picha fulani akilini. Taswira inafuatwa na kipengele cha sitiari kwa karibu. Vipengele hivi vinaonekana kutumika kwa kiwango kikubwa katika methali tunazochunguza kwa sababu huwa zinarahisisha uelewa wa ujumbe unaosukwa katika methali zinazohusika.

Mount Kenya University

Wakiishadidia hali hii, Waititu na Oyugi (2005) wanafafanua kuwa taswira inapotumika katika kazi ya fasihi, huchora picha ya maudhui yanayowasilishwa akilini mwa hadhira lengwa. Kwa njia hii, taswira hufanikisha uelewa wa haraka wa ujumbe wa kazi ya fasihi inayorejelewa. Taswira husaidia kugadisha picha akilini na kunasisha ujumbe wa methali teule kwa wanajamii. Picha mbalimbali kama vile kuingiwa na mwiba, jino kuuma, mwambao wa kinyonga, kupasuliwa kwa jipu, silaha, mgonjwa kitandani na nyinginezo, huwa zinaibuka akilini mwa msikilizaji. Hali hii huisaidia hadhira lengwa kueleweka kwa ujumbe kwa wepesi. Nao Robinson (2003) pamoja na King'ei (2003) wanaeleza kuwa sitiari hutumika kukebehi, kuasa au kuelimisha kwa njia iliyofichika ili msemewa asikwazike.

Imethibitika kwamba vingepengele mbalimbali vya fani vinatumika kuwasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali teule za Kiswahili. Vipengele vyenyewe ambavyo ni takriri, taswira, isitiari, tashihisi, kinaya, kejeli na kweli kinzani zimejadiliwa katika vijisehemu vinavyofuata.

### 4.1.1 Takriri

Takriri ni mojawapo ya vipengele ambavyo hutumika katika uundaji wa methali za Kiswahili. Kipengele hiki hujitokeza pale ambapo neno ama maneno, silabi au hata sauti fulani hurudiwarudiwa. Sababu maalumu ya kurudiwarudiwa huku ni kujenga msisitizo wa jambo fulani. Kwa hivyo, kauli au jambo linalonenwa au kutamkwa huwa ni rahisi kunata kwenye akili za anayesikiliza (Wamitila, 2003).

Kwa hivyo, takriri ni marudiorudio ya herufi, sauti, silabi au neno au pengine wazo katika kazi ya kifasihi. Urudiaji huu huibua athari fulani kwenye fikra za masomaji ama msikilizaji na kwa hivyo kutilia maakini ujumbe unaosisitizwa (Msokile, 1993). Kwa mujibu wa Yego

(2013) takriri ni marudiorudio ya vipengele fulani vya kazi za kifasihi zaidi ya mara moja kwa kulinganisha na vipengele vingine vya kazi hiyo. Kwa kawaida, takriri hujitokeza kama neno, sentensi au aya ambayo inarudiwa zaidi ya mara moja kwa madhumuni ya kusisitiza jambo fulani la kimsingi ambalo mtunzi wa kazi ya kifasihi ananuia kuelezea. Takriri husaidia kwa kusisitiza au kutaka kitu fulani kifahamike na kuonekana kwa wepesi zaidi katika mawazo ya msikilizaji au msomaji.

Kati ya methali za Kiswahili 90 zinazochambuliwa, 5 au 5.5% zimethibitika kuwa zinatumia kipengele hiki cha takriri katika muundo wake. Data ya methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zitumiazo takriri anuwai zimeainishwa katika 1(a-e) hapa chini. Methali tano za Kiswahili katika kundi 1 (a-e) zinatumia ama takriri ya neno (a-e) au takriri ya silabi (d) kuwasilisha ujumbe wake kwa kurejelea ugonjwa (b, c, d), uuguzi (e) na tiba (a, b).

**1.** *(a) Dawa ya **moto** ni **moto***
*(b) Dawa si **chungu**, **chungu** ni maradhi*
*(c) **Ngoja ngoja** huumiza matumbo*
*(d) **Mzaha mzaha** hutimbuka usa**ha***
*(e) **Ganga ganga** za **mganga** humwacha mgonjwa na matumaini*

Katika 1(a) neno moto limerudiwa mara mbili. Neno moto katika kipande cha kwanza cha methali hii linaonyesha uchungu utokanao na ugonjwa wakati ule mtu anapougua. Sifa za moto zinaeleweka vizuri miongoni mwa wanajamii wote kuwa moto unapowaka huchoma na kuteketeza vyote vilivyo karibu na kuvimaliza hata ikiwa ni vyuma au mawe, humalizwa na kubaki majivu pekee. Ugonjwa unamithilishwa na moto; unapomwathiri mtu huambatana na uchungu ambao huwasha viungo vya mwili wa mgonjwa na kutokana na uchungu huo mhusika huwa hajiwezi na hulemewa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Isitoshe, mtu hujawa na uchungu wa hisia na mawazo. Uchungu uliojawa na majuto kutokana na athari

mbaya za ugonjwa. Moto unapowaka huhitaji kuzimwa ili usilete madhara zaidi na mbinu zote za kukabiliana nao hutumiwa. Katika kipande cha pili cha methali hii, neno moto linarejelea tiba au dawa. Ugonjwa unapomwathiri mtu humhitaji kukabiliana nao hadi mgonjwa apone. Njia bora ya kukabiliana na ugonjwa ni kumuuguza mgonjwa kwa kutumia dawa mjarabu. Dawa nyingi huwa chungu kutokana na virutubisho vikali ambavyo hutumiwa kutengeneza dawa zinazohusika. Ingawa dawa ni chungu, humhitaji mgonjwa avumilie kuzitumia ili apate kupona.

Dhana ya uchungu pia inajitokeza katika sehemu ya kwanza ya methali 1(b). Neno chungu katika muundo wa methali hii linaashiria tiba au dawa inayotuliza uchungu ambao husababishwa na ugonjwa. Dawa kwa kawaida huwa chungu. Uchungu wa dawa aghalabu husababishwa na kemikali chungu na kali ambazo hutumiwa huzitengeneza. Zamani, dawa za mitishamba zilikuwa zinatumika kutibu magonjwa mbalimbali. Waganga ndio waliokuwa na ufahamu wa aina mbalimbali za miti, matawi na mizizi iliyotumiwa kutibu na kuponya magonjwa tofautitofauti. Dawa hizo za mitishamba zilitengenezwa kwa kukata sehemu za miti kama vile matawi, kubambua magamba ya miti, maua, matunda au kuchimbua mizizi ya miti inayohusika. Baadaye, sehemu hizi za miti ziliwekwa majini na kuchemshwa kwa muda fulani. Matokeo aghalabu yalikuwa kinywaji kichungu kilichotumika kama dawa. Kwa kawaida dawa huwa chungu na humbidi mgonjwa avumilie ili aitumie na kupata nafuu. katika sehemu ya mwisho ya methali, neno chungu linatumiwa kuashiria taabu na shida za ugonjwa ambazo mgonjwa hupitia anapoathirika na huhitaji kutibiwa ili apone. Uchungu huu unaweza kuwa wa kihisia au wa kimwili. Mtu akiugua hupatwa na machungu ya hisia na majuto mengi na hubaki akijiuliza maswali mengi yasiyo na majibu kama vile, kwa nini yeye akaugua? Je, atapona? Atatoa wapi fedha za kugharamia matibabu? Maswali haya hujaza uchungu moyoni mwake. Mgonjwa huyu husalia kuomba msaada ili afanyiwe mambo

Mount Kenya University

ambayo angejifanyia kabla ya kuugua. Neno chungu linaporudiwa pia linaleta wizani fulani katika kuikariri methali hii, na pia uradidi huu unasaidia kukumbukika kwa methali hii kwa sababu muundo wake hautumii maneno mengi.

Neno ‘ngoja’ katika methali 1(c) ambayo inarejelea ugonjwa, limerudiwa ili kuweka msisitizo wa kule kuchelea kutafuta tiba au uuguzi mtu anapoumwa. Magonjwa mengi aghalabu hutoa dalili fulani kabla ya kumwathiri mgonjwa kwa kiwango kikubwa. Watu wengi huwa wanazipuuza hizi dalili zinazojitokeza mapema na kusubiri kwa matumaini kwamba maumivu yasababishwayo na ugonjwa yatatulia. Wengine nao hujiuguza kwa njia anuwai kama vile kunywa maji ya limau, kumeza dawa za kutuliza maumivu ilhali wengine huchukua muda na kupumzika kwa siku kadhaa kitandani bila ya fahamu kuwa kutulia kwa uchungu sio kupona kwa ugonjwa. Mtu anapochelewa kuutibu, ugonjwa unaweza kumwathiri kwa kiwango kikubwa na hatimaye ukawa ugonjwa sugu unaosemekana ‘kuumiza matumbo’, yaani sehemu zingine muhimu za mwili wa mgonjwa.

Methali 1(d) inatumia aina mbili za takriri – takriri ya neno ‘mzaha’ pamoja na takriri ya silabi -*ha*. Kama ilivyo kwa neno ‘ngoja’ katika methali 1(c), neno ‘mzaha’ linarudirudiwa kusawiri mapuuza na kutomakinikia dalili au hali ya awali ugonjwa na mgonjwa mwenyewe. Ugonjwa wenyewe unapokosa kushughulikiwa mapema, kwa visingizio vya utani na masihara, huishia kuwa sugu na usiodhibitika. Methali hii inairejelea hali hiyo kuwa ni ‘usaha’. Usaha ni uchafu wa majimaji au ute utokao sehemu ya mwili iliyo na ugonjwa wa kidonda au jeraha. Mtu anapougua ugonjwa wa kidonda kisha akakosa kutibiwa kwa haraka hatimaye usaha hutokea ambao hunuka na kuvutia nzi pamoja na wadudu wengine wanaopenda uchafu kama vile mabuu. Mgonjwa akiuguza kidonda upesi na mara baada ya

kupata jeraha, hakiwezi kutoa usaha. Hata hivyo, akichelea kukishughulikia huwa kinatoa usaha mwingi na huchukua muda mrefu kupona; au hata kikageuka kuwa donda ndugu.

Takriri ya silabi ***-ha*** na ***-nga*** inajitokeza katika methali 1*(d na e).* Silabi hizi zinarudiwa mara tatu katika kila methali, mtawalia. Utokezaji wa silabi hizi katika muundo wa methali zinazohusika unaweza kufasiriwa kuwa ni kina cha kati na cha mwisho katika vipande viwili vya methali hizi. Mbali na kurahisisha ukariri wa methali hii, uradidi wa silabi hizi unajenga kumbukumbu na kusisitiza madhara yanayoweza kutokana na kutotunza au kutibu kidonda kwa wakati ufaao. Isitoshe, takriri ya silabi hizi inajenga mvuto wa methali zinazohusika. Zinapotamkwa, silabi zinazorudiwarudiwa zinarahisisha uelewekaji wa ujumbe pasipo kulazimu matumizi ya maneno mengi ambayo yanaweza kumkanganya mlengwa wa methali.

Kwa kuusawiri uuguzi, methali 1(e) pia imetumia takriri kusisitiza umuhimu wa ‘ganga ganga’ za muuguzi au tabibu ambazo humfanya mgonjwa kupata nafuu anapofuata maagizo. ‘Ganga ganga’ katika methali hii inaashiria zile juhudi za mganga za kumshughulikia au kumuuguza mgonjwa. Hili linahimiza haja ya kutafuta uuguzi kwa watu walio na ujuzi huo kwani wanao ueledi wa kuuguza na kutibu na hatimaye kumwezesha anayeugua kupata nafuu. Kwa kutumia msimbo wa kiishara, mojawepo ya misingi iliyojenga nadharia ya Simiotiki, unaohusishwa na namna wasikilizaji wanavyoelewa maana ya kiishara katika kazi za fasihi, imebainika jinsi takriri katika methali teule inavyotumika ili kujenga ishara zinazotilia mkazo au msisitizo wa ujumbe uliosheheniwa na methali hizo. Takriri hii imejengwa kwa kutumia lugha ya kiishara kutokana na msimbo wa kiishara wa nadharia ya Simiotiki kurejelea umuhimu na juhudi za mganga katika uuguzi na tiba za magonjwa. Akichunguza takriri katika methali za Wahaya, Farida (2018) anafafanua kwamba takriri hutumiwa ili kuleta msisitizo ama mkazo wa jambo na pia hurahisisha kuweka jambo akilini

mwa msikilizaji au msomi. Hii ni kwa kuwa mtu anaporudia jambo huwa lina baki akilini kwa urahisi ukilinganisha na kuliskia jambo fulani mara moja pekee. Pia anashughulikia aina za takriri ambazo zinahusika katika methali teule.

Kwa ujumla, msisistizo unaothibitishwa na vipashio vinavyorudiwarudiwa unashiria umuhimu wa kutekeleza maana au ujumbe unaokaziwa kwenye methali hizi. Takriri kwa maoni yetu inasaidia uelewa wa ujumbe wa methali teule bila kutumia maneno mengi ambayo pengine mwanajamii hangeweza kuyakumbuka anapotumia methali hizi. Pamoja na kukoleza ujumi na sanaa ya methali, takriri pia humtia mtu hamu ya kuisema methali fulani kutokana na ule mchezo wa vina au silabi na maneno yanayojirudia. Vinginevyo, matumizi ya takriri pia yanaweza kutokana na upungufu wa maneno kwa aliyetunga methali hizi na kwa hivyo akalazimika kutafuta maneno yenye silabi zinazoendana ili kuunda maneno yanayokidhi mahitaji yake. Kimsingi, tamathali hii ya usemi inawezatumiwa na mtunzi wa methali kuashiria umahiri wake katika fani hii.

### 4.1.2 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi inayotumika kuvipa vitu sifa zote au baadhi ya sifa za binadamu kama vile hisi mbalimbali, kutembea, kuongea na pia vitu hupewa muonekano wa kibinadamu. Kwa mujibu wa Msokile (1993) tashihisi huelezwa kwa kurejelea mazingira matatu: kwanza, ni sitiari ambayo huashiria kitu kisicho mtu kupewa tabia za binadamu. Pili, ni sitiari ambayo sehemu ya maumbile ya binadamu hukipa kitu fulani sifa hizo za kibinadamu. Mwisho, ni sitiari ambayo huwakilisha kitu kisicho na uhai na kukipa sifa za kibinadamu. Nao Njogu na Chimerah (1999) wanaifasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo hukipa kitu kisichokuwa na uhai mkamilifu sifa za kitu chenye uhai kinachojitegemea katika mazingira yake. Akitoa kijalizo, Senkoro (2011) anadadavua kuwa

tamathali hii pia hupewa fasili ya binadamu. Hili ni kutokana na sababu kuwa vitu visivyo na sifa za kibinadamu hupewa sifa hizo.

Tamathali hii huvitia nguvu vitu ambavyo kwa kawaida huwa vitulivu na kuvifanya vionekane katika mwendo wa taharuki na picha. Hali hii husaidia msikilizaji kupata mvuto ulioimarishwa na usanii na maana au ujumbe wa mwasilishaji wa methali au anayetumia methali katika maongezi kwa uwazi zaidi. Kipengele hiki cha fani huvipa vitu visivyo uhai sifa za kibinadamu ambapo vitu hivyo huyatekeleza matendo ya kibinadamu. Vitu ambavyo havina uwezo wa kutekeleza jambo lolote hupewa uwezo wa kutenda mambo kama afanyavyo binadamu katika hali yake ya kawaida. Katika data ya methali 90 zilichanganuliwa, methali 3 au 3.3% zinazoshadidia hali hii zimeainishwa katika 2(a-c) hapa chini:

**2.** *(a) Ngoja ngoja huumiza matumbo*
*(b) Sitafuga ndwele na waganga tele*
*(c) Dawa inayowasha inakupenda*

Methali 2(a) inahuisha kitendo cha ‘kungoja’ ili kuwasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa kuonyesha umuhimu wa kutafuta matibabu kwa haraka mtu anapougua. Kungoja ni ile hali ya kuchukua muda kabla ya kutekeleza jambo. Neno ‘ngoja’ limepewa sifa za kibinadamu za kuumiza. Kuumiza hapa kunarejelea kuhasiri au kuharibu ile hali nzuri ya afya. Ingawa kitenzi ‘ngoja’ hakina uwezo wa kuumiza kama ambavyo binadamu awezavyo kuumiza, kinatumiwa kwa njia hii kuutilia mkazo ujumbe na matokeo ya kungojea mtu anapougua. Mara nyingi mtu anapopata dalili za ugonjwa fulani huchukuwa muda kabla ya kwenda kutafuta matibabu kwa muuguzi au kituo cha afya. Dalili hizi huongezeka na hatimaye mgonjwa hujipata katika hali mbaya zaidi baada ya muda fulani. Mtu anapochukua muda kabla ya kwenda kutafuta tiba, ugonjwa huendelea kuathiri viungo mbalimbali vya mwili, na

jambo hili linaweza kupelekea kuathirika hata kwa viungo ambavyo havingeathirika iwapo angetafuta matibabu mapema pindi alipogundua ana dalili za ugonjwa. Hata hivyo, mtu anapochukua hatua za haraka na kwenda kutafuta uuguzi, hujisaidia hivi kwamba ugonjwa hauwezi kupata muda wa kujikoleza mwilini na hata kupelekea sehemu mbalimbali za mwili kuathirika zaidi.

Methali ya 2(b) imebebeshwa ujumbe unaorejelea uuguzi kwa kutumia tamathali ya usemi ya tashihisi. Ndwele, ambacho ni kisawe cha ugonjwa, inapewa sifa za kibinadamu, mfugo au kiumbe mwenye uhai. Yaani, ndwele ni kiumbe aliye na sifa ya kufugwa. Kufuga ni kule kuweka wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, ndege ili kupata manufaa fulani baada ya kuwatunza. Manufaa haya huwa ni kupata maziwa, samadi, mayai au nyama. Baadhi ya mifugo pia huwa kivutio nyumbani, au kipimo cha utajiri wa mtu katika jamii. Hili lina maana kuwa ufugaji wa ndege na wanyama humfaidi mfugaji anayehusika. Ndwele inahuishwa na kupewa sifa hizi za wanyama na ndege wanaofugwa na kwa njia hiyo kuchora picha kwamba kuna faida ya kukaa na ugonjwa pasipo kutafuta uuguzi au matibabu. Kwa mujibu wa methali hii kufuga ni kule 'kutunza' au kukaa na ugonjwa, pengine nyumbani, bila kutafuta matibabu. Hali hii inayozua swali, je, kuna faida gani kukaa na ugonjwa mwilini bila kutafuta matibabu? Methali hii inasisitiza umuhimu wa mtu kwenda kutafuta matibabu. Kazi ya waganga huwa ni kutibu wanaougua magonjwa mbalimbali. La mno ni kuwa waganga, hata kama ni wengi au tele, huwa hawawatafuti wanaougua bali ni wagonjwa ndio hutafuta waganga na kujua waliko ili wauguzwe. Hivyo basi unayeugua anafaa kumtafuta mganga ili aweze kuuguzwa ugonjwa alionao badala ya kukaa nao, asipojukumika kutafua mmoja wa wale waganga wengi anabaki katika hali yake ya kuugua.

Katika methali ya 2(c) dawa, ingawa chungu au yenye kuchoma mwilini, inahuishwa na kupewa hisia za kimapenzi. Inawasilisha ujumbe unaosawiri tiba kwa matumizi ya tamathali ya tashihisi. Uhuishi huu wa dawa unaashiria uhusiano wa karibu unaokuwepo baina ya mgonjwa na dawa. Watu wanapokuwa katika mapenzi, mara nyingi huwa pamoja kwa sababu mapenzi huwapa mshikamano, hususan wa kimawazo. Wakati mwingine wapendanao hukosana lakini kwa sababu ya kuthamini penzi lao hubidi kutafuta njia za kusuluhisha matatizo yao. Sio kila wakati wapendanao hufikiria kwa njia moja, maono yao yaweza kuwa tofauti na pia vitendo vingine huleta ugomvi kati yao. Hatimaye, hupatana na kurudiana kwani hata kama kukosana kupo, kuna faida katika mahaba yao wapendanao. Uhusiano huu wawapendanao unajitokeza katika methali hii kwa kuipa dawa zile hisia za kimapenzi. Hata kama dawa ni chungu mgonjwa huihitaji ili apone. Ili mgonjwa apone huhitaji uhusiano wa karibu na dawa. Muuguzi huwa anamwelekeza kuzitumia dawa kiasi fulani baada ya masaa fulani bila kukosa. Hata kama dawa ni chungu na huwasha mtu anapozitumia, hubidi kuzitumia hadi apone.

Tashihisi inatumika kusaidia wanajamii kuelewa zaidi ujumbe unaobebwa na methali ambazo zinatumia kipengele hiki katika muundo wake. Kipengele hiki cha fani pia husaidia kwa kumpa msikilizaji wa methali teule mvuto wa kusikiliza yanayosemwa. Kwa kuzingatia msimbo wa kiurejelezi katika nadharia ya simiotiki, msamiati ambao unatumika katika utamaduni wa jamii ya Waswahili ndio unatumika kuunda methali teule. Hili linasaidia kuelewaka kwa methali hizi kwa urahisi.

Timmany (2020) anahuisha Ukimwi na kiumbe aanyeitwa zimwi katika uchunguzi wake wa tamathali za usemi na taswira katika utenzi wa Ukimwi ni Zimwi. Msikilizaji wa methali hizi anaposikia jina zimwi anakumbuka za fasihi simulizi namna zimwi katika hadithi husika

Mount Kenya University

linachorwa kuwa ni kiumbe anayedhuru watu. Mtunzi anahuisha Ukimwi kwa kusema ugonjwa wa Ukimwi hutafuna mtu unapompata. Pia Ukimwi unahuishwa unapopewa sifa za kibinadamu mtunzi anaposema ugonjwa huu huingia mwilini mwa mtu bila hodi na ya kwamba ugonjwa huu unapenda kuishi katika kumbi za burudani.

### 4.1.3 Taswira

Taswira ni picha zinazojengeka akilini mwa msomaji au msikilizaji anapoisoma kazi yoyote ya fasihi kutokana na maelezeo ya msimuliaji au mwandishi wa kazi inayorejelewa. Picha hizi hurahisisha uelewaji wa kazi inayohusika miongoni mwa hadhira lengwa (Ntaragwi, 2004). Nao Oyugi na Waititu (2005) wanaelezea taswira kuwa ni kipengele ambacho kwacho msanii hutumia msamiati utoao picha halisi ya yale anayotarajia kueleza hivi kwamba msikilizaji huelewa picha inayokusudiwa akilini mwake.

Katika uchunguzi wake wa dhamira zinazojengwa na taswira katika methali za Wapemba, Khatib (2014) anatalii methali zinazosheheni taswira. Anabainisha aina mbalimbali za taswira zinazotumika katika methali hizi kwa mfano, taswira za kisaikolojia, kiastronomia, kibotania, kizuolojia na vilevile za kiteolojia. Utafiti huu unachunguza taswira ya vitu vya kawaida kwa mfano kiatu, kitanda, mwiba, jina, moto na dawa ili kutoa taswira zilizo katika methali teule na ujumbe uliosukwa ndani ya taswira hizi. Katika uchunguzi wake wa ufumbaji katika riwaya ya Kiswahili, Ayiera (2017) anajadili taswira mbalimbali zinazojitokeza katika kazi za Katama Mkangi. Anagundua kuwa, kupitia ujenzi wa taswira, wahusika mbalimbali wanahusika kama vile wahusika wateule, wachochole, matope na wanamapinduzi. Taswira hizi zinasaidia kujenga ufahamu bora wa kuchanganua taswira katika methali teule.

Akichunguza tamathali za usemi na taswira katika *Utenzi wa Ukimwi ni Zimwi* ulioandikwa na Mohmoud Abdulkadir, Timammy (2020) anaeleza kuwa tamathali za usemi na taswira zinatumika kufumba ujumbe wa kazi ya mtunzi. Taswira ya Ukimwi kulinganishwa na zimwi ni picha tosha ya kuashiria vile ugonjwa huu ulivyo janga kubwa la kuogofya na vile unaweza kumeza au kuangamiza watu katika jamii. Utafiti huu unatupa mwanga wa kufahamu jinsi ya kuangazia kipengele hiki cha taswira katika utafiti huu.

Ogutu (2021) anaeleza taswira kuwa ni picha inayomjia mtu akilini mwake anaposoma, kutazama au kusikiliza kazi yoyote ya kifasihi. Anaendeleza maelezo yake kwa kusema kuwa taswira hufumbata maana fiche zilizo na jazanda.

Ibrahimu na wenzake (2021) wanachunguza taswira kama mojawapo ya vipengele vya fani katika fasihi ya watoto. Wanaangazia mwingiliano uliopo baina ya taswira na picha. Inathibitika kwamba taswira inapofungamana na picha, watoto huelewa ujumbe uliopo katika riwaya za watoto upesi na kwa wepesi.

Akichunguza taswira ya jamii ya kisasa kwa mujibu wa riwaya teule za kisasa zilitungwa na Wamitila, Mutua (2022) anabaini kuwa picha za ukosefu wa utaratibu wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika jamii ya kisasa unajitokeza mno. Ingawa uchunguzi huu hauhusiani na utafiti wetu, unatusaidia uelewa wa kipengele cha taswira na jinsi ya kukishughulikia katika utafiti huu.

Katika utafiti unaochanganua vigezo vitumikavyo kujenga wahusika katika ushairi wa Kiswahili, Sikuomba na Bulaya (2023) wanagundua kuwa wahusika katika diwani ya ushairi iliyotungwa na Seif Khatib wamebainishwa kwa mujibu wa vigezo vya kisiasa, kiishara, kitaswira, kidini pamoja na kifasihi simulizi. Kazi hii inaonyesha njia mbalimbali za

kuwajenga wahusika katika ushairi ambazo kipengele cha taswira husaidia kujenga. Hata kama utafiti huu haukufaidi utafiti wetu kwa kina unatoa mwanga wa kuelewa taswira ni nini.

Wamitila (2003) anaainisha aina mbili kuu za taswira. Kwanza, analezea taswira za kimaelezo na pili, zile zinazotokana na ishara. Taswira za kimaelezo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au anayesimulia na huwa hazina maana fiche au ya ziada. Nazo taswira za kiishara huunda picha iliyo na ujumbe uliofichika na kwa hivyo ishara hizi huhitaji kufumbuliwa ili kupata maana inayokusudiwa na mtumizi wa methali. Methali teule zinazochunguzwa zinatumia taswira za kiishara kupasha ujumbe wake kwa wanajamii. Picha hizi hujengwa katika mafumbo ambayo hutumika kuufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Nadharia ya simiotiki inawiana na mada ya utafiti huu wetu kwa kuwa methali nyigi zinatumia lugha yenye taswira, mafumbo, ishara na picha ili kuwasilisha ujumbe wa methali teule. Hii ina toa maana kuwa kinachosemwa katika methali fulani kuna uwezekano kuwa sio kile kinachojitokeza bayana katika msamiati unaotumika lakini chaweza kuwa kitukingine mbali sana na kinachirejelewa.

Methali teule za Kiswahili katika 3 (a-ii) zinaashiria matumizi ya taswira kuwasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa, uuguzi na tiba.

**3.**

a. *Baada ya donda msumari moto.*
b. *Chendacho kwa mganga hakirudi.*
c. *Dawa ya jipu kulipasua.*
d. *Hapana jeraha bila silaha.*
e. *Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda.*
f. *Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda.*
g. *Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu*
h. *Dawa ya moto ni moto.*
i. *Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*
j. *Jino liumalo hung'olewa.*

Mount Kenya University

k. *Jino la pembe si dawa ya pengo.*
l. *Kufanyika gaga sio kupona kwa donda.*
m. *Kidole kimoja kikiumia chenzake chapwita*
n. *Kutaataa sio dawa ya kufa.*
o. *Kuzunguka mbuyu si dawa ya shetani.*
p. *Mapenzi kikohozi hayawezi fichika.*
q. *Donda ndugu laisha dawa*
r. *Maradhi huja shoti, yakitoka ni mtambao wa kinyonga.*
s. *Mwenda mbio hujikwaa dole.*
t. *Mwenda pole hajikwai.*
u. *Mwenye kuficha kidonda, kilio kitamfichua.*
v. *Ng'ombe mteua jani ni mgonjwa.*
w. *Nzi kufa juu ya kidonda si haramu.*
x. *Si hasara nzi kufa juu ya kidonda.*
y. *Ukiwaa uwe na subira.*
z. *Uzee hauna dawa.*
aa. *Kwa mdogo pumu kwa mkubwa mafua*
bb. *Mwana kidonda, mjukuu kovu*
cc. *Ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini akasaidiwe*
dd. *Pembe si dawa ya kuku.*
ee. *Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo.*
ff. *Mficha ndwele hapati dawa.*
gg. *Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha.*
hh. *Wanja wa Manga si dawa ya chongo.*
ii. *Kidole kimoja hakivunji chawa*

Methali zinazotumia taswira kuashiria ugonjwa ni 3(d, e, f, g, h, i, m, o, p, r, s, t, u, v, w). Katika 3(d), jipu, ugonjwa ambao husababishwa na bakteri na hufanya sehemu inayoathirika kufura na wakati mwingine hutoa usaha na huwasha sana. Ili kupata nafuu kutokana na ugonjwa huu, mgonjwa huhitaji kulipasua lile jipu. Jipu hupasuliwa kwa sindano ama kifaa chembamba kilicho na makali. Jipu linapopasuliwa huanza kupona na uchungu na ule usaha huisha. Methali hii inachora jipu ambalo limefura na linalomsumbua mgonjwa. Ili kuliponya lile jipu mgonjwa sio lazima aende kuuguzwa na tabibu ila anaweza kulipasua na kupona. Jipu linaashiria magonjwa madogo madogo ambayo hayafai kumsumbua mtu anapougua na anaweza kujitibu yeye mwenyewe ama akajitafutia huduma ya kwanza hata kabla ya kwenda kwa mganga ili kutafuta tiba. Dawa inatumika kuchora suluhisho la ugonjwa wa jipu ambalo ni kulipasua.

Mount Kenya University

Methali 3(e) inatoa picha ya jeraha kama ugonjwa unaotokana na silaha. Neno silaha linatumika kutoa picha ya kitu kinachomuumiza mtu na kupata jeraha mwilini mwake ambao ndio ugonjwa unaorejelewa hapa. Silaha inatumika kuchora picha ya chanzo cha ugonjwa kwa mtu anapougua. Taswira inayojitokeza katika methali hii ni kuwa kila ugonjwa anaougua mtu huwa na chanzo chake. Ni vigumu sana mtu augue bila kuwa na kisababishi cha ugonjwa wenyewe. Chanzo cha uwele chaweza kuwa viini vinavyosababisha magonjwa kama bakteria na virusi, msongo wa mawazo, silaha kama vile panga, mishale ama hata vifaa vinavyotumiwa na wanadamu katika shughuli mbalimbali za kila siku. Silaha inatumika hapa kuchora picha ya kinachosababisha ugonjwa. Silaha inapotumiwa pengine wakati wa vita ama ikamchoma mtu kwa bahati mbaya huleta ugonjwa wa jeraha ambao huhitaji kuuguzwa.

Katika 3(f) kwapa ni sehemu ya mwili ambayo iko chini ya bega na huwa inatoa harufu mbaya ambayo huitwa kikwapa. Kikwapa kinachora picha ya fedheha ambayo magonjwa mengine humletea mgonjwa. Mtu anayeweza kutoa harufu ya kikwapa huenda akawa na haya au soni anapopita mbele ya watu ama anapokaa mahali palipo na halaiki ya watu. Watu watashangaa mahala ambapo harufu mbaya inapotoka. Wanapogundua inatoka mwilini mwa mtu fulani, atahusishwa na uchafu na asiyependa usafi. Huenda hali hii ya kunuka ikafanya atengwe na watu na kusemwasemwa vikaoni jambo ambalo litamharibia sifa na kumgumbika soni. Methali hii inatoa picha ya kikwapa ambacho kinatoka mahali pasipo na kidonda. Hii inachora uhusiano uliopo baina ya ugonjwa wa kidonda na harufu mbaya ya kikwapa. Ugonjwa unapompata mtu hufuata na madhila mengine ambayo pengine mgonjwa hapo mbeleni hakuwa ameyaona. Kutokana na ugonjwa mtu anaweza tengwa hata na watu wa karibu, familia au hata mpenziye, anaweza kukosa kazi ama akafutwa kazi, kukosa amani na kuandamwa na uchungu moyoni ama hata ugonjwa ukapelekea kufa. Haya yote yanachora harufu mbaya ya kikwapa itokayo kidondani.

Methali hii 3(g) inatoa picha ya uhusiano wa karibu kati ya mgonjwa na kitanda unaoletwa na ugonjwa. Mtu anapougua mara nyingi ugonjwa huathiri afya yake njema na kumwacha akiwa hoi na anayetegemea msaada wa watu wengine katika shughuli zake nyingi kama sio zote za kila siku. Mgonjwa hulazwa kitandani kwa kipindi fulani ili auguzwe hadi atakapopona. Kitanda husalia mahali ambako mgonjwa hujipata na hubaki pale kwa muda mrefu anapougua angalau kupata liwazo kwa muda na auguzwe. Kwa kawaida mtu akiwa mzima wa afya hulala kitandani tu wakati anahisi usingizi hususan usiku. Lakini mtu anapougua hubaki pale kitandani kwa muda mwingi, iwe mchana au usiku, awe na usingizi ama asipokuwa nao usingizi. Picha ya mgonjwa na kitanda inachora taswira anayoonyesha ukaribu kati ya mgonjwa na kitanda unaoletwa na ugonjwa.

Picha ya kulinganisha kunjikwaa baina ya sehemu mbili za mwili ambazo ni kidole na ulimi inatumiwa katika 3(i). Ulimi ni sehemu ndogo ya mwili ambayo huwa kinywani mwa mtu na hutumika katika maongezi, kutafuna chakula na kumeza. Kazi kuu ya ulimi ni kusaidia kutamka maneno kwa ufasaha. Mtu anapoongea anaweza kusema mengi mazuri au mambaya. Mdomo huwa na wepesi sana wa kuyasema maneno yoyote na kwa hivyo ulimi unafaa kulindwa kwa kutosema sana ama kuwa mwangalifu sana kwa mtu anapoongea mahali palipo na watu. Maneno mazuri yanaposemwa hufurahisha na yanaweza kutumika kutuliza moyo wa anayeumia na kumpa tumaini. Mtu anaposema maneno mambaya na ya kukwaza kwa bahati mbaya ama kwa kudhamiria kama vile kutusi mtu au kusema maneno ambayo hayaendani na maadili ya jamii huwa anajipata katika hali ya mshikemshike na yanaweza kumharibia maisha yake, uhusiano wake na watu, kufanya apoteze kazi ama akafungwa jela miaka mingi. Mtu kama huyu anaweza kuishi kujilaumu ama kulaumiwa na watu wengine kwa kile kitendo chake cha kuyasema maneno maovu. Maneno haya yanaposemwa yanaweza kuwakwaza wengine na lile jeraha likabaki nyoyoni mwao daima.

Mtu anapojikwaa kidole huwa ni rahisi kuuguza kidole na kwa muda mfupi kidole hupona jeraha lake na likasahaulika. Taswira ya ni afadhali kunjikwaa kidole inajichora akilini mwa mtu kuliko ulimi. Jeraha la kidole laweza kuwa shufaa kuliko ulimi ambako jeraha ambalo ni jeraha linaloletwa na meno yanapouma ulimi au maneno maovu yatokayo kinywani ni chungu na laweza kuzuia mtu kula au hata kuongea kwa urahisi na kwa ufasaha au kusababisha jeraha la moyo kwa mtu mwingine.

Wakati mwingine kutokana na maambukizi ya bakteria meno huuma na hubidi mtu atafute uuguzi. Picha inayochorwa na methali hii 3(j) ni ya sehemu ndogo ya mwili na ambayo ni muhimu sana kwani hutumika kusaga chakula ili mwili upate lishe la kujenga mwili. Jino au meno hutumika kumpa mtu sura nzuri usoni haswa wakati wa kutabasamu meno pia huwa kama pambo. Jino linapouma huhitaji kuuguzwa na mara nyingi tiba yake huwa ni kung'olewa. Ili mwili mzima upone sehemu hii inapougua huhitaji kutenganishwa na mwili ili mwili mzima upate kuuguzwa. Jino linaleta taswira pia ya sehemu ndogo ya mwili lakini inapougua mwili mzima unathirika kwani kutafuna chakula huwa vigumu na kwa hivyo huhitaji tiba ili mwili mzima upone. Taswira inayotokea hapa pia ni kwamba viungo vya mwili hutegemeana kwa kila hali hivi kwamba sehemu moja ya mwili ikiumia huathiri sehemu nyingine kwa njia ya moja kwa moja. Jino linapoumia linaathiri mwili mzima kwani mtu hawezi kula, jambo ambalo linaathiri mwili mzima.

Jamii ya Waswahili ilikuwa na imani za kijadi ambako waliamini mtu akiugua baadhi ya magonjwa yanaweza kuuguzwa kwa kuzunguka mti wa mbuyu mara kadhaa na muda fulani. Kuna wale waliofuata ile itikadi ya kuzunguka mbuyu na wakapona ila wengine hawakupona. Methali hii 3(n) inachora picha ya mtu aliye na ugonjwa na inayetafuta tiba. Shetani ni neno linalotumika kuchora shida au ugonjwa usio wa kawaida na kwa hivyo

anahitaji kuuguzwa kwa njia isiyo ya kawaida. Aliye na shida anachorwa akitafuta suluhisho kwa kuzunguka mti unaoitwa mbuyu.

Mapenzi yanapewa taswira ya ugonjwa wa kikohozi katika 3(o). Mtu anapouugua ugonjwa huu hutoa sauti kubwa kwa mdomo inayosikika na yeyote aliye karibu.Vivyo hivyo mapenzi hayawezi fichika wawili wanapopendana. Kila aliye karibu atawajua kwa uwazi wapendanao hata wakijaribu kuficha penzi lao. Vilevile kama vile kikohozi huwa ni rahisi sana kuambukizanwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, vivyo hivyo ndivyo mapenzi huambukizanwa kati ya mtu na mwingine.

Pia methali 3(s) inatumia maneno 'kuficha na kufichuka' kwa kurejelea aliye na ugonjwa. Kuna magonjwa ambayo huwa ni haramu kuyataja wala kuseme yana mwathiri mtu. Magonjwa ya zinaa kama vile Ukimwi, kaswede na kisonono huwa yanaandamwa na aibu yanapomwathiri mtu na ikijulikana na wanajamii, kwa hivyo mtu akiathirika na magonjwa haya huwa anafanya juhudi juu chini asijulikane na wanajamii. Magonjwa haya huwa na uchungu na mengine huathiri hata mwendo wa anayeathiriwa. Yanapokaa kama hayajatibiwa huathiri mwili na dalili zake huonekana peupe. Neno kilio linatumika kuchora taswira ya uchungu na maumivu ambayo huambatana na ugonjwa. Hata kama mtu atauficha ugonjwa alionao ni kwa muda tu kwani maumivu yatamfanya kwenda kutafuta uuguzi au tiba. Methali hii inatoa picha ya kuweka mambo wazi kwani kuyaficha ni kwa muda mfupi tu kabla ya julikane na watu wote.

Methali 3(p)imetumia neno shoti kuchora picha ya jinsi ugonjwa huingia mwilini mwa mtu kwa mwendo wa kasi mno. Mtu anaweza kuwa mwenye siha njema asubuhi na jioni awe hali mahututi ama hata akaaga dunia. Hii inachora taswira ya jinsi miili yetu huwa dhaifu hata kama kwa juu inaonekana yenye afya. Vilevile mnyama anayeitwa kinyonga ambaye

mwendo wake ni wa polepole ametumika ili kutoa picha ya jinsi ugonjwa huchukua muda mrefu kupona mtu anapougua. Picha ya kuwa na subira mtu anapougua inajitokeza kwa wazi.

Katika 3(q na r), methali hizi zinachora hali mbili ambazo ni kinzani, kwenda mbio na kwenda polepole ambapo matokeo yake bado yanakinzana. 3(q) inachora taswira ya anayekwenda mbio au haraka bila uangalifu wowote ambako huishia kwa kujeruhi kidole. Kwa kawaida anayetembea hobelahobela asilimia kubwa huwa kuna uwezekano wake kukunguwaa na kuumiza vidole vyake. Methali 3 (r) inatoa picha ya anayeenda kwa uangalifu na nafasi yake ya kujikwaa huwa finyu sana na hata akikunguwa hawezi jiumiza. Taswira ya utaratibu na kuwa mwangalifu mtu anapotembea inajitokeza katika methali hizi ili kutojiumiza ama akapata jeraha. Nayo methali 3(t) inatoa picha ya athari mbaya inayoletwa na ugonjwa. Kwa kawaida ng’ombe akiwa na afya huwa yu ala aina nyingi za majani lakini akianza kuteua majani mwili wake hudhoofika na hii huwa ishara inayoashiria kuwa afya yake si nzuri tena. Neno kuteua limetumika kuonyesha jinsi mtu akiwa mgonjwa huchagua kile alacho pasipo hiari yake. Jambo hili linachora picha ya msaada wa dharura ambao mtu huhitaji anapoanza kuonyesha dalili za kuugua kama vile ng’ombe hujikokota hadi zizini akiugua na kungoja msaada wa anyemfuga. Mtu anapougua huwa anatoa dalili za ugonjwa na huhitaji kusaidiwa ili apate nafuu.

Katika methali 3(u na v) zinachora taswira ya uhusiano wa ukaribu ulio na manufaa kati ya kidonda na nzi. Ingawa kidonda kwa anayeugua huwa ni ugonjwa unaomuumiza na huhitaji kuuguzwa, kwa nzi huwa na manufaa na huwa ndio tegemeo la nzi kama chakula chake ili aweze kuishi. Kutokana na usaha utokao kwenye kidonda, nzi hupata mlo na wakati mwingine mbawa zake hunatwa na huo usaha na hatimaye hufia palepale juu ya kidonda. Kwa hivyo nzi akifa juu ya kidonda huwa yu afa akitafuta mlo.

Picha ya kuwa na subira mtu anapougua inajitokeza waziwazi katika methali 3(w). Mtu anapougua, ugonjwa unaweza kumwathiri kwa haraka, lakini safari ya kuuguza au kutibu ugonjwa wenyewe huwa refu na yenye uchungu na yenye hisia zilizojaa uchungu mwingi. Mgonjwa huhitaji kumtembelea muuguzi mara kwa mara na kumeza dawa chungu ama hata wakati mwingine kufanyiwa upasuaji ili apone.

Taswira ya hali ya kuzeeka ambako ni kuwa na umri mkubwa unaotokana na kuishi kwa muda mrefu inajichora akilini mwa mtu. Mtu aliye na mvi kote kichwa na kunyanzi kwenye uso, aliye ma mkongojo na aliyejipinda ni picha inayojitokeza akili mwa mtu. Kwa uhakika mtu akiwa mzee hutegemea usaidizi wa walio karibu na yeye ili kufanya mambo mengi katika maisha yake. Jambo hili huwa halipendezi mtu hivi kwamba lazima ungojee msaada wa mtu mwingine kutenda jambo lile ulilokuwa unaweza kulitekeleza ujanani. Hali hii ya uzee huwa haipendezi mtu yeyote na kama kungekuwa na uwezekano, kila mtu angependa kuisha maisha ya ujanani ambayo huwa na mbwembwe na raha nyingi. Mwili wa ujanani huwa unapendeza kwa sura na pia huwa na nguvu za kufanya mambo mengi bila kutegemea usaidizi wa mtu yeyote. Neno dawa limetumika kuashiria kuwa hakuna suluhisho la uzee, mtu anapozeeka hawezi kurudi ujanani kamwe taz. 3(x).

Methali teule 3(a, g, i, k, na v) zinazotumia taswira kuashiria uuguzi zinaelezewa katika sehemu hii. Methali 3*(a)* inatumia picha ya kiatu kama ishara ya kuuguza. Mtu anapotembea bila viatu anaweza kudungwa na miiba, kujikwaa vidole ama akapata jeraha kutokana na silaha ama vitu fulani kama upanda, mawe, mbao, msumari au shoka miguuni mwake. Mtu anapokumbana na hali kama hii ndio huwa anakumbuka umuhimu wa viatu kuwa vingemkinga kutokana na hali hii ya kuumizwa mguuni mwake. Taswira ya kuchukua tahadhari kabla ya hatari inajitokeza akili mwa mtu.

Mount Kenya University

Neno moto katika 3*(g),* linatumiwa kushiaria ugonjwa na maumivu yatokanayo na ugonjwa ule na pia linatumika kuashiria uuguzi. Picha ya aina mbili za mioto inajitokeza akilini mwa mtu ambapo moto unatumiwa kuuzima moto mwingine. Mtu anapougua ambao ndio moto huhitaji kuuguzwa ili apone. Ugonjwa huwa na uchungu mwingi na huhitaji dawa ambazo huwa chungu ili kuutuliza ugonjwa wenyewe. Ili kuuguza sehemu ya mwili ambayo ni jino linapouma, huhitaji kulitoa. Picha ya kung'olewa kwa jino inajotokeza wazi wazi. Ili kupata nafuu kutokana na ugonjwa unaomwathiri mgonjwa, yeye huhitaji kujua jinsi ya kuuguza ugonjwa ule, kama ilivyo suluhisho kwa kuling'oa jino liumalo taz. 3 ( i).

Mtu anapougua na kupata kidonda, huhitaji muda fulani ili kukiuguza kile kidonda. Mara nyingi kidonda hupona kwa hatua, na katika hatua fulani kwenye mchakato wa kupona kidonda huwa na gaga. Gaga ni weusi au rangirangi zinazoteakea mahali kuna kidonda kabla kidonda kipone kabisa. Asiyejua hatua hii katika mchakato wa kupona kwa kidonda anaweza dhani kidonda kimepona, ila si hivyo. Methali hii 3*(k)* inachora picha ya kuchukua kutahadhari mtu anapougua na kuwa na subra ya kutosha ili angojee kupona kikamilifu kabla ya kurudia shughuli zake za kawaida za kila kuchao.

Taswira ya kupona kwa ugonjwa unapomvamia mtu inachoreka bayana katika 3*(v).* Ili mtu apone baada ya kuuguwa, huhitaji subira ya muda mrefu. Subira inatumika kutoa taswira ya kule kungojea mtu anapougua. Kuna ile subra mtu humlazimu awe nayo wakati anauguzwa na muuguzi na kuna subira ya baada ya kuuguzwa. Mtu anapouuguzwa huhitaji kuwa na subira na kufuata maagizo yote anayopewa na muuguzi. Anafaa kufuata utaratibu anaopewa wa matumizi ya dawa na kliniki za kumtembelea muuguzi kila wakati anapopewa miadi na muuguzi wake. Pia subira huhitajika baada ya kupona ili kurejelea shughuli zake za kila siku kikamilifu.

Mount Kenya University

Methali teule 3(c, i, j, k na l) zinazotumia taswira kuashiria tiba. Maelezo yake yanatolewa katika sehemu iliyo hapa chini. Taswira ya jipu linalopasuliwa inajitokeza kama ishara ya tiba kutokana na ugonjwa wa jipu. Jipu ni uvimbe ambao hutoa usaha na huwa unawasha ndani kwa ndani unapomwathiri mtu. Ili mtu apone huhitaji kuchukua hatua ya kulipasua lile jipu kwa sindano na mara moja jipu linapopasuliwa, mchakato wa kupona huanza pale taz. 3(*c*).

Katika methali 3(j), inachora picha ya anayeumwa na jino na hatimaye kuling'oa. Pahala ambapo jino hung'olewa huwa kunaachwa pengo. Meno ni sehemu ya mwili ambayo ni muhimu kwa kuwa husaidia kusaga chakula, kuongea na husaidia kumpa mtu sura nzuri ya uso. Kwa sababu hizi, jino linapong'olewa wakati mwingine huwa ni bora kutafuta tiba ya lile pengo na ndipo wakati mwingine mtu huwekwa jino la pembe ya ndovu ama la chuma. Jino hili la kuwekwa haliwezi kuwa kama lile na mwanzo na huhitaji kubadilishwa baada ya muda fulani ndiposa haliwezi likawa tiba ya milele ya lile pengo lililoachwa.

Taswira ya kutaataa na kufa inachomozwa na methali hii ya 3(l). Kifo cha mtu hutokana na sababu nyingi, mojawepo ikiwa ugonjwa unapomwathiri mtu. Kabla mtu afe huwa anatoa dalili fulani za kuashiria ako katika hali mahututi na huenda akaaga. Kule kufurukuta na kuwayawaya sio tiba ya kufa ila kama ugonjwa umemwathiri kwa kiwango kikubwa ataaga hatimaye.

Methali 3 (h, i, j, p) zinatumia sehemu za mwili kama vile ulimi, dole na jino kuleta ujumbe unaosawiri ugonjwa uuguzi na tiba katika methali teule kwa matumizi ya kipengele hiki cha taswira. Taswira zinazojitokeza ni madhara yanayoweza kuletwa naviungo fulani vya mwili vikiathirika na magonjwa na jinsi viungo vingine vinavyoweza kuleta madhara kwa viungo vingine. Ulimi unaweza kuleta jeraha katika moyo wa mtu unapotumiwa kutoa maneno

Mount Kenya University

mambaya au maovu. Magonjwa mengine kama vile kuumwa na jino suluhu lake ni kuling'oa lile jino linalouma ili mtu aweze kupona.

Katika methali 3(o, s, na t) zinatumia taswira kwa kutumia viumbe kama vile ng'ombe, kinyonga na nzi ili kuwasilisha ujumbe unaosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Viumbe hawa wanajulikana na wanajamii na kwa hivyo ujumbe wa methali zinazorejelea viumbe hawa vitaeleweka kwa urahisi. Kinyonga na mwendo wake wa pole pole anashadindia jinsi ambavyo ugonjwa huchukua muda kabla utoke mwilini mwa mtu, anapougua. Ng'ombe ni mnyama anayefugwa nyumbani na huwa na faida nyingi kwa mfugaji na kwa jamii kama vile maziwa, nyama na ni kiashiria cha utajiri, anapougua faida zake hizi huwa hazipatikani na hujikokota hadi zizini na kulala akingojea msaada. Hii inatoa taswira ya jinsi ugonjwa humfanya mtu aliye na manufaa mengi kwa jamii abaki hoi na wakuomba msaada na sijiweze kwa lolote. Nzi na kimo chake kidogo huwa anang'ang'ana kutafuta mlo wake mahala popote anapotumaini kuupata hadi anaelekea kwenye kidonda anapopatana na kifo chake. Kiumbe huyu anachora taswira ya kuhatarisha maisha na kutia juhudi hadi kupata kile mtu atakacho hata kama kuna hatari.

Taswira husaidia kugadisha picha akilini na kunasisha ujumbe wa methali teule kwa wanajamii au wasikilizaji. Picha tofauti tofauti zinaibuka akilini mwa msikilizaji, anaposikia methali hizi zikitumiwa kama vile mtu akidungwa na mwiba, nzi akifa juu ya kidonda, anayeenda polepole na kwa utaratibu, mtamabao wa kinyonga, kuzunguka mbuyu. Hizi ni baadhi ya taswira zinazojitokeza katika methali hizi teule.

Kwa mujibu wa muhimili wa kiishara katika nadharia ya simiotiki mtafiti anabaini kuwa viashiriwa vinavyotumika kuzijenga taswira hizi zilizo katika methali teule, hubeba maana ya ndani inayoakisi jamii husika. Khatib (2014) akitalii dhamira zinjengwazo na taswira katika

methali za wapemba, amechunguza methali zilizotumia fani hii ya taswira na kugundua aina mbalimbali za taswira zimetumika kama vile taswira za kibotania, kisaikolojia, kizuolojia, kijiolojia, kiastronomia, kiteolojia na katika vitu vya kawaida. Katika utafiti huu tunazingatia taswira ya vitu vya kawaida kama vile kiatu, kitanda, mwiba, jina, dawa na moto ili kutolea taswira zilizo katika methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Kwa kurejelea kazi ya Abrahams (1999) na Cuddon (2013) wanaainisha aina za taswira kama vile taswira sikivu, joto, baridi, mnuso, oni, muojo na safari. Katika utafiti huu tumeangazia taswira katika ujumla wake bila kuainisha katika aina zake mbalimbali.

Akiangazia kipengele hiki, Farida(2018) amechunguza taswira zinazojitokeza katika methaliza kiswahili kwa ujumla wake kama vile; taswira za wanyama, taswira za matunda, taswira zinazazotokana na mazimwi, nyoni, wadudu, makao, silaha na hatimaye za viungo mbalimbali vya mwili.

Kutokana na kazi za watafiti hawa, mtafiti wa kazi hii amesaidika na kutambua kwamba taswira ni kipengele muhimu katika methali zinazofanyiwa utafiti na husheheni ujumbe maalamu wa kiteolojia na vilevile za vitu vya kawaidaa kuchorea mwanajamii picha akilini mwake zinapotumika kwa kurejelea muktadha wa yanayosemwa ama kujadilianwa katika jamii kama vile kitanda kinachora picha akilini mwa mwanajamii na kuona jinsi mgonjwa hujilaza kitandani anapougua, mwiba nao unatucholea picha ya maumivu yanayoletwa na mwiba na hata kulemaa kunakoweza kutokana na kudungwa na mwiba wenye sumu.

Ibrahim, Nyandiba na Mohochi (2021) wakichunguza taswira kama kipengele mojawepo ya vipengele vya kifani katika fasihi ya watoto, waliangazia picha kama kipengele cha fani katika fasihi ya watoto na mwingilano uliopo baina ya picha na taswira. Waligundua kuwa

taswira inapofungamanishwa na picha hufanya maana katika riwaya za watoto kueleweka kwa urahisi na hadhira lengwa ambayo ni watoto. Kazi hii kuntu inasaidia mtafiti wa utafiti huu kwani kuna picha ambayo hujengeka katika akili za mwanajamii anayetumia methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba ambazo husaidia kueleweka kwa urahisi maana zinazobebwa na methali hizi.

### 4.1.4 Sitiari

Sitiari kama vipengele vinginevyo vya fani katika fasihi, hulinganisha vitu viwili au zaidi zilizo na sifa tofauti kama ilivyo katika tashibiha. Tofauti iliyoko kati ya sitiari na tashibihi ni kuwa sitiari huwa haitumii viunganishi; mithili ya, kana kwamba, kama, sawa na na vinginevyo (Msokile, 1993). Naye Msokile (1992) anaielezea sitiari kuwa tamathali ya usemi ambayo kimsingi huhusisha matendo, vitu ama tabia za vitu vyenye maumbile yasiyolandana.

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo hulinganisha dhana mbili au hata zaidi, ijapokuwa dhana hizo huwa na sifa zisizofanana bila matumizi ya vilinganisha. Ulinganishi huu wa kiistiari huifananisha dhana moja na nyingine moja kwa moja na mara nyingi hutumia neno ‘ni’ katika ulinganisho wake (Wamitila, 2003).

Mutiso (2005) naye anaeleza kuwa sitiari ni mbinu ya kulinganisha vitu kwa kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia. Huu mlinganisho hauhusishi maneno; kama vile, mithili ya, kama na visawe vyake..

Wamitila (2008:421) katika kazi yake nyingine anasema kuwa, msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana. Kwa hivyo ili uchunguzi wa sitiari uweze kukamilika, ni lazima kuchunguza dhana tatu muhimu katika sitiari; kilinganishi yaani kile kinachotumiwa kama msingi wa

kufananisha, pili ni kilinganishwa yaani kile kinachofananishwa na hatimaye ni msingi yaani sifa yenyewe ya ulinganishi.

King'ei (2003) na Robinson (2003) wanadai kuwa methali hujaa sitiari na hutumika katika mazungumzo kwa nia ya kuasa, kutoa elimu na hata kutoa kejeli kwa njia ambayo imefubwa na kuwekwa tasfida. Samwel na wenzie (2013) wasema kuwa sitiari pia huitwa istiara, istiari ama jazanda hii ni tamathali ya usemi (maneno, kirai au miundo) inayaotumika kutoa picha fulani katika akili na inayotoa athari fulani au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira.

Mutiso (2005) naye anaeleza kuwa sitiari ni mbinu ya kulinganisha vitu kwa kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia. Huu mlinganisho hauhusishi maneno kama vile, mithili ya, kama na visawe vyake.

Mwakio (2016) naye anatoa maana ya sitiari na kusema kuwa ni mlinganisho wa moja kwa moja ambao hutokea kwa kuhamisha maana ya tabia, sura, sifa umbo au muundo fulani kutoka kwa kitu kimoja hadi kwenda kwa kitu kingine. Sitiari ni tamathali ya usemi itumikayo katika kulinganisha vitu viwili vilivyo na sifa tofauti bila ya matumizi ya viunganishi vya ufananisho kama ilivyo katika tashibiha (Kyando, 2013).

Akiangazia tamathali za usemi na taswira za Ukimwi katika Utenzi wa Zimwi ulioandikwa na Abdulkadir, Timammy (2020) anatoa maelezo ya jinsi sitiari imetumika kulinganisha Ukimwi na zimwi ambaye ni kiumbe wa kufikirika apatikanaye katika hadithi za fasihi simulizi za Waswahili. Kiumbe huyu ni mkubwa kimwili kwa njia ya kustaajabisha, hutia kiwewe na humeza na kuwamaliza binadamu. Ukimwi unalinganishawa na zimwi kwa

Mount Kenya University

minajiri huangamiza watu wengi. Uchunguzi huu unasaidia uchunguzi wetu kwa kutupa mwongozo wa jinsi ya kuangazia kipengele cha sitiari katika methali teule.

Kahigi (2020) anaeleza kuwa sitiari ni kipengele kinachotumia kitu kimoja kurejelea kitu kingine. Kwa kimsingi, isitiari hutumia mfananisho wa vitu viwili kwa minajili ya kutumia dhana moja kurejelea dhana nyingine iletayo uhamishaji wa maana.

Tunapozingatia fafanuzi za wataalamu hawa tunaweza kutoa maana ya sitiari kuwa ni mlinganisho wa moja kwa moja ambao hutokea kwa kuhamisha maana ya sifa, tabia, sura, muundo au umbo fulani kutoka kwa kitu kimoja kwenda kwa kitu kingine. Vitu ambavyo hulinganishwa huchukuliwa kuwa ni sawa sawa kabisa na havina tofauti yoyote ile.

Katika mfano twawezasema Zedi ni fisi. Katika mfano huu mienendo ya fisi ya ulafi imehamishwa hadi kwa Zedi ambaye alionyesha tabia ya ulafi alionayo. Sitiari kwa sehemu kubwa hufanana na tashbiha ila hulandanisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi vya; mithili ya, sawa na na kama. Vitu, hali au watu hulinganishwa na vitu, hali au watu wengine kana kwamba vitu, hali au watu hao ni sawa kabisa.

Nia kuu ya matumizi ya sitiari ni kutoa picha ya uhusiano ama ulinganisho uliopo wa vitu, hali au watu tofauti tofauti katika kujenga uzito wa maana. Muundo wa isitiari hujengeka katika sehemu tatu kuu; kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi. Mambo haya matatu yanapaswa kuhusiana ndio ujumbe uliokusudiwa ufasirike vifaavyo. Maana inayojitokeza kutokana na isitiari hutegemea muktadha wa matumizi ya isitiari inayohusika.

Kuna aina mbalimbali za isitiari kama vile isitiari kuu, isitiari chakavu, isitiari kikaida, isitiari hisimseto, isitiari sahili, isitiari radidifu, isitiari mseto, isitiari changamano na isitiari ya

dhana.Katika utafiti huu tunaangazia isitiari katika ujumla wake bila kuzingatia aina mbalimbali za isitiari.

Methali teule katika 4 (a-ii) zinaashiria matumizi ya isitiari kuwasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa, uuguzi na tiba:

**4.**

a) *Baada ya kifi ni tabibu.*
b) *Baniani mbaya kiatu chake dawa.*
c) *Buyu kali ni dawa ya mwana mimba.*
d) *Dawa ya jipu kulipasua.*
e) *Dawa ya moto ni moto.*
f) *Dawa ya deni ni kulipa.*
g) *Dawa ya hasira ni kicho.*
h) *Kinga ni bora kuliko tiba.*
i) *Kipendacho roho ni dawa.*
j) *Mapenzi kikihozi hayawezi fichika.*
k) *Maradhi huja shoti yakitoka ni mtambao wa kinyonga.*
l) *Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda.*
m) *Neno jiwi ni jeraha la moyo.*
n) *Neno ovu ni jeraha la moyo.*
o) *Penzi la moyo ni dawa.*
p) *Sahau ni dawa ya waja.*
q) *Ugonjwa ni suna, kufa ni faradhi.*

r) *Afichaye ugonjwa hazai*

s) *Daawa si dawa.*

t) *Yaliyopita si ndwele ganga yajayo.*

u) *Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa.*

v) *Jino la pembe si dawa ya pengo*

w) *Kipendacho moyo ni dawa*

x) *Kuzuia ni bora kuliko kuponya*

y) *Maneno mengi maradhi*

z) *Mkimbilia sheria hujiponya*

aa) *Mwana mui dawa ya mlango.*

bb) *Nduli na mchimba dawa shauri lao ni moja*

cc) *Nia njema taibu,nia mbaya harabu*

dd) *Sahau ni dawa ya waja*

ee) *Sikio la kufa haliskii dawa.*

ff) *Mwenye kovu haliwai na kidonda*

gg) *Mwenye kovu haliwai na kidonda*

hh) *Ukiona ambari na zinduna ipapo.*

ii) *Ukiona zabadi na zinduna i papo.*

Methali teule zinazotumia isitiari kurejelea ugonjwa ni 4*(j, k, l, m, n, q).* Methali 4*(j)* inatumia ugonjwa wa kukohoa kuulinganisha na zile hisia za mapenzi. Hili ni kwa kuwa ugonjwa huu wa kukohoa unapomwathiri mtu hutoa sauti kubwa kwa mdomo anapokohoa inayosikika na kila mtu aliyekaribu. Mapenzi nayo huwa kama kile kikohozi ambako hisia za mahaba huwa hazifichiki kwa

wapendanao. Anayempenda mwingine hata akijaribu kuficha hisia za mapenzi, huwa ni kwa muda mfupi kisha anashindwa kuficha penzi lake na linajulikana na kuonekana wazi na anayempenda na wengine walio karibu.

Neno shoti katika 4*(k)* limetumika kulinganisha ile kasi ambayo ugonjwa huingia mwilini mwa mtu. Maradhi huingia mwilini mwa mtu mara moja tu kwa ghafla au haraka sana na kufanya hali na afya yake kubadilika kwa kiwango kikuu. Si ajabu kupata mtu akiwa katika hali nzuri na yenye afya na baadaye kidogo yule mtu akawa katika hali mahututi, hajijui, hajifahamu. Vile vile mwendo wa kinyonga ambao huwa ni wa polepole sana, umetumika kiistiari kuashiria jinsi ambavyo kuuguza ule ugonjwa huwa mwendo wa polepole na huchukua muda mrefu kabla mtu apone.

Mount Kenya University

Katika 4*(l),* isitiari imetumika kuashiria uhusiano uliopo baina ya mgonjwa na kitanda. Neno mwenzi ambalo linaashiria uhusiano wa karibu kama wa urafiki baina ya kitanda na mgonjwa. Uhusiano huu wa karibu hujitokeza kwa lazima kwani mgonjwa anapougua hulazwa kitandani hadi atakapopona. Hii ni kwa kuwa kitanda ndio sehemu ambayo huwa tulivu na iliyo na godoro laini ambalo mgonjwa anaweza kupata tulio la muda anapouguzwa.

Katika 4*(m,* na *n),* Kuna maneno ambayo yakinenwa kiholela huwa yanaumiza moyo wa yule anayeambiwa. Maneno haya huwa maovu na huwa yanakata kama msumeno katika hisia na moyo wa mtu na jeraha la moyo ambalo huwa linaaacha madhara moyoni mwa mtu kwa muda mrefu. Kama vile silaha, mfano upanga, hukata na kuacha , ndivyo maneno maovu madhara yake yanafananishwa na jeraha linaloachwa na silaha. Jeraha la moyo laweza kosa kuonekana kwa macho ya mtu lakini uchungu ambao huachwa moyoni mwa mwathiriwa huwa ni makubwa sana.

Methali teule inayotumia isitiari kurejelea uuguzi 4*(h).* Neno 'kinga' linatumika kuashiria kuzuia. Kabla ugonjwa huja mwathiri mtu sana , huwa kuna dalili ambazo hujitokeza mwanzoni, kama vile ulegevu mwilini, uchungu katika viungo mbalimbali vya mwili, kukohoa, kisunzi, kuhara na ishara nyinginezo. Anayeugua akizingatia dalili hizo anaweza kutafuta uuguzi kabla ya kuathirika zaidi. Mgonjwa anapochelea kutafuta tiba wakati unaofaa, ugonjwa hujikoleza mwilini na hatimaye mwili huishiwa na nguvu na kudhoofika kiwango cha kutojiweza tena. Hapa mgonjwa huhitajia kumtembelea muuguzi ili atibiwe. Kutibu ugonjwa huwa ni ngumu na huchukua muda mrefu kuliko kuzuia. Sitiari inatumika kulinganisha hali mbili ambazo ni kinga na tiba. Ubora na umuhimu wa kinga unadhihirika kwani huzuia madhara yanayoweza kutokana na kutochukua tahadhari kabla ya ugonjwa kumwathiri mtu sana.

Methali zinazotumia isitiari kurejelea tiba ni 4*(b, c, d, e,f, i, o na p)*. Katika 4*(b)*, maneno *buyu kali* yanatumika kulinganishwa na ukali au uchungu wa dawa. Mbuyu ni mti uliohusishwa na imani na itikadi za jamii ya Waswahili. Jamii hii iliamini kuwa mizimu ya wafu na majini walikaa katika ule mti. Pia mtu huu huwa unaishi kwa muda mrefu sana kuliko miti mingine. Mti huu ulikuwa na faida kochokocho kwa jamii kwani ulitoa mboga kwa matawi yake na pia ulitoa kivuli wakati wa jua. Neno buyu linatumika kiisitiari kurejelea dawa kama tiba. Dawa hutegenezwa kutokana na mchanganyiko wa kemikali na chuma mbalimbali ambazo huwa ni kali ili kuua viini kama vile bakteria , protozoa, fungi na virusi ambavyo husababisha ugonjwa. Buyu ni tunda la mbuyu na matunda haya huwa matamu yanapokomaa na kuiva. Matunda haya yakiwa bado hayajakomaa huwa machungu sana na hutumika kama dawa ya kutuliza uchungu unaotokana na maradhi. Mama aliye na mimba analinganishwa na mtu anayeugua maradhi fulani na anahitaji kutibiwa. Mara nyingi mimba huandamwa na changamoto nyingi za kiafya kutokana na mabadiliko ya homoni mwilini mwa mwanamimba. Ili kutuliza changamoto na maumivu yatokanayo na uja uzito, mwanamimba hubidi avumilie uchungu wa buyu ili maumivu yatokanayo na mimba yamuache.

Methali 4*(c, d, e, f)* zimetumia neno dawa kulilinganisha na suluhisho za hali tofauti. Katika *(c)* neno dawa kama tiba ya ugonjwa wa jipu. Ugonjwa huu huwa ni uvimbe ambao hufura kwenye ngozi ya mwili wa mtu na hutoa usaha ambao hunuka, na huwa na uchungu mwingi. Ili mtu aweze kupona, jipu hili huhitaji kutibiwa na linapopasuliwa hata bila kwenda kutafuta uuguzi kutoka kwa mganga huwa linapona. Neno dawa katika (*d), (e) na (f)* linatumika kama isitiari kulinganisha tiba na hali tatu ambazo ni deni, moto na hasira. Mtu akiugua na afya yake kudhoofika, huwa anakaa katika ile hali hadi atakapotafuta tiba. Kama vile ugonjwa humwadama mtu ndivyo mtu akiwa na deni huwa anaandamwa na lile deni kila wakati. Deni

laweza kuwa la kifedha, la hisani fulani uliyotendewa na mtu ama ya ahadi mtu alimpa mwingine. Ili lile deni liweze kuisha, tiba ama suluhisho lake ni kuilipa ile deni. Mtu akilipa deni huwa hajifichi tena kutoka kwa wale waliokuwa wakimdai na huwa na amani ndani ya roho yake kwa kufahamu kuwa hakuna anaye mdai kwa lolote wala chochote. Katika *(e)* neno moto linatumika mara mbili, kulinganisha hali mbili, neno moto katika kipande cha kwanza cha methali hii *dawa ya **moto,*** neno hili linalinganisha ugonjwa na uchungu utokanao na ugonjwa. Moto kwa kawaida huwa ni kitu ambacho huwaka kutokana na nishati. Moto unapowaka huchoma chochote kilicho karibu. Katika kipande cha pili cha methali *ni **moto,*** neno hili linalinganisha moto na ukali wa dawa ambayo inahitajika kuuponya ule ugonjwa ama uchungu unaoletwa na ugonjwa. Dawa huwa kali na hulazimu mgonjwa azimeze ili apone.

Neno penzi katika *(o)* linalinganisha penzi na dawa. Penzi ni ule msukumo au mvuto wa hisi za moyoni kuhusu mtu au kitu fulani. Msukumo huu huwa mkubwa hivi kwamba mtu akikosa kumpata yule mtu ampendaye au kitu akipendacho huwa hana amani moyoni na hana furaha yoyote. Kule kutotulia na kukosa furaha na amani moyoni kunalinganishwa na ugonjwa ambao unahitaji tiba. Wakati mtu anapompata ampendaye au akipendacho huwa roho yake inafurahia, kuwa mchangamfu na kila aliyekaribu naye bila shaka atagundua roho yake imejaa furaha. Kupata kile mtu akipechando ama amupendaye kweli ni dawa ya moyo.

Katika *(p)* neno 'sahau' linatumika kulilinganisha na dawa kwa mwanadamu. Kila siku mtu hupitia mazuri ambayo angependa kuyakumbuka kila siku ya maisha yake. Pia mtu hupitia madhila na mambo magumu ambayo angependa kuyasahau haraka iwezekanavyo. Mambo mengine kama vile kifo, ajali, kuachwa na umpendaye, kupoteza kazi, kutengwa na wandani na mengine kama haya ambayo ni hasi huwa ni ya kuhuzunisha, kuatua moyo na kila mtu

ayakumbukapo machozi humtiririka kuwili hata bila hiaria yake mwenyewe. Baada ya muda fulani kadiri muda unavyoyoyoma, mtu huweza kusahau yale yote aliyopitia na roho kutulia. Katika maumbile ya mtu, akili za mtu zinauwezo wa kukumbuka mambo fulani kwa kipindi fulani kisha akayasahau. Huku kusahau kumefananishwa na dawa kwa kuwa kupitia kusahau kule moyo hurejelea na hali ya kawaida na kuweza kuendelea na maisha yake.

Ugonjwa ni hali ambayo humpata kila binadamu katika jamii. Wakubwa kwa wadogo, maskini kwa matajiri, hujipata katika hali hii katika kipindi fulani katika maisha yao. Hii ndio maana sitiari imetumika kwa kiwango kikubwa katika methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba kwa kuwa jamii ya Waswahili walifahamu kuwa ujumbe ulio katika methali hizi utawafikiwa wanajamii wengi na itakuwa ni rahisi kwao kuuelewa ujumbe wenyewe.

Nsookwa (2011), akiangazia kwa kina zaidi kipengele cha sitiari zilizo katika methali za Kiswahili na zilizo katika methali za Kiganda, anachambua na kubainisha ishara zitokanazo na matumizi ya sitiari katika methali hizo. Ijapokuwa ameangazia matumizi ya isitiari kwa ujumla wake katika methali za Kiswahili na za Kiganda, kazi hii imesaidia utafiti huu kwa kuwa methali zinazofanyiwa utafiti katika kazi hii zimesheheni sitiari kwa kiwango kikuu. Hili ni kutokana na ajiri kwamba methali tunazozichambua zimetumia maneno ambayo yametumiwa kama viashiria vya ujumbe unaonuiwa kuwasilishwa na methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba, kama zinavyoorodheshwa hapo mbeleni katika sehemu hii.

Kwa mujibu wa Msokile (1992) sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwa kawaida inahusisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti. Ulinganisho huu unazingatia misingi au sifa inayopatikana au zinazopatikana katika vitu vyote viwili, lakini sifa hizo haziwi wazi kati ya kitu na kitu.

Mount Kenya University

Sitiari husaidia kujenga picha akilini mwa mtu, picha ambayo hutoa athari fulani kwa kuamsha mwitikio wa ujumbe kwa mtu katika matumizi ya methali hizi teule. Kwa njia ambayo inajificha na iliyo na tasfida, sitiari pia husaidia kujenga kejeli katika kuwasilisha ujumbe wake.

#### 4.1.5 Kinaya

Kejeli ni tamathali itumiayo maneno ambayo kwa kawaida huwa kinyume sana na maana kamili ya maneno yenyewe yanayotumiwa (Msokile, 1993). Kejeli inaweza kugawika katika makundi matatu ambayo ni; kinaya drama, kinaya rahisi na kinaya inayoeleza ajali. Katika utafiti huu tunaangazia kinaya kwa ujumla wake kuchunguza methali teule katika usawiri wa ugonjwa uuguzi na tiba.

Mbatia (2000) anaeleza kinaya kuwa kimsingi hutumiwa kutilia mkazo na vilevile huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo jinsi mambo yaonekanavyo na jinsi yalivyo hasa katika fasihi ya kishatiti. Nao Mwangi na Wamalwa (2016) wanaeleza kinaya kama matumizi ya maneno yaliyo na ukinzani wa anavyodhamiria msemaji. Kwa hivyo, hapa mwandishi au msemaji hujenga ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa.

Baldick (2001) naye katika kutolea kinaya maana anasema kuwa ni hali ambapo futuhi tatizi inadhihirika hivi kwamba kauli ambayo huwa ya moja kwa moja hudindimizwa na muktadha uliopo na kwa hivyo kutoa muonekano ambao ni tofauti kabisa.

Kwa mujibu wa Mbatia (2008) kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi ambavyo mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo sasa (uhalisia wake). Kinaya hutumika mara nyingi kukebehi au kukejeli mtu, tabia au mwenendo wa mtu fulani. Kinaya

Mount Kenya University

huhitaji uelewa wa hali ya juu wa mtu ili kuweza kupata maana inayoletwa na maneno yaliyotumiwa.

Kuna aina tatu za kinaya; kinaya cha kiusemi, kinaya cha kidrama na kinaya cha kihali. Kinaya cha kiusemi hujidhihirisha ambapo matendo ya wahusika hujitokeza yakiwa kinyume na matarajio ya msomaji. Kinaya cha kidrama ni pale ambapo matendo au hali fulani hujitokeza katika drama ambazo wahusika hawaelewi ya kwamba zinatokea ilhali msomaji au hadhira ina fahamu kutokea kwake. Na hatimaye kinaya cha kihali ni pale ambapo wahusika hufanya matendo ambayo ni kinyume na matarajio ya msomaji au hadhira. Kwa maoni yetu kinaya ni kipengee cha kifani ambacho maana inayotolewa na maneno yanayotumika hutoa maana iliyo kinyume cha msamiati uliotumiwa.

Oiko (2017) katika uchaganuzi wa mtindo katika tamthilia za Arege amegundua kuwa kipengele hiki cha kinaya kinatumika sana katika kazi hizi kuwakejeli Waafrika unaoufuata ukoloni mamboleo kikasuku. Pia anatumia kipengele hiki kuonyesha kuwa Waafrika ndio chanzo cha madhila wanayokumbana nao katika kila sehemu ya maisha yao. Utafiti huu unasaidia kuelewa kinaya kwa kina na jinsi kipengele hiki hutumika kuwasilisha ujumbe katika methali teule.

Katika uchunguzi wao  wa Uchanganuzi wa toni katika Ushairi wa Kithaka  wa Mberi, Ongarora na wenzake (2020) wameangazia kinaya kama mojawepo ya toni za kuwasilisha ujumbe unaohusu mtazamo au mawazo fulani katika ushairi huu na kuibua athari kubwa inayokusudiwa na mwandishi. Kazi hii haijatusaidia mno kwani inaangazia kinaya kama toni ilhali katika utafiti huu kinaya kinachunguzwa kama kipengele cha kuwasilisha ujumbee maalum katika methali teule.

Methali teule zilizosheheni kinaya kuwasilisha ujumbe unaosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba ni 5(a-ii)

**5.** *(a) Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu.*
*(b) Baada ya donda msumari moto.*
*(c) Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda.*
*(d) Mali ya mgonjwa faida ya mfumu.*
*(e) Mganga hajigangi.*
*(f) Shibe ya waganga hutoka kwa wagonjwa.*
*(g) Utamu wa kidonda umemwua nzi.*

Methali zinazowasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa kwa matumizi ya kipengele cah kinaya ni 5*(a, b, c* na *g).* Kila siku, mtu huwa anajikita katika shughuli mbalimbali za kujitafutia kipato cha kila siku kama vile ukulima, biashara, kazi za ofisini, katika viwanda na kwingineko. Katika shughuli hizi mtu hukumbana na hali tofauti tofauti ambazo zinaweza kuweka maisha yake au afya yake hatarini. Kuna viwanda ambavyo hutumia kemikali mbaya sana kama malighafi kuunda bidhaa zake na vingine hutengeneza bidhaa zilizo na makali kama vile misumari, visu, mabati na kadhalika. Katika ukulima mtu anapolima, pale shambani mtu anaweza kukumbana na mawe na kujikwaa ama anaweza kudungwa na mwiba. Ili asidungwa na miiba, mtu huhitaji kujikinga kwa kuvalia viatu ili asipate madhara yoyote anapofanya kazi au kutembea mle. Viatu huwa ni muhimu sana kwani ni aina ya vazi ambalo huvaliwa miguuni ili kujikinga na madhara kama vile kujikwaa vidole na kudungwa na vifaa vilivyo na makali. Ni kinyume na matarajio ya kwamba baada ya mtu kudungwa na mwiba na kuumizwa ndipo anapokumbuka umuhimu wa viatu taz. 5(a).

Katika 5*(b)*, mtu anapoathirika na ugonjwa fulani mwili wake huwa unadhoofika, afya yake kudindimia na huishiwa na nguvu na humlazimu kuuguzwa ili apone. Magonjwa mbalimbali huchukua muda tofauti kupona ili mtu arejelee hali yake ya kawaida. Kuna yale magonjwa huchukua muda mrefu sana kupona na mengine muda mfupi na hata mengine hayaponi na

Mount Kenya University

mtu huishi nayo hadi kufa kama vile saratani, Ukimwi na kisukari. Ni matarajio ya kila mtu kupata nafuu na baadaye kupona. Mtu anaweza kuugua ugonjwa ambao utamlazimu kwenda nchi za nje kama India, Ulaya ama Marekani kutafuta matibabu. Huwa ni bei ghali mno kumpeleka katika yale mataifa na kulipia gharama ya matibabu pia huwa juu sana. Baada ya kupelekwa kule na kukaa kwa kipindi fulani baadaye yule mtu anaweza kosa kupoana na hatimaye hufia kule na kurudi akiwa kwa jeneza. Ni kinyume na matarajio ya wengi kwamba baada ya kupata mahangaiko ya kwenda kutafuta uuguzi na harasa kubwa ya matibabu ya yule mtu, anafia kule nchi za ng'ambo na kurudi akiwa maiti.

Kidonda ni aina ya ugonjwa ambayo humwathiri mtu na hutokana na kukwaruzwa au kukatwa sehemu fulani ya mwili na kitu chenye makali kama kisu, msumeno au chuma. Kidonda hutoa usaha unaonuka na huvutia nzi. Kikwapa ni harufu mbaya ambayo hutoka katika sehemu ya mwili iliyo chini ya bega, iitwayo bega. Harufu hii tutokea baada ya kutoa jasho nyingi, ikiwa mtu amefanya kazi nyingi, ametembea kwa kasi muda mrefu ama kukaa mahali palipo na joto nyingi. Kikwapa pia huwa ni uvundo utokao kwenye kidonda kabla hakijapoana. Ni matarajio ya kuwa na ule mnuko wa kikwapa mahali palipo na kidonda, lakini ni kinyume na matarajio pasipo na kidonda kuwe na ule uvundo utokanao na kidonda taz. 5(c).

Nzi ni kiumbe mdogo ambaye huruka kwa mbawa zake na hupenda sehemu zilizo na uchafu na hueneza magonjwa yatokanayo na uchafu. Nzi huruka kutoka sehemu moja chafu hadi nyingine akitafuta chakula. Kidonda hutoa uvundo na usaha ambavyo humvutia nzi hata akiwa mbali. Katika shughuli zake za kutafuta chakula hupatana na mtu aliye na ugonjwa wa kidonda na kutua pale ili kula ule usaha utokao kidondani. Mbawa zake huweza kukwama

kwenye ule usaha ambao huwa na mnato na hatimaye hufia pale. Ni kinyume na matarajio kuwa ule utamu wa chakula chake nzi hatimaye humuua yeye taz. 5(g).

Methali zinazowasilisha ujumbe unaorejelea ugonjwa kwa matumizi ya kipengele cha kinaya ni 5 *(d,e na f)*. Mganga ni mtu aliyenaweledi wa hali ya juu katika kuuguza na kutibu magonjwa mbalimbali. Watu wote walioathirika na magonjwa humtegemea yeye na wosia wake ili kupata tiba. Magonjwa nayo huwa hayatambui kabila, umri, cheo, jinsia au taaluma ya mtu na yanaweza kumwathiri yeyote wakati wowote. Licha ya kwamba mganga huwa na ujuzi mwingi wa kuuguza na kutibu magonjwa aina nyingi, yeye pia huugua na huhitaji tiba. Baadhi ya waganga huugua magonjwa yale yale ambayo wao hutibu wagonjwa wengine na kupona. Wengine huugua na hatimaye hufa kutokana na magonjwa kama hayo. Ni kinyume na matarajio ya wagonjwa wale huwa wanatibiwa na mganga yule ya kwamba mganga yule auguapo yeye mwenyewe hawezi jitibu na kupona ila hutafuta matibabu kutoka kwa waganga wengine taz. 5(e). Wakati mwingine humbidi alipe gharama kubwa kutibiwa ugonjwa unaomwathiri. Si ajabu kuwa kuna mganga ambaye huishi na ugonjwa ambao alikuwa anatibu alipokuwa na afya njema na hatimaye kuaga dunia kutokana na ugonjwa uo huo.

Katika 5*(d na f)*, maneno ‘mfumu’ na ‘waganga’ yanarejelea watu ambao hutoa matibabu kwa wawele. Watu hawa huwa na ujuzi wa kiwango cha juu kuuguza na kutibu wagonjwa na huwa ni tegemeo katika jamii kwa taaluma hii yao. Ndio mgonjwa aweze kutibiwa huhitaji kutoa gharama fulani ili aweze kupokea uuguzi au tiba kutoka kwa mfumu au mganga. Malipo haya mara nyingi huwa ghali mno na huwa ni lazima yatolewe kabla mgonjwa hajaganguliwa. Mgonjwa wakati mwingine huhitaji kuomba msaada ili asaidiwe kupata fedha za gharama ya uuguzi. Mtu anapouguzwa huwa si lazima apone kwa kuwa kuna uwezekano wa kutopona na kuishi na maradhi yale. Pia mgonjwa anaweza kuaga dunia hata baada ya

kutumia fedha nyingi. Yale malipo ambayo mfumu au mganga hulipwa huwa hayarudishwi hata kama mgonjwa atakufa. Waganga wengi huwa wanapata fedha nyingi sana kutokana na huduma zao za kuuguza na kutiba wagonjwa. Waganga wasipopata wagonjwa, kazi yao itakosa maana na wao pia watakosa mali na utajiri utokanao na kazi yao. Ingawa wagonjwa huwa wanawatembelea bila hiari ila ni kwa sababu ya magonjwa, waganga wakiwaona wale wagonjwa wamepiga foleni ndefu kutafuta matibabu, nyoyo zao hudunda kwa furaha kwani wanajua kwao wingi wa wagonjwa ni shibe kwao. Matarajio ya jamii ni watu waishai bila magonjwa lakini ni kinyume na matarajio ya jamii kwa waganga kwani wao kila asubuhi huamka wakitarajia wagonjwa ili wapate lishe lao la kila kuchao.

Kinaya hutoa ujumbe kwa njia ya kukebehi au kukejeli hali ya kutomakinika kwa mtu na pia fani hii inatumika kutoa ujumbe ulio kinyume na matarajio katika methali teule.

### 4.1.6 Kwelikinzani

Baldick (k.s.t) anatoa maelezo ya kwelikinzani kama kauli au matamshi ambayo kwa njia ya kushangaza ambayo huimbua mgongano na kujikinza kiasi cha kuchochea kuwaza juu ya muktadha mwingine ambamo hali iliyoelezwa inaweza kuwa ukweli. Kwa mfano, “mtoto ndiye baba wa mwanamume.” Pia mfano mwingine, ni kweli kinzani kuwa ‘alikuwa mtu mpweke aliyependa kupiga gumzo na wageni.’ Dhana hii ya kweli kinzani huweza kueleza mtu au hali fulani ambayo ina sifa wazi za ukinzani. Katika utafiti wa kwelikinzani mambo mawili ya kimsingi huhitajika (Wamitila 2008). Mwanzo ni kufahamu maana ya juujuu yanayoashiria ukinzani wenyewe na pili maana ya kindani ambayo hukusudiwa na mtumizi kumpasha msikilizaji ujumbe.

Kutokana na ufafanuzi huu, ni bayana kuwa kwelikinzani ni kauli ambayo inasheheni mawazo mawili ambayo hufanya hali kuwa isiyowezekana kamwe au isiyo ya kawaida, hata kama huenda ikawa ni kweli. Ni kweli ambayo bado ni kama uongo, neno mbalo linajitokeza kama ni la kinyume ilhali ni sahihi. Laweza semwa kuwa ni fumbo la maneno. Kitu, mtu au hata hali ambayo ina sifa mbili au zaidi ambazo ni kinyume na kwa sababu hiyo kuonekana kuwa la ajabu.

**6.** *(a) Kuna kufa na kupona, na kuliwa na kingugwa.*

Methali hii inaonyesha hali mbili zinazopingana. Mtu anapougua hupitia wakati mgumu na madhila mengi yanayotokana na ugonjwa ambao anaugua. Kuna magonjwa ambayo hupona baada ya muda mfupi na magonjwa mengine huchukua muda mrefu kabla ya kupona. Mtu akiugua huwa anatarajia mambo matatu, mwanzo mtu anaweza kupona aidha haraka ama baada ya muda mrefu wa kuuguzwa na tabibu. Pili mtu anaweza kuishi na ugonjwa ule hadi kifo. Mara nyingi magonjwa ambayo huletwa na virusi huwa hayaponi. Magonjwa mengine ambayo huadhiri kinga za mwili pia hukosa tiba na hubidi mgonjwa kuyadhibiti kwa kumeza dawa katika maisha yake yote. Tatu kunamagonjwa ambayo huwa yanaathiri mgonjwa kwa kiwango kikubwa baada ya muda mfupi au mrefu, humwelekeza kaburini. Dhana ya kufa na kupona ni dhana mbili ambazo zinapingana na katika maisha ya mwanadamu anaweza kuwa katika hali moja tu kwa wakati wake, hawezi katu kuwa katika zile hali mbili kwa wakati mmoja.

Sehemu hii imejishughulisha na vipengele vya fani vinavyojenga methali teule. Vipengele hivi ni muhimu kwani huwa vinabeba ujumbe maalum katika methali zinazohusika. Katika methali teule za utafiti huu, kipengele cha takriri kinatumika kusisitiza ujumbe katika methali. Msisitizo huu husaidia kukumbukika kwa ujumbe uliosisitizwa. Kipengele cha

tashihisi kinaupa ugonjwa, uuguzi au tiba sifa za kibinadamu uhai ili iwe rahisi kueleweka na mwanajamii na pia husaidia kwa kumpa msikilizaji wa methali teule mvuto wa kusikiliza yanayosemwa. Taswira inasaidia kuchora picha ya ujumbe uliobebwa na methali ili kurahisisha uelewa wa ujumbe wenyewe. Kipengele cha sitiari husaidia kutoa picha fulani katika akili ya wanajamii na ambayo huleta athari fulani ambayo huamsha mwitikio wa ujumbe kwa wanajamii wanaotumia methali hizi teule. Sitiari pia inasaidia kutoa ujumbe ulio na kejeli katika methali hizi kwa njia ambayo inafubwa na iliyo na tasfida. Kinaya kinatumika katika methali hizi teule kukebehi au kukejeli hali ya kutomakinika kwa mtu. Kinaya pia kimetumika kutoa ujumbe ulio kinyume na matarajio katika methali hizi. Kejeli inatumika kuwasilisha ujumbe mzito ulio kwenye methali zinazotafitiwa kwa njia ya kukebehi au kudhihaki na kumfanya mtu afikirie kwa undani ujumbe unaowasilishwa na methali hizi teule.

## 4.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Ujumbe

Lengo hili linaangaziwa kwa kuongozwa na msamiati mkuu katika utafiti huu ambapo tunachambua jinsi ugonjwa huwasilishia ujumbe, jinsi uuguzi huwasilishia ujumbe na hatimaye jinsi tiba huwasilishia ujumbe katika methali teule za Kiswahili.

**Jedwali 4.2: Maudhui ya Methali za Kiswahili Zinazochambuliwa**

| Na | Kipengele cha Maudhui | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1) | Ugonjwa | 66 | 73.3 |
| 2) | Uuguzi | 17 | 18.8 |
| 3) | Tiba | 7 | 7.7 |
| | **Jumla** | **90** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kama inavyodhihirika katika jedwali 4.2 hapo juu, maudhui ya ugonjwa ndiyo yanayochukua asilimia kubwa zaidi (73.3%), yakifuatwa kwa umbali na maudhui ya uuguzi yanayosheheni asilimia 18.8 na hatimaye maudhui ya tiba yanachukua asilimia ya chini kabisa (7.7%). Hii ni bayana kuwa maudhui ya ugonjwa yanayochukua asilimia kubwa yanamiliki methali nyingi zaidi ambazo ni 66 ilhali maudhui ya uuguzi yako na asilimia inayofuata kwa kusheheni methali 17 na hatimaye maudhui ya tiba ndiyo yanayosheheni methali chache zaidi ambazo ni 7 pekee ya jumla ya methali zote zinazofanyiwa utafiti huu.

### 4.2.1 Ugonjwa Kuwasilishia Ujumbe

Jamii ya Waswahili inatumia ugonjwa kuwasilisha ujumbe kwa kuwa ugonjwa huathiri kila mwanajamii wakati fulani maishani mwake. Magonjwa huathiri wanajamii wote bila kubagua kwa mikabala ya kijinsia, kielimu, kijamii, falsafa ya mtu maishani ama hata kiumri. Hii ina maana kuwa kwa kutumia ugonjwa kubeba ujumbe, inakuwa rahisi sana kwa kila mwanajamii kuelewa ujumbe ule kwa urahisi na haraka.

Waterman (2009) akichunguza nyimbo za matambiko ya uponyaji katika jamii ya Watumbuka nchini Malawi, anagundua kuwa waganga wa jamii hiyo hutumia ngoma na uchezaji kama njia mojawapo ya kuuguza na kutibu magojwa tofauti tofauti ambapo mganga hucheza ngoma ili kutuliza mizimu ambayo huleta magonjwa na hatimaye mgonjwa huponywa kupitia nyimbo za matambiko. Mtafiti huyu anaonyesha jinsi nyimbo huwasilisha ujumbe unaoweza kutumiwa kumuuguza mgonjwa.

Haji (2011) anaeleza jinsi mizimu, ambao ni viumbe wa kifikirika, hutumika kuleta uuguzi kwa mgonjwa inapopandishwa kwa kutumia nyimbo za kiganga na mganga ili hiyo mizimu iweze kuongea na yule mganga ili kutoa matibabu.

**Jedwali 4.3: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Ugonjwa**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1) | Kutahadhari kabla ya hatari | 15 | 22.81 |
| 2) | Dhima ya uzazi | 2 | 3.1 |
| 3) | Ugonjwa kama kiashiria cha tatizo | 14 | 21.4 |
| 4) | Matumaini | 8 | 12.3 |
| 5) | Kudhubutu kutenda mambo hatari | 3 | 4.5 |
| 6) | Umuhimu wa uvumilivu maishani | 5 | 7.6 |
| 7) | Utendaji mambo kwa utaratibu | 3 | 4.5 |
| 8) | Utendaji mambo kwa wakati | 5 | 7.6 |
| 9) | Kuhamasisha ushirikiano | 11 | 16.2 |
| | **Jumla** | **66** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kutokana na Jedwali 4.3 hapo juu ujumbe wa kuchukua tahadhari kabla ya hatari unachukua asilimia kubwa ambayo ni 22.81 ukifuatwa kwa karibu na ujumbe ambapo ugonjwa hutumika kama kiashiria cha tatizo katika maisha ya mwanajamii. Ushirikiano ni muhimu katika jamii na ujumbe huu umechukua asilimia 16.2, ukifatwa na ujumbe wa kuwapa watu matumaini maishani. Dhima ya uzazi,umuhimu wa uvumilivu maishani, utendaji mambo kwa utaratibu, kudhubutu kutenda mambo hatari na utendaji mambo kwa wakati ni jumbe zingine ambazo zimesheheni asilimia chini ya kumi kuwasilishia ujumbe kwa kurejelea dhana ya ugonjwa katika methali teule.

Methali zinazosheheni ujumbe kwa kurejelea ugonjwa zinazorodheshwa katika sehemu hii:

1. *Afichaye ugonjwa hazai*
2. *Agunduaye ndwele ndiye mganga*
3. *Baada ya donda msumari moto*

Mount Kenya University

4. *Adhihakiye kovu hajaona jeraha*
5. *Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu*
6. *Dawa si chungu, chungu ni maradhi*
7. *Dawa ya deni ni kulipa*
8. *Donda ndugu laisha dawa*
9. *Hapana uchungu usio tulia*
10. *Iliyopita si ndwele ganga ijayo.*
11. *Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*
12. *Dawa ya hasira ni kicho*
13. *Dawa ya jipu kulipasua*
14. *Dawa ya moto ni moto*
15. *Donda ndugu laisha dawa*
16. *Hapana uchungu usiotulia.*
17. *Hapana jeraha bila silaha*
18. *Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
19. *Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*
20. *Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha*
21. *Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda..*
22. *Jino liumalo hung'olewa*
23. *Kidole kimoja kikiumiachenzake chapwita*
24. *Kipya kinyemi ingawa kidonda.*
25. *Kinga ni bora kuliko tiba.*
26. *Kufanya gaga si kupoa donda.*
27. *Kufanyika gaga sio kupona kwa donda*
28. *Kuna kufa na kupona, na kuliwa na kingugwa*
29. *Kwa mdogo pumu kwa mkubwa mafua*
30. *Mali ya mgonjwa faida ya mfumu.*
31. *Maneno mengi maradhi*
32. *Mapenzi kikohozi hayawezi fichika.*
33. *Maradhi huja shoti yakitoka, ni mtambao wa kinyonga.*
34. *Mficha ndwele hapati dawa*
35. *Mganga hajigangi.*
36. *Mgonjwa haulizwi dawa*
37. *Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda*
38. *Mkimbilia sheria hujiponya.*
39. *Mwenda mbio hujikwaa dole.*
40. *Mtambua ndwele ndiye mganga*
41. *Mwana mui dawa ya mlango.*
42. *Mwenda pole hajikwai.*
43. *Mwenye kovu haliwai na kidonda.*
44. *Mwenye kuficha kidonda,kilio kitamfichua.*
45. *Mwana kidonda,mjukuu kovu*
46. *Mwenye kovu asidhani  kapoa.*
47. *Mwenye matende hana mapaja.*
48. *Mzaha mzaha hutumbuka usaha.*
49. *Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda*
50. *Neno jiwi ni jeraha la moyo.*

Mount Kenya University

*51. Neno ovu ni jeraha la moyo.*
*52. Ngoja ngoja huumiza matumbo*
*53. Buyu kali ni dawa ya mwana mimba.*
*54. Mwenye kovu haliwai na kidonda*
*55. Nzi kufa juu ya kidonda si haramu.*
*56. Pumu zimepata kikohozi*
*57. Shibe ya waganga hutoka kwa wagonjwa.*
*58. Sitafuga ndwele na waganga tele*
*59. Shingo ya kuitikiza sio chungu.*
*60. Si hasara nzi kufa juu ya kidonda*
*61. Ugonjwa ni suna, kufa ni faradhi.*
*62. Ukiona ambari na zinduna ipapo.*
*63. Ukiona zabadi na zinduna i papo*
*64. Ukiwaa uwe na subira.*
*65. Umeingiwa mti.*
*66. Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo.*

Methali hizi teule zinatumia ugonjwa kuwasilisha jumbe mbalimbali kama inavyodhihirika katika sehemu hii.

#### 4.2.1.1 Kutahadhari kabla ya Hatari

Methali hizi teule zinztumia ugonjwa kushadindia ujumbe ambao unaleta dhana ya kuchukua tahadhari kabla ya hatari kutokea.

**7.** *a) Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu*
*b) Baada ya donda msumari moto*
*c) Hapana jeraha bila silaha*
*d) Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*
*e) Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha*
*f) Mwenye kovu haliwai na kidonda*
*g) Kinga ni bora kuliko tiba.*
*h) Kufanya gaga si kupoa donda.*
*i) Kufanyika gaga sio kupona kwa donda*
*j) Mwenda mbio hujikwaa dole*
*k) Mwenda pole hajikwai*
*l) Mwenye kovu asidhani kapoa*
*m) Mzaha mzaha hutumbuka usaha*
*n) Neno jiwi ni jeraha la moyo.*
*o) Neno ovu ni jeraha la moyo*

*p) Ngoja ngoja huumiza matumbo*

Methali hizi zinawasilisha ujumbe kuwa mtu anafaa kuchukua tahadhari kulinda afya yake kabla ya kukumbana na hatari fulani zinazoweza kudhoofisha afya yake. Pia ni vyema kuchukua tahadhari na kungojea mtu apone kabisa kabla ya kuchukua hatua zingine maishani kama vile kufanya kazi ngumu ambazo zinaweza kumfanya arudi katika hali ya kuugua.

#### 4.2.1.2 Dhima ya Uzazi

Methali hizi zinazofuata zinatumia ugonjwa kuwasilisha ujumbe kuonyesha umuhimu au nafasi ya uzazi katika jamii.

**8.** *a) Afichaye ugonjwa hazai*
*b) Buyu kali ni dawa ya mwana mimba*

Methali hizi zinawasilisha ujumbe kuhusu umuhimu wa kutafuta tiba iwapo mtu anashida ya utasa. Hili lina maana kuwa jamii ya Waswahili ilidhamini watoto katika jamii yao. Hili ni kwa kuwa walijua ya kwamba njia moja ya kimsingi ya kuendeleza jamii yao ilikuwa ni kupitia kuzaana. Jamii hii ilidhamini watoto hivi kwamba watoto walionekana kama mali kwa familia. Hili lilipelekea wanamume kuoa wake wengi ili kusaidia kupata watoto wengi katika familia ya mwanamume mmoja. Mwanamke asiyepata watoto alionekana mwenye kasoro na aliyepungukiwa kijamii na mara nyingi alipewa talaka na mumewe na kuonenaka asiyefaa katika jamii. Mwanamke kama huyu ndiye aliyelengwa kwa methali hizi.

Kuna magonjwa ambayo yakimwathiri mtu hupatwa na utasa na hapa inabidi aliyeathirika kumtembelea mganga ili aweze kuaguliwa ili akapate watoto. Matibabu ambayo angepata mara nyingi waganga wangetengeneza dawa kali za miti ya kichakani na huwa ni chungu. Bibi akipata mimba wakati mwingine huwa anapatwa na magonjwa mbalimbali ambayo

yanaweza kuharibu mimba hiyo na hubidi atunzwe vizuri na kwa maakini hadi anapozaa mtoto. Ili kutunza mimba ya mwanamke, ilibidi awe akimtembelea mganga mara kwa mara. Akimtembelea mganga alikuwa akipewa dawa za miti kama mbuyu na mingine ili kulinda mimba hadi apate mtoto ili kuendeleza jamii.

#### 4.2.1.3 Ugonjwa kama Kiashiria cha Tatizo

Methali hizi teule zinatumia ugonjwa kama vile jipu, donda na jeraha kuwasilisha ujumbe wa jinsi ugonjwa unatumika kama kiashiria cha tatizo kwa wanajamii.

**9.** *a) Dawa si chungu, chungu ni maradhi*
*b) Mzaha mzaha hutumbuka usaha*
*c) Dawa ya hasira ni kicho*
*d) Dawa ya jipu kulipasua*
*e) Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda*
*f) Donda ndugu laisha dawa*
*g) Mwana kidonda, mjukuu kovu*
*h) Maneno mengi maradhi*
*i) Mwenye kuficha kidonda, kilio kitamfichua*
*j) Mwenye kovu haliwai na kidonda*
*k) Hapana uchungu usiotulia*
*l) Umeingiwa mti*
*m) Sitafuga ndwele na waganga tele.*
*n) Neno ovu ni jeraha la moyo*

Methali hizi zinatumia ugonjwa kama tatizo ambalo linahitaji kutibiwa ama kuuguzwa. Matatizo haya yaweza kuwa ya kijamii, kiafya, kiuchumi ama hata mahusiano baina ya wanajamii. Katika maisha ya watu na mwingiliano wao, matatizo mbalimbali hutokea na huhitaji utatuzi. Ugonjwa unapomkumba mtu huhitaji kuuguzwa ili mtu arudi katika hali yake ya kawaida. Vivyo hivyo mtu anapokabiriwa na matatizo katika maisha huhitaji kuyatatua ili maisha yake yaweze kuendelea.

#### 4.2.1.4 Matumaini

Mount Kenya University

Sio kila wakati katika maisha ya mwanadamu maisha huwa shwari, kuna nyakati zingine mambo huenda mrama na mtu huhitaji kutiwa moyo na kupewa matumaini ya kuendelea na maisha. Methali zinazofuata zinatumia ugonjwa kama njia bora ya kumpa mwanajamii anayekufa moyo kutekeleza jambo fulani, kumpa tumaini la kuendeleza maisha yake.

**10.** *a) Aendaye kwa mganga hakosi jambo*
*b) Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo*
*c) Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*
*d) Dawa ya jipu kulipasua*
*e) Hapana uchungu usiotulia*
*f) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
*g) Mkimbilia sheria hujiponya*
*h) Ukiwaa uwe na subira*

Wakati mwingine kiza kikubwa hukumba maisha ya mwanadamu na kushindwa na la kufanya. Hili ni kutokana na shida ama majanga anayopiti kama vile madeni, shida za kifamilia, magonjwa ama shida za kikazi. Maisha huwa kama bembea, mara iko juu na wakati mwingine huwa chini. Nyakati za misukosuko ya maisha mtu huhitaji kupewa matumaini ya kuwa siku za usoni sitakuwa nzuri. Methali hizi zinabeba ujumbe wa matumaini kwa mwanajamii. Japo maisha huwa na panda shuka nyingi, ni vizuri kuwa na matumaini ya kuwa mambo yatarudi katika hali ya kawaida.

#### 4.2.1.5 Kudhubutu Kutenda Mambo Hatari

Woga huwa kama adhabu. Mtu anapoongozwa na woga hawezi kutekeleza mambo mengi katika maisha yake. Yafaa mtu kujituma kwa bidii kutekeleza anayoweza bila hofu. Methali hizi zinatumia ugonjwa kuwasilisha ujumbe wa kuwahimiza wanajamii kufanya jambo lolote lile bila woga kama linamfaidi au kufaidi wanajamii.

**11.** *a) Nzi kufa juu ya kidonda si haramu*
*b) Si hasara nzi kufa juu ya kidonda*
*c) Jino liumalo hung'olewa*

Mount Kenya University

Ugonjwa unatumika kuonyesha kuwa ni vyema mwanajamii kufanya jambo ambalo litamfaidi yeye hata kama wakati mwingine litahatarisha afya yake au hata maisha yake. Kama hilo jambo linamfaidi au kufaidi jamii kwa jumla ni vyema kulitekeleza. Nzi ni mdudu mdogo anayeruka kwa mbawa zake na hupenda uchafu. Huruka kutoka sehemu moja chafu hadi nyingine akitafuta chakula. Nzi hupenda kula usaha utokao kidondani. Ingawa kuna hatari ya nzi kufia kidondani anapotafuta chakula chake yeye hujikakamua na hufuata mtu kila aendapo kama anacho kidonda kwa hapo kidondani ndipo chakula chake kipo.

#### 4.2.1.6 Umuhimu wa Uvumilivu Maishani

Katika maisha, mtu hupitia mema na mambaya, mengine kutoka kwa maadui na mengine kutoka kwa asiotarajia kama marafiki au watu wa familia. Methali hizi zinasheheni ujumbe wa umuhimu wa uvumilivu katika maisha kwa kusawiri ugonjwa.

**12.** *a) Ukiwaa uwe na subira*
*b) Agunduaye ndwele ndiye mganga*
*c) Yaliyyopita si ndwele, ganga yajayo.*
*d) Hapana uchungu usio tulia*
*e) Iliyopita si ndwele ganga ijayo*

Ugonjwa unapompata mwanajamii hubidi apitie hali ngumu ya kutojiweza na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kibinafsi na ya kikazi na kijamii. Kabla apone na kurejelea hali ya kawaida huhitaji avumilie kwa muda fulani. Methali hizi zinahimiza uvumilivu wa anayaugua hadi atakapopona.

Mount Kenya University

#### 4.2.1.7 Utendaji Mambo kwa Utaratibu

Magonjwa mengine humpata mtu kutokana na kutokuwa mwangalifu katika maisha yake. Ili kutimiza malengo yake ya kiafya, mtu anahitaji kuwa mwangalifu na kufanya mambo kwa uangalifu kama vile methali hizi vinavyotoa ujumbe wa utaratibu katika kufanya mambo kwa kusawiri ugonjwa.

**13.** *a) Mwenda mbio hujikwaa dole*
*b) Mwenda pole hajikwai*
*c) Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*

Kutembea kwa uangalifu na kwa maakini kunaweza kumuokoa mtu kutokana na madhila ya uchungu wa mwili na hisia, kuuguza jeraha na kuokoa muda wake pia. Ni shufaa mtu atembee polepole achukue muda mwingi kufika, kuliko kwenda mbio ilhali mtu ajikwae akose kufika alipokuwa anaenda kutokana na jeraha la kujikwaa.

#### 4.2.1.8 Utendaji Mambo kwa Wakati

Methali hizi teule zinasawiri ugonjwa kuwasilisha ujumbe wa kuhimiza watu kufanya mambo wanayofaa kufanywa kwa wakati wake au wakati ufaao.

**14.** *a) Ngoja ngoja huumiza matumbo.*
*b) Jino liumalo hung'olewa.*
*c) Mgonjwa haulizwi dawa*
*d) Mzaha mzaha hutimbuka usaha.*
*e) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini.*

Magonjwa humwadhiri mtu kwa kutochukuwa jukumu la kulinda afya kwa njia zinazofaa na wakati ufaao. Kwa kuchelewa kuchukua hatua ya kulinda afya yake wakati ufaao mtu anaweza kukumbwa na athari kubwa ya kiafya. Mtu anapougua anahitaji kumwona mganga mara moja ili kuuguzwa na kupata nafuu.

Mount Kenya University

#### 4.2.1.9 Kuhamasisha Ushirikiano

Hivi kwamba umoja na ushirikiano ni jambo la muhimu katika jamii, ugonjwa unatumika kuwasilisha ujumbe wa hamasisho la ushirikiano kwa wanajamii. Methali zifuatazo zinadhihirisha haya.

**15.** *a) Kidole kimoja kikiumia chenzake cha pwita.*
*b) Dawa ya jipu kulipasua.*
*c) Dawa ya moto ni moto.*
*d) Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda.*
*e) Mwana mui, dawa ya mlango*
*f) Mwana kidonda mjukuu kovu*
*g) Mwenye matende hana mapaja.*
*h) Mwenye kovu haliwai na kidonda*
*i) Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa.*
*j) Ukiona ambari na zinduna i papo.*
*k) Ukiona zabadi na zinduna i papo.*

Ugonjwa unatumika kuashiria ushirikiano ambao huletwa na ugonjwa. Ili mtu apate nafuu huhitaji ushirikiano wa karibu kati yake na muuguzi na kufuata maagizo anayopewa na yule muuguzi. Pia kuna magonjwa mengine ambayo huwa yanashikamana na mengine na yanapoambukiza mtu huwa yanamwathiri mtu kwa wakati mmoja.

### 4.2.2 Uuguzi Kuwasilishia Ujumbe

Baadhi ya methali katika uchunguzi huu zinabeba maudhui ya uuguzi, ambao unatumika kuwasilisha ujumbe fulani kwa jamii kama vile ushirikiano, kuonya dhidi ya ulafi na tamaa, kutahadharisha na kuwapa wanajamii matumaini. Methali hizi ni;

**Jedwali 4.4: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Uuguzi**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1) | Matumaini | 6 | 35.3 |

Mount Kenya University

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2) | Kuuguza ni tendo la utu | 1 | 5.9 |
| 3) | Kuuguza ni kutamauka | 3 | 17.6 |
| 4) | Tahadhari | 1 | 5.9 |
| 5) | Subira | 1 | 5.9 |
| 6) | Uuguzi ni kikoa | 2 | 11.8 |
| 7) | Umuhimu wa ujuzi katika jamii | 3 | 17.6 |
| | **Jumla** | **17** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kutokana na jedwali 4.4 hapo juu, ujumbe wa matumaini unachukua asilimia 35.3 ukifuatwa na ujumbe wa utamaushi na umuhimu wa ujuzi katika jamii, kila ujumbe ukiwa na ailimia 17.6 huku uuguzi kama kikoa ukiwa na asilimia 11.8. Jumbe zingine ambazo ni kuuguza kama tendo la utu, kuchukua hadhari na kuwa na subra maishani zinachukua asilimia 5.9 kila kipengele kuwasilisha ujumbe kwa kurejelea dhana ya uuguzi katika methali teule.

Methali zinazosheheni ujumbe unaowasilishwa kwa dhana ya uuguzi ni;

1. *Aendaye kwa mganga hakosi jambo*
2. *Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo.*
3. *Sitafuga magonjwa na waganga tele*
4. *Usipouguza mwele una koo la ujuko.*
5. *Agunduaye ndwele ndiye mganga*
6. *Chendacho kwa mganga hakirudi*
7. *Donda ndugu laisha dawa*
8. *Sikio la kufa halisikii dawa*
9. *Wanja ya manga si dawa ya chongo*
10. *Ukiwaa uwe na subira.*
11. *Ukiona ambari na zinduna i papo*
12. *Ukiona zabadi na ziduna i papo*
13. *Agunduaye ndwele ndiye mganga.*
14. *Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
15. *Mtambua ndwele ndiye mganga*
16. *Hapana uchungu usio tulia*
17. *Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*

Waterman (2009) akichunguza nyimbo za matambiko ya uponyaji katika jamii ya Watumbuka nchini Malawi, anagundua kuwa waganga wa jamii hiyo hutumia ngoma na uchezaji kama njia mojawapo ya kuuguza na kutibu magojwa tofauti tofauti ambapo mganga hucheza ngoma ili kutuliza mizimu ambayo huleta magonjwa na hatimaye mgonjwa huponywa kupitia nyimbo za matambiko. Mtafiti huyu anaonyesha jinsi nyimbo huwasilisha ujumbe unaoweza kutumiwa kumuuguza mgonjwa.

Katika utafiti huu kama vile nyimbo huwasilisha ujumbe fulani maalumu kwa wauguzi katika jamii ya Watumbuka nchini Malawi, methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumika kuwasilisha ujumbe unaosawiri uuguzi kama vile; ujumbe wa matumaini, kuwa hata baada ya mtu kuugua kuna matumaini kwamba aliyeugua atapata nafuu, ujumbe kwa kutamausha, ya kwamba sio lazima aliyeuugua akienda kwa mganga apate nafuu, ujumbe wa kutahadharisha, subira mtu anapougua, ujumbe wa umoja na ushirikiano.

**4.2.2.1 Matumaini**

Ujumbe wa matumaini unaobebwa na methali hizi teule unasawiri uuguzi wa ugonjwa.

**16.** *a) Aendaye kwa mganga hakosi jambo*
*b) Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo*
*c) Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*
*d) Hapana uchungu usiotulia*
*e) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
*f) Iliyopita si ndwele ganga ijayo*

Methali hizi zinabeba ujumbe wa matumaini kwa mwanajamii. Japo maisha huwa na panda shuka ni vizuri kuwa na matumaini ya kuwa mambo yatarudi katika hali ya kawaida.

Katika methali 17(a) mtu anapougua humlazimu kutafuta mganga ili aweze kutatuliwa shida ya ugonjwa uliomwathiri. Hii ina maana kuwa hakuna aendaye kwa mganga pasipo na haja.

Mgonjwa huwa na imani kuwa akienda kwa mganga ugonjwa alionao utapata kuuguzwa au kutibiwa. Magonjwa huathiri afya ya mtu, kimwili, kisaikolojia, familia, uhusiano na watu wengine, kikazi na pia kiuchumi. Mambo haya yanaweza kumwacha mtu katika hali mbaya asijue la kufanya. Ili mtu aweze kuendelea na maisha kama hapo mbeleni, humbidi mtu kusahau madhara yaliyoletwa na magonjwa na kufurahia hali yake ya afya ili aweze kuendelea mbele na yale anahitaji kufanya ili kuendeleza maisha yake. Huwa ni rahisi kuugua lakini vigumu kurejelea hali ya kiafya. Magonjwa humsumbua anayeugua na kumlazimu kuacha shughuli zake za kila siku na kwanza kujilaza kitandani hadi anapopata nafuu. Katika hali yake ya kuugua, mgonjwa huwa na matumaini ya kurejelea afya yake njema anapomtembelea muuguzi au mganga ili aweze kutibiwa na kupona.

Methali 17(b c, d na e) pia zinaleta ujumbe wa matumaini kwa aliyepitia hali ngumu haswa ya kiafya kuwa mtu akipona hafai kukwama kwa ugonjwa ulio mwathiri mbali yafaa asahau na kutazama mbele na kutumainia mazuri ya siku zijazo. Pia mtu akiugua yafaa afuatilie maagizo ya mganga hadi asikose matumaini atakapopona.

#### 4.2.2.1 Kuuguza ni Tendo la Utu

Methali ifuatayo inasawiri uuguzi kuwasilisha ujumbe wa dhima ya kumtunza mwanajamii mwenzako auguapo kwani leo itakuwa ni yeye na kesho ni wewe.

**17.** *a)Usipouguza mwele una koo la ujuko.*

Mtu anapougua huwa hajiwezi na hutegemea msaada wa waliokaribu na yeye hadi anapopata nafuu. Katika jamii kuna shughuli nyingi ambazo kila mwajamii hufanya ili kujikimu kimaisha na kuna shughuli za kijamii ambazo kila mwanajamii anafaa kujukumikia kila siku. Ili mtu aweze kuwa wa msaada kwa mgonjwa hubidi aache shughuli zake za kila siku ili

kumuuguza mgonjwa. Wanajamii wengine wanaweza kuona hiyo ikiwa kazi nyingi na washindwa kutoa ule msaada na hapo ndio mtu huonekana akiwa amepotoka kimaadili kulingana na maadili na kaida za jamii na anaweza akakosa wa kumsaidia yeye anapohitaji msaada.

#### 4.2.2.2 Kuuguza ni Kutamauka

Methali hizi zinatumia uuguzi kusawiri jinsi uuguzi wakati mwingine hukatisha tamaa ya kutafuta matibabu hata kama mtu anaugua.

**18.** *a) Chendacho kwa mganga hakirudi*
*b) Donda ndugu laisha dawa*
*c) Sikio la kufa halisikii dawa*

Mgonjwa anaougua huhitaji kumtembelea mganga ili akatibiwe. Ili kupata huduma za mganga, mgonjwa huhitaji kwenda na zawadi ya mganga ili amtunuku ama malipo ya huduma anayopokea. Zawadi inaweza kuwa kubwa ua ndogo. Lililo la kweli ni kuwa mgonjwa akipokea uuguzi na kumpatia mganga zawadi yake au malipo, apone asipone, ile zawadi aliyotoa kwa mganga haiwezi kumrudia yule mgonjwa.

Magonjwa huwa ya aina nyingi na kuna yale ambayo hupona kwa haraka, mengine huuka kwa muda mrefu kabla ya kupona na mengine hayaponi kamwe. Kidondo kinapoenea sehemu kubwa mwilini huitwa donda. Madonda haya husababishwa na magonjwa hatari kama vile ya kisukari au saratani na huwa hayaponi. Madonda haya hata ya kiuguzwa vipi huwa hayana tiba, lake tu ni kumaliza dawa tu. Methali hii inawasilisha ujumbe wa kukatisha tamaa hivi kwamba magonjwa mengine hayana tiba hata mtu ayauuguze kwa muda mrefu, bado yanabaki kumsumbua.

#### 4.2.2.3 Tahadhari

Uuguzi katika methali hii unatumika kuwasilisha ujumbe wa tahadhari kwa wanajamii ya kwamba kuna mambo au hali fulani ambazo zikimwathiri haziwezi kubadilishwa.

**19.** *a)Wanja ya manga si dawa ya chongo*

Kuna magonjwa ambayo humuadhiri mtu na yanaweza kutibiwa hata baada ya kuuguzwa kwa muda mrefu au mfupi. Kuna mengine ambayo hutokana na maumbile au mengine yakisha ingia mwilini kutibiwa huwa haiwezekani. Ujumbe wa methali hii ni kutahadahrisha kuwa yale yasiyoweza kutibiwa, anayeuuguwa akubali hali aliyonayo.

### 4.2.2.4 Subira

Uuguzi unasawiri ujumbe wa subira katika methali hii;

**20.** *a)Ukiwaa uwe na subira.*

Huwa ni rahisi sana kuugua au ugonjwa kuingia mwilini lakini huwa ni vigumu sana kupata nafuu mtu anapouugua. Kurejelea hali yake ya afya tena huhitaji uvumilivu wa kutosha kabla mtu apone. Huhitaji kumuona mganga kila mara kwa kipindi fulani, kunywa dawa chungu na kudungwa sindano na maumivu ya mwili kila wakati. Hapa ndio mtu huhitajika kuwa na subira ya kutosha bila kukata tamaa.

### 4.2.2.5 Uuguzi ni Kikoa

Uuguzi unatumika kuwasilisha ujumbe wa ushirikiano na umoja katika jamii. Hakuna mtu anayeweza kuishi peke yake bila kutegemea wengine kwani leo itakuwa ni kwangu na keshoye ni kwako. Maisha ni kutegemeana, mmoja kuwa kijalizo cha mwingine.

**21.** *a) Ukiona ambari na zinduna i papo*
*b) Ukiona zabadi na ziduna i papo*

Mount Kenya University

Mtu akiugua huhitaji kuuguzwa na mganga ili aweze kupona. Mganga huwa na dawa ambazo hutumia ili kumuuguza aliye uugua. Dawa hizi huwa za aina tofauti na huhitaji kumpa mgonjwa dawa hizi tofauti ili apate tiba. Kuna zile dawa huwa ni lazima ziambatane au kuchanganywa ili ziweze kumponya anaye ugua. Vilevile kuna magonjwa ambayo mara nyingi huambatana yanapomwathiri mtu. Kwa mfano ugonjwa wa kisukari huambatana na msukumo wa damu na kuna uwezekano mwingi mtu anapougua kisukari hatakosa ugonjwa wa msukumo wa damu.

#### 4.2.2.6 Umuhimu wa Ujuzi katika Jamii

Methali hizi teule zinatoa ujumbe wa umuhimu wa ujuzi katika jamii kwa kusawiri uuguzi. Ujuzi wa kufanya mambo mbalimbali katika jamii ni muhimu na walio na ujuzi huu husaidia kutatua changamoto zinazowakumba wanajamii.

**22.** *a) Agunduaye ndwele ndiye mganga.*
*b) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
*c) Mtambua ndwele ndiye mganga*

Ili kutekeleza jambo lolote katika jamii, huhitaji mtu au watu walio na ujuzi wa kulifanya jambo lile. Watu katika jamii wanapougua huenda kwa waganga kwa kuwa wanaamini kuwa waganga wana ujuzi tosha wa kuwauguza ili wapate tiba. Kwa kuwa waganga ndio walio kuwa na ujuzi wa kutibu, walisifika sana na kujulikana kote katika jamii na wagonjwa walikuwa wakielekezwa kwa walioonekana kuwa na ujuzi wa hali ya juu wa kuuguza wagonjwa. Aliyeugua na kuchelewa kwenda kumuona mganga ama akakosa matumaini ya kupona, basi angesemewa methali hizi ili apate mshawasha wa kwenda kumuona mganga na kuganguliwa ili apate tiba.

### 4.2.3 Tiba Kuwasilishia Ujumbe

Kuna methali ambazo zinatumia tiba kuwasilisha ujumbe fulani katika methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Methali zifuatazo zinasheheni ujumbe unaosawiri tiba katika methali teule.

**Jedwali 4.5: Ujumbe Uwasilishwao kwa Dhana ya Tiba**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1) | Tiba ni suluhisho | 4 | 57 |
| 2) | Tiba ni hali fulani | 3 | 43 |
| | **Jumla** | **7** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kutokana na jedwali 4.5 hapo juu inabainika wazi kuwa asilimia 57 ya methali zinawasilisha ujumbe uletao suluhu kwa kurejelea dhana ya tiba na asilimia 43 inasheheni methali zinazowasilisha ujumbe unaolenga hali fulani kwa kusawiri tiba. Methali zinazosheheni ujumbe kwa kusawiri tiba ni:

1. *Dawa ya deni ni kulipa*
2. *Jino la pembe si dawa ya pengo*
3. *Sahau ni dawa ya waja*
4. *Mkimbilia sheria hujiponya.*
5. *Pembe si dawa ya kuku*
6. *Mganga hajigangi*
7. *Maradhi huja shoti yakitoka ni mtambao wa nyoka*

#### 4.2.3.1 Tiba ni Suluhisho

Dawa kama inavyotumika kuponya magonjwa mbalimbali inatumika katika methali zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba kuleta ujumbe wa suluhisho katika maisha ya mwanadamu. Mwanadamu hukubwa na matatizo mbalimbali na kwa hivyo huhitaji utatuzi wa matatizo hayo.

**23.** *a) Dawa ya deni ni kulipa.*
*b) Mkimbilia sheria hujiponya*
*c) Pembe si dawa ya kuku*
*d) Jino la pembe si dawa ya pengo*

Neno dawa katika 24(a, c na d) linatumika katika methali hizi kuwasilisha ujumbe wa kupata suluhisho la jambo fulani katika jamii.

Mtu akiwa na deni huhitaji kuilipa kama walivyoagana na aliyempa deni kwa kuwa bila kulipa lile deni litabaki pale. Kuna wale ambao hupewa deni na baadaye kutoa ahadi za uongo ya kuwa watalipa. Kila kuchao wao hujificha ili wasipatikane, japo watajificha kwa muda upi hatimaye huwabidi kulipa lile deni kwani kujificha sio suluhu ya deni. Kwa hivyo tiba au suluhisho la deni ni kuilipa deni yenyewe. Katika hali ya kawaida ya maisha, hakuna mtu katika jamii anayeweza kusema anajitosheleza kwa kila kitu au jambo. Huhitaji msaada wa mtu au watu wengine ili kutatua shida inayoweza kuwa inamkumba, na hapo ndipo anaweza kujipata katika hali ya deni au madeni. Lile deni mtu anaweza kuwa nalo linafananishwa na ugonjwa. Kama vile ugonjwa humwandama mtu hadi anapouuguzwa na kupona, vivyo hivyo ndivyo deni humfuata aliye na deni hadi anapolilipa lile deni. Kama mtu amepewa deni huhitaji kulipa lile deni ili liishe. Kule kulipa lile deni ndiko kunakofananishwa na dawa kwani mwenye deni anapolipa deni huuguza anayemdai na kujiuguza mwenyewe kutokana na kudaiwa kulipa deni lile taz. 24(a).

Sheria ni kanuni ambazo hutoa mwongozo jinsi mambo yanavyofaa kufanywa na zikikiukwa mhusika huadhibiwa.Sheria inafananishwa na tiba. Katika maisha ya mwanadamu kila

sehemu ya maisha yake huongozwa na sheria zilizoandikwa ama kaida katika jamii. Sheria hizi ndizo huwa zinaweka mipaka katika shughuli zake na anayezikiuka sheria hizi hujipata katika hali tatanishi na hubidi azifuate sheria zilizowekwa. Anayefuata sheria kila wakati yeye huwa hana shaka kwani hujua sheria itamuokoa na mashaka yanayompata. Sheria huwa kama tiba kwa anayezifuata taz 24(b).

Katika 24(c), kuku ni ndege ambaye hufugwa nyumbani kutokana na faida zake kwa binadamu kama vile kutaga maya, akichinjwa ni nyama, manyoya yake hutumiwa kama marebesho na pia kinyesi chake hutumiwa kama mbolea. Kuku anatumika kuwasilisha ujumbe unaosawiri tiba. Kuku huwa hana pembe na kwa hivyo kile asichokuwa nacho na ambacho hawezi kuwa nacho hakiwezi kumsaidia hata wakati anapohitaji kuuguzwa. Kuku na vifaranga wake huwa na adui yake mkuu, mwewe, kutoka jadi kama vile hadithi za fasihi simulizi hueleza. Uadui huu, kwa kuku na vifaranga wake, huwa kama ugonjwa ambao siku zote hauishi ila humfuata wakati wowote kila mahali. Kuku huwa hana pembe ambazo zinaweza kumkinga kutokana na uvamizi wa mwewe hata hivyo kwa kuwa mwewe humvamia ghafla na hutoka juu angani hata kama kuku angekuwa na pembe, zile pembe hazingemkinga kutokana na uvamizi wa mwewe. Kuna magonjwa ambayo hayana kinga hivi kwanba hata mtu akitia bidii kwa njia gani bado yanampata. Ujumbe wa methali hii unampa mtu kuvumilia wakati anathirika na ugonjwa ambao hawezi kupona.

Meno ni viungo vidogo vya mwili amabvyo ni vya muhimu sana katika misha ya mwanadamu. Meno husaidia katika kutafuna chakula ikiwa ndio kazi yake ya kimsingi. Meno pia hutumika kama pambo katika uso wa mtu, mpangilio wake unaopendeza huvutia mtu anapocheka ama anapoongea. Rangi yake nyeupe pia huwa pambo tosha kwa mtu. Vile vile meno hutumika kumpa mtu sura ya kupendeza kwani wasio kuwa na meno hata wakiwa

wachanga huonekana wakiwa na uso ulioregea na hata kupatwa na makunyanzi. Hata hivyo, mara nyingi, kadiri mtu anavyozeeka hukabiriwa na maradhi tofauti tofauti. Mojawepo ya maradhi haya huadhiri meno au ufizi. Ugonjwa unapoadhiri jino huwa na uchungu mwingi sana na kwa hivyo hubidi mtu atafute msaada kwa muuguzi ili kupata ushauri au kuuguzwa ili apate tiba. Ugonjwa wa kuumwa na meno hulazimu mtu kung'olewa jino au meno na kubakia na pengo au mapengo Baada kubaki katika ile hali ya pengo au mapengo, bado umuhimu wa meno hubaki ili aweze kutafuna chakula au kudumisha urembo. Ili kukidhi hitaji lile huwa kuna meno ambayo ni bandia ambayo huuzwa na waganga kuziba pengo au mapengo yaliyoachwa na meno yaliyong'olewa. Hata akiwekwa meno bandia kama vile ya pembe, dhahabu au la mfupa haliwezi kuwa kama aliloliumba Mungu.

#### 4.2.3.2 Tiba ni Hali Fulani

Kama vile maradhi hutokana na hali mbalimbali nayo tiba hutokana na hali tofauti tofauti kama vile katika methali hizi hali fulani zinatumika kuwasilisha ujumbe unaosawiri tiba.

**24.** *a) Sahau ni dawa ya wanja*
*b) Mganga hajigangi*
*c) Maradhi huja shoti yakitoka ni mtambao wa nyoka*

Hali ya kusahau inatumika kuashiria tiba katika maisha ya mwanadamu katika 25 (a). Kuna mambo ambayo humkumba mwanadamu lakini kadri muda unavyoyoyoyoma mja huyasahau hata kama yalikuwa na athari hasi katika maisha yake. Kuhasau huku ndiko huwa tiba ya roho au katika maisha yake. Mtu anapofanya jambo huwa analifanya kwa kusudio/nia njema au kusudio mbaya. Mtu anaweza kuwa na nia nzuri anapolifanya jambo lakini matokea ya lile jambo analotenda yakawa mambaya kuliko tumainio lake. Kama yule mja anafanya jambo kwa nia njema hata likiharibika huwa ni rahisi kumwelewa.

Hakuna mja anayeweza kujitosheleza kwa kila kitu maishani. Methali hii 25 (b) inatoa ujumbe wa hali ya kutegemeana kwa wanajamii katika maisha kwa kusawiri tiba. Maishani mwa watu hakuna anayeweza kuishi katika upweke au katika ombwe, katika hali moja, wakati mmoja au mwingine hutegemea mwenzake ili kukamilisha shughuli zake. Mgonjwa anapougua huhitaji msaada wa waliokaribu naye ama huhitaji msaada wa mganga ili aweze kuuguzwa au kutibiwa Vilevile kuna wakati mwingine ambapo mganga huugua na huhitaji kutibiwa. Anapougua hawezi kujiuguza mwenyewe na hubidi kumuona mganga mwingine ili amtibu.

Katika 25(c), mtu anapougua hujipata katika hali ambayo hajiwezi kwa lolote au chochote na huhitaji msaada wa mtu mwingine ili aweze kufanya shughuli zake zote.Wakati mwingine, pasipo kutarajia, mtu hujipata anaugua na kulemewa kabisa hivi kwamba hata kutembea au kula kwake huwa ni mzigo. Wakati mwingine magonjwa huwa yanamdhuru mtu polepole bila hata mtu kujua kuna magonjwa yanayomwandama ama hata wakati mwingine mtu huwa anaelewa kuna ugonjwa unao mwadama lakini anachelewa kutafuta uuguzi. Kuna magonjwa kama vile kisukari na saratani ambayo humwathiri mtu polepole bila hata kugundua kuna ugonjwa unaomwadhiri, hatimaye ndio mtu hugundua kuwa ugonjwa unaomwathiri mtu huwezi kuponywa ama kama utauguzwa itakuwa safari ndefu sana na inaweza kosa kuzaa matunda ya kuuguzwa na kupona. Safari ya kumuuguza anayeuguua na kupata tiba huwa ni ngumu, yenye majonzi kwa mgonjwa na kwa walio karibu naye na huwa sfari refu vile vile. Inaweza kuchukua siku, miezi au hata miaka kabla mtu apate tiba. Kule kuchukua muda kabla ya kuugua ndiko kunakofananishwa na mwendo wa kinyonga ambaye kwa maumbile yake mwendo wake huwa wa polepole sana.

Katika uchunguzi wake kuhusu usawiri wa mhusika wa kiume katika methali za Kimeru, Raymond (2016) anabainisha jinsi mwanaume anavyochorwa na kuchukuliwa katika jamii ya Wameru. Kwa kuwa jamii ya Wameru imeegemea upande wa kuumeni, methali nyingi anazochambua zinamtaja mwanamume kwa kumpa hadhi ya juu alinganishwapo na mwanamke. Mwamaume anasawiriwa kama kiumbe aliye wa maana zaidi kuliko mwanamke katika asasi mbalimbali za kijamii. Katika ndoa, mwanamume anasawiriwa kama kiongozi katika jamii yake na ndiye anayetawala mambo na shughuli zote katika familia, mwanamke kazi yake kuu ni ya kuzaa na kufanya yale anayoambiwa na mumewe. Katika utawala mwanamume ndiye mtawala na mwanamake mtawaliwa. Mwanamke analazimishwa kupashwa tohara hata kama tohara yenyewe inamletea madhara ya kiafya katika mwili wake anapojifungua. Mwanamke hapati nafasi sawa na mwanamume ya kufanya kazi. Kuna zile kazi zinatengewa wanawake na zile maalum za wanamume.

Kazii hii ya Raymond, inamsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu katika jamii ya wameru na mwanamme kama kiumbe wa muhimu zaidi kuliko mwanamke. Kazi hii inasaidia katika kujenga utafiti wetu katika kuchunguza usawiri wa ugonjwa uuguzi na tiba ili kwasilisha ujumbe unaosheheniwa na methaliteule zinazochunguzwa.

### 4.3 Athari za Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba katika Ufasiri wa Ujumbe

Hali hizi tatu ambazo ni ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumika kufasiri ujumbe unaolenga jamii kwa njia mbalimbali zinazoleta athari tofauti tofauti kwa wanajamii. Kuna athari chanya na athari hasi. Ingawa kuna athari hasi, athari chanya zinachukua asilimia kubwa ya athari kulingana na utafiti wetu. Athari chanya ni kama vile uhusiano wa karibu unaojengwa na methali hizi, watu kuhimizwa kuwa waangalifu, mambo yafaa kufanywa kwa utaratibu, uwajibikaji, ustahamilivu, kujenga matumaini wakati wa hali ngumu na mapenzi kati ya

wapendanao. Baadhi methali teule zinabeba ujumbe ulio na athari hasi ni kama vile utamaushi, kiwewe na makovu yasiyosahaulika nayayoachwa na ugonjwa, ubaguzi na unyanyapaa kwa wenye magonjwa fulani katika jamii, usiri usio na faida, hasara na hadaa ya vitu vipya.

### 4.3.1 Athari za Matumizi ya Ugonjwa kwa Ufasiri wa Ujumbe

Methali teule za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba husheheni jumbe totautitofauti zinapofasiriwa. Katika sehemu hii uchunguzi unaohusiana na athari zinazotokana na usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika kufasiri ujumbe unafanywa. Ugonjwa unatumika kuwasilisha ujumbe maalum katika jamii ya Waswahili. Ugonjwa unatumika kwani ni hali ambayo humkumba mwanajamii yeyote na kwa hivyo ujumbe unawafikia wanajamii wengi na kuweza kutafsiri ujumbe unaobebwa na methali zinazohusika kwa wepesi na haraka.

Katika methali teule zinazosawiri ugonjwa kufasiri ujumbe zinaleta athari chanya na hasi kwa wanajamii. Baadhi ya athari chanya zinazosheheni ujumbe unaosawiri ugonjwa ni; mambo yanafaa kufanywa kwa utaratibu maalumu, ni afadhali kuchukua tahadhari au kuwa na uangalifu kwa yale tunayofanya, kukuza uhusiano wa karibu, ni vizuri kufanya maamuzi ya haraka kwa uangalifu, kukuza ustahamilivu na faida ya msaada kwa wanaouhitaji. Vilevile kuna athari hasi chache zinazotokana na methali hizi ambazo ni; hadaa itokanayo na vitu vipya, hasara inayoweza kutokana na maamuzi ya haraka, ubaguzi na unyanyapaa unaotokana na baadhi ya magonjwa katika jamii na makovu ambayo huachwa daima maishani mwa watu.

Mount Kenya University

**Jedwali 4.6: Athari za Matumizi ya Ugonjwa Kusawiria Ujumbe**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| (1) | Utaratibu katika utendaji Mambo | 3 | 4.5 |
| (2) | Tahadhari na Umakinifu Maishani | 15 | 22.8 |
| (3) | Jihadhari na usemacho | 5 | 7.6 |
| (4) | Mahusiano ya karibu | 13 | 19.6 |
| (5) | Maamuzi ya haraka | 6 | 9.1 |
| (6) | Ukuzaji wa ustahamilivu | 6 | 9.1 |
| (7) | Ukarimu na msaada kwa wahitaji | 6 | 9.1 |
| (8) | Hadaa ya vitu vipya | 3 | 4.5 |
| (9) | Hali ya kukurupuka | 4 | 6.1 |
| (10) | Ubaguzi na Unyanyapaa | 5 | 7.6 |
| | **Jumla** | **66** | **100** |

**Chanzo : Data Uwandani, 2023**

Kutokana na Jedwali 4.6 inadhihirika kuwa ujumbe wenye tahadhari na umakinifu katika maisha ndio unaochukua asilimia kubwa kwa kurejelea methali teule ambayo ni 22.8 . Hili ni kutokana na sababu kuwa wanajamii hukumbwa na hatari nyingi maishani mwao na kwa hivyo, yamfaa kuchukua hadhari bila kupuuza. Ujumbe unaochochea utangamano na uhusiano wa karibu katika jamii unachukua nafasi ya pili kwa asilimia 19.6 katika methali zinazochunguzwa. Jumbe za maamuzi ya haraka, ukuzaji wa kustahamili na ukarimu na msaada kwa wahitaji znafuata kwa asilimia 9.1 kwa kila ujumbe. Ubaguzi na unyanyapaa, kujihadhari na mtu asemacho kila wakati zinashaheni asilimia 7.6 kwa kila ujumbe. Hatimaye, hadaa ya vitu vipya na utartibu katika kutenda mambo ni jumbe zilizo na asilimia iliyo chini 4.5, katika methali teule. Asilimia kubwa ya jumbe hizi zinaleta athari chanya

Mount Kenya University

kama vile utaratibu wakati wa kutenda mambo, faida ya kutahadhari na kuwa maakini katika maisha, faida ya mahusiano ya karibu, ukuzaji wa ustahamilivu. Jumbe zilizo na athari hasi ni hadaa ya vitu vipya, hila ya kukurupuka na ubaguzi na unyanyapaa.

#### 4.3.1.1 Utaratibu katika Utendaji wa Mambo

Binadamu hukumbwa na mambo tofauti na huhitajika kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja au kwa muda mfupi alionao. Ili yote yaweze kutimia hubidi yafanywe kwa utaratibu maalum.

**25.** *a) Mwenda pole hajikwai*
*b) Ugonjwa ni suna, kufa ni faradhi*
*c) Mwenda mbio hujikwaa dole.*

Methali hizi zinadhihirisha umuhimu wa utaratibu na uangalifu mkubwa kwa yale tunayoyafanya yasije yakawa ndio chanzo cha magonjwa yanayotuathiri. Mtu anapotembea kwa haraka huwa hana nafasi nzuri ya kuangalia anapokanyanga na kwa hivyo anaweza kukanyanga kitu kinachoweza kumuumiza au akajikwaa kidole au sehemu nyingine ya mwili. Utaratibu unaweza kumuokoa mtu kutokana na kujikwaa ambao ni ugonjwa unaoweza kumgharimu mtu muda na pesa za kumuuguza au kumtibu.

#### 4.3.1.2 Hadhari na Umakinifu Maishani

Ni vyema kuwa mwangalifu kwa mtu ambaye amekuwa katika hali mbaya ya athari za ugonjwa kwa kuwa mwonekano wake unaweza ashiria kama amepona lakini athari za ugonjwa ule ziwe zinamwathiri bado.

**26.** *a) Mwenye kovu asidhani kapoa*
*b) Maneno mengi maradhi*
*c) Baada ya donda msumari moto*
*d) Mwenda pole hajikwai*
*e) Neno jiwi ni jeraha la moyo*

*f) Shingo ya kuitikiza sio chungu*
*g) Dawa ya hasira ni kicho*
*h) Kufanya gaga si kupoa donda.*
*i) Kufanyika gaga sio kupona kwa donda*
*j) Neno ovu ni jeraha la moyo*
*k) Ngoja ngoja huumiza matumbo*
*l) Donda ndugu laisha dawa*
*m) Sitafuga ndwele na waganga tele*
*n) Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu*
*o) Mwenda mbio hujikwaa dole*

Ni vizuri kuchukua tahadhari kabla ya hatari. Mtu anapougua huwa anachukua muda mwingi kabla ya kupata nafuu na kabla ya kurudi katika hali yake ya kiafya. Mtu kama huyu huhitaji awe mwangalifu katika mienendo yake, afanyacho na anachokula ili aweze kudumisha afya yake, asije akadanganyika anapopata nafuu kidogo na kudhani ameshapona kabisa . Asipokuwa mwangalifu anaweza kujipata amerudi katika hali yake mbaya kiafya na kubaki akijutia kutochukua tahadhari.

Maneno maovu yanaposemwa yanaweza kuumiza moyo wa anayeambiwa na kuishi kama jereha moyoni mwake. Kwa hivyo ni vyema chukuchuwa tahadari kabla ya kusema lolote. Magonjwa mengine hayawezi kupona hata yakiuguzwa kwa muda mrefu, magonjwa kama haya humbidi aliyeathirika kukubali hali hiyo na kutafuta njia za kuyauguza tu.

**4.3.1.3 Jihadhari na Usemacho**

Mdomo hutumiwa kuongea na wakati mwingine mtu asipojihadhari anaweza sema maneno ya kuwakwaza wengine na kubaki akijutia maneno yake.

**27.** *a) Maneno mengi maradhi*
*b) Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha*
*c) Mapenzi kikohozi hayawezi fichika*
*d) Neno jiwi ni jeraha la moyo*
*e) Neno ovu ni jeraha la moyo*

Mount Kenya University

Katika mtagusano wa wanajamii wa kila siku katika maisha, watu hupatana na kuongea mambo mengi ya muhimu, kula soga ama hata kutaniana. Mipaka ya maongezi ya watu hutawalia na mambo kama vile hadhi ya mtu katika jamii, umri, hali ya mtu, uhusiano wa watu, jinsi na mada inayozungumziwa. Kwa kuzingatia haya ni muhimu kutilia maanani mzungumzo na maneno anayotumia mtu ili asije akamkwaza mwenzake kwa maneno yasiyofaa. Kama vile mwili unaweza umizwa pia maneno maovu yanaweza kuumiza moyo wa mtu na kuishi na lile jeraha milele. Kwa hivyo ni vizuri mtu kujihadhari na asemayo yasije yakawa kidonda moyoni mwa mtu mwingine.

#### 4.3.1.4 Mahusiano ya Karibu

Uhusiano kati ya watu, hali au vitu hujengwa kutokana na hali ya kujitakia au ya kulazimishwa na hali fulani kama ilivyo kati ya mgonjwa na kitanda.

**28.** *a) Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda*
*b) Kidole kimoja kikiumia chenzake chapwita*
*c) Kuna kufa na kupona, na kuliwa na kingugwa*
*d) Hapana jeraha bila silaha*
*e) Mwenye kovu haliwai na kidonda*
*f) Mwana kidonda,mjukuu kovu*
*g) Dawa ya deni ni kulipa*
*h) Mwenye matende hana mapaja*
*i) Pumu zimepata kikohozi*
*j) Ukiona ambari na zinduna ipapo.*
*k) Ukiona zabadi na zinduna i papo*
*l) Dawa ya jipu kulipasua*
*m) Dawa ya moto ni moto*

Mtu anapougua huwa hajiwezi na wakati mwingine huwa hata hajielewi wala kujitambua na ifikapo hapa hubidi kulazwa kitandani. Anayeugua hulazimika kubaki pale kitandani kila wakati usiku na mchana hadi wakati anapopata nafuu. Methali hii inaonyesha uhusiano wa

karibu mno ambao huletwa na ugonjwa kati ya mgonjwa na kitanda au mahali ambapo mgonjwa hujilaza au kulazwa auguapo.

Uhusiano huu unaweza kuwa kwa hiari ambapo mtu hujilaza kitandani kama ugonjwa unaomuathiri haujaathiri afya yake kwa kiwango kikuu. Wakati mwingine uhusiano huu huwa ni wa lazima kwani wakati mgonjwa huwa amelemewa na kutojiweza hulazwa pale kitandani pasi hiari yake na hapo ndipo hulazimika kukaa na basi wakati ule uhusiano wake na kitanda kuwa wa lazima kwa kipindi fulani hadi anapopata nafuu. Kula, kunywa na hata kwenda haja ndogo na kubwa huwa pale pale kitandani.

### 4.3.1.5 Maamuzi ya Haraka

Maamuzi ambayo huchukuliwa na mgonjwa ama anayemsaidia anapougua husaidia kuokoa maisha ya mgonjwa kama vile methali hii inadhihirisha.

**29.** *a) Mgonjwa haulizwi dawa.*
*b) Sitafuga ndwele na waganga tele*
*c) Ngoja ngoja huumiza matumbo*
*d) Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*
*f) Jino liumalo hung'olewa*
*g) Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*

Mtu anapougua huhitaji kumuona mganga ili aweze kuuguzwa na kupata tiba ya ugonjwa unaomwathiri. Mara nyingi mtu akiwa na mtu mgonjwa huhitaji kukata shauri na kumtafutia matibabu anayeugua. Wanamume mara nyingi wanahusishwa na kasumba ya kutotembelea hospitali ili wauguuzwe wanapougua. Mara nyingi wao huvumilia hata wakati mtu amelemewa na ugonjwa kiasi kwamba hata kutoka kwa kitanda kwenda msalani pekee ni shida na yeye akiulizwa anasema hana shida kubwa atapona. Wakati kama huo ndio walio karibu naye huona kuwa hamna haja tena kuvumilia na mara moja humtafutia uuguzi au tiba kwa waganga hata bila idhini yake ili kuokoa maisha yake.

Mount Kenya University

Vile vile mtu yeyote yule anapougua huhitaji kukata shauri ya kwenda kumuona muuguzi au kutafuta matibabu ili apate kuuguzwa. Jambo hili ni la maana kwani huweza kuokoa maisha ya mtu. Wale ambao huugua na kukosa kukata shauri au huchelewa kukata shauri ya kwenda kuuguzwa wanaweza kujipata katika hali mbaya zaidi kiafya ama hata wakati mwingine kupoteza maisha yao.

Kukata shauri ni jambo la maana zaidi kwakuwa linaweza kumuokolea mtu pesa nyingi na pia muda mwingi unaotumika kumuuguza mtu. Hili linaweza kutokana na kauli kuwa mtu anapokata kauli kwenda kumuona muuguzi wakati ugonjwa hujaenea kote mwili na kumdhoofisha kiafya, hutumia muda mfupi hospitalini ama kitandani anapolazwa na pia hutumii pesa nyingi kuuguza ugonjwa alionao.

**4.3.1.6 Ukuzaji wa Ustahamilivu**

Methali hizi teule zinatoa ujumbe wa kustahimili wakati mtu anapougua.

**30.** *a) Dawa si chungu, chungu ni maradhi*
*b) Dawa inayowasha inakupenda*
*c) Iliyopita si ndwele ganga ijayo*
*d) Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo*
*e) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
*f) Hapana uchungu usiotulia.*

Mtu anapougua huhitaji kumuoana muuguzi au mganga ili apewe matibabu. Mgonjwa huhitaji kumeza dawa kwa kipindi fulani ili aweze kupona kutokana na maradhi anayougua. Kwa kawaida, dawa hutengenezwa kutokana na kemikali ambazo huwa ni chungu zinapotiwa kinywani ili kuzimeza. Pia mgonjwa humbidi kustahamili kudungwa sindano wakati mwingine kwa muda mrefu ili aweza kupona. Methali hii inasisitiza umuhimu wa kustahimili uchungu wa dawa. Ambaye huchukulia dawa ni chungu na hataki kuzitumia basi hubaki na uchungu wa ugonjwa unaomwathiri hadi anapokubali kuzitumia dawa.

#### 4.3.1.7 Ukarimu na Msaada kwa Wahitaji

Msaada wowote huwa wa muhimu sana mtu anapougua kama vile methali hizi inavyashiria.

**31.** *a) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini*
*b) Jino liumalo hung'olewa*
*c) Agunduaye ndwele ndiye mganga*
*d) Mganga hajigangi.*
*e) Mtambua ndwele ndiye mganga*
*f) Buyu kali ni dawa ya mwana mimba*

Ni dhahiri shahiri kwamba mtu anapougua huwa hajiwezi kwa lolote, kutembea huwa ni vigumu na hata kula humuwia ngumu. Hii ina maana kuwa mgojwa huhitaji msaada kwa kila jambo afanyalo. Humbidi mtu akiugua kurudi nyumbani kwa jamii yake ama anapoita nyumbani na kutulia pale akitarajia kupata msaada kutoka kwa walio karibu naye.

Msaada huu unaotolewa na walio karibu na yeye ndio unaoweza kuwa tegemeo la mwisho katika maisha ya anayeugua. Ndio aweza kusaidiwa au kupata msaada wa jamii yake hubidi kuwe na uhusiano mwema kati yake na jamii yake. Wakati mwingine anayeugua huhitaji msaada zaidi ya anaopokea kutoka kwa jamaa wake wa karibu. Magonjwa mengine huhitaji msaada wa damu kama vile wakati wa upasuaji wa sehemu nyeti au za muhimu mwilini kama vile moyo, figo na ubongo. Bali na msaada wa damu, pia huhitaji msaada wa kifedha na kimawazo. Hili linategemea uhusiano wa ukaribu unaofanya wanajamii waungane pamoja na kumsaidia aliye na hitaji la kiafya na msaada wa tiba.

Msaada pia wa muuguzi ni muhimu kwani bila kuuguza na kumpa tiba anaye uguua, juhudi zote za wanajamii zaweza kuwa za bure. Muuguzi anahitajika na ujuzi alionao wa kuuguza na kutibu ambao ni wa muhimu zaidi mgonjwa anapouugua.

#### 4.3.1.8 Hadaa ya Vitu Vipya

Moyo wa mtu huvutika kwa urahisi kwa vitu vipya na kwa hivyo ni rahisi kujipata katika mtego au hali isiyoridhisha kama ugonjwa.

**32.** *a) Kipya kinyemi ingawa kidonda*
*b) Si hasara nzi kufa juu ya kidonda*
*c) Nzi kufa juu ya kidonda si haramu.*

Katika hali ya kawaida ya mtu, vitu vilivyo vipya machoni pake hupendeza kuliko vile vya zamani ama alivyozoea kuviona. Mtu anaweza kubeza vya zamani akiviona kama havifai ila viwe ndivyo vya msaada zaidi kuliko vile vipya. Neno kidonda ambao ni ugonjwa, linatumika kuashiria kitu kisichochadhamani lakini chaweza kupendeza. Nzi anapokiona kidonda hufurahia kwa usaha utokao kidondani huwa chakula chake pasipokujua kuwa anaweza patana na kifo chake pale kidondani.

#### 4.3.1.9 Hali ya Kukurupuka

Kuna faida kubwa ya kutekelaza mambo wakati unaofaa ili kujikinga na athari mbaya za kuchelewa. Methali hizi zinaashiria faida ya kinga kwa ugonjwa inapotolewa wakati unaofaa.

**33.** *a) Ituuzayo tia hiyo, isiyokuwako sio dawa*
*b) Sitafuga ndwele na waganga tele*
*c) Afichaye ugonjwa hazai*
*d) Kuzuia ni bora kuliko kuponya*

Mtu anapougua mara nyingi huwa haendi kumuona mganga mara moja ila kwanza huchukua muda kuona kana kwamba atapata nafuu akiwa nyumbani. Pia maradhi mengine huwa hayana ukali mwingi mwanzoni mtu anapougua na kwa hivyo watu wengi huchelewa kumwona muuguzi. Kuchelewa pia kunaweza kutokana na hali aliyo mtu kiuchumi hivi kwamba hana hela za kugharamia malipo ya muuguzi na kwa hivyo anachukuwa muda kabla ya kupata fedha.

Mount Kenya University

Mtu anapochelea kwenda kuuguzwa, ugonjwa bado huwa mwilini na unaweza kuwa ukienea na kuathiri viungo vingine vya mwili na hatimaye ikawa vigumu kuutibu ule ugonjwa. Kwa hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kwenda kumuona muuguzi pindi tu mtu anaugua bila kuchelewa kwa kuwa kuchelewa kunaweza kukamleteama madhara zaidi.

#### 4.3.1.10 Ubaguzi na Unyanyapaa

Methali hizi zinadhihirisha ubaguzi na unyanyapaa kati ya watu wazima na watoto kulingana na majina yanayopewa ugonjwa fulani hata kama ugonjwa yenyewe ni wa aina moja.

**34.** *a) Kwa mdogo pumu kwa mkubwa mafua*
*b) Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha*
*c) Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi*
*d) Mwana mui dawa ya mlango*
*e) Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda*

Kuna magonjwa ambayo huwapata watoto na vilevile watu wazima. Katika methali hii inatoa taswira ya ubaguzi uliopo baina ya magonjwa ya watoto na yale ya watu wazima. Licha ya kuwa aina ya ugonjwa ni moja lakini unapewa majina tofauti kwa kurejelea umri wa mwathiriwa. Hili hufanyika ili kutumia jina ambalo linaonenaka ni la heshima kwa watu wazima na kwa hivyo kubagua watoto kwa kutumia jina ambalo halionyeshi heshima kwa watoto.

Ubaguzi huu hutokea hata katika uuguzi wa magonjwa haya. Watu wazima wanaweza kupokea uuguzi wa hali ya juu katika hospitali za kifahari ilhali watoto wanaweza kujipata wakifatutiwa uuguzi katika hospitali za kawaida tu zilizo za kiwango cha chini.

Pia walio na hela katika jamii wanapouugua hupata uuguzi wa hali ya juu katika hospitali za kiwango cha juu na wale ambao ni maskini hulazimika kusalia nyumbani, kutafuta dawa za miti shamba ambazo huonekana duni na za kiwango cha chini au huwalazimu kutafuta tiba

katika hospitali za kawaida na ambazo huonekana kuwa za kiwango cha chini katika jamii na mara nyingi huwa zina hudumu duni ama kukosa hudumu zingine kabisa.

### 4.3.2 Athari za Matumizi ya Uuguzi kwa Ufasiri wa Ujumbe

Matumizi ya methali teule kusawiri uuguzi katika kufasiri ujumbe yana athari chanya ya kujenga matumaini, uwajibikaji na athari mbili hasi ambazo ni utamaushi na kiwewe au makovu yasiyosahaulika yanayoachwa na ugonjwa baada ya mtu kuuguzwa.

Baadhi ya methali katika uchunguzi huu zinatumika kuufikisha ujumbe fulani kwa jamii unaosawiri uuguzi kwa mfano, kuleta matumaini kwa mwanajamii anayeweza kuwa akipitia kipindi kigumu cha maisha, uwajibikaji katika jamii, hali ya kutamauka, ushirikiano na umoja katika jamii.

**Jedwali 4.7: Athari za Matumizi ya Uuguzi kwa Ufasiri wa Ujumbe**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| (1) | Ukuzaji wa matumaini | 7 | 41.2 |
| (2) | Uwajibikaji | 2 | 11.7 |
| (3) | Utamaushi | 4 | 23.5 |
| (4) | Ushirikiano na umoja | 3 | 17.6 |
| (5) | Kiwewe na makovu yasiyosahaulika | 1 | 6 |
| | **Jumla** | **17** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kutokana na jedwali 4.7 inadhihirika kuwa ujumbe wa ukuzaji wa matumaini katika jamii unabeba asilimia 41.2 katika methali teule. Asilimia 23.5 ni ujumbe wa utamaushi, 17.6

ujumbe wa ushirikiano na umoja katika jamii, 11.7 ni ujumbe wa uwajibikaji na hatimaye asilimia 6 imesheheni methali moja yenye ujumbe wa kiwewe na makovu yasiyosahaulika yatokanayo na ugonjwa

#### 4.3.2.1 Ukuzaji wa Matumaini

Baadhi ya methali zinatoa ujumbe ambao ni chanya unaleta athari ya kutoa matumaini pale ambapo mgonjwa anaweza kuwa na ugonjwa fulani unaomsubua kwa muda mrefu na pengine akakosa matumaini ya kutafuta uuguzi tena ama akakosa matumaini ya kupona.

**35.** *a) Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini.*
*b) Hapana uchungu usiotulia*
*c) Iliyopita si ndwele ganga yajayo.*
*d) Ukiwaa uwe na subira*
*e) Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo.*
*f) Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa*
*g) Mtambua ndwele ndiye mganga*

Methali hizi zinaonyesha matumaini ambayo mgonjwa huwa nayo anapomtembelea mganga wakati anapougua. Hii ni kwa kuwa mgonjwa huwa na imani na tumaini kuwa kutokana na ganga ganga za mganga hali yake ya kiafya inayodhoofika na kumwacha katika hali asiyojiweza itabadilika kwa zile juhudi za mganga na kuwa mzima tena. Vile vile methali hizi zinatoa ujumbe wa matumaini kwa aliye ugua maradhi fulani. Kwa kawaida mtu anapougua hupitia wakati mgumu kwa kuwa magonjwa mara nyingi huandamana na maumivu katika mwili. Maumivu haya hutegemea aina ya ugonjwa na sehemu inayoadhirika au sehemu zinazoadhirika. Ili mgonjwa apate tulizo kutokana na maumivu hubidi kumuona muuguzi ili aweze kutibiwa. Anapotibiwa uchungu na maumivu yanayotokana na ugonjwa alionao hatimaye hutulia. Methali hizi ni mfano mwema wa kumpa aliye na uchungu unaotokana na ugonjwa wa kumpa tumaini ya kwamba atapata nafuu.

Mount Kenya University

Methali hizi vile vile zinatoa ujumbe ulio na matumaini kwa kurejelea ugonjwa. Mtu anapougua huhitaji kuchukua muda fulani kabla apone, aidha unaweza kuwa muda mrefu ama ukawa muda mfupi. Anayeugua huhitaji kumtembelea muuguzi mara kwa mara ili aweze kuuguzwa ama kukaa karibu na muuguzi ili aweze kuangalia hali ya afya yake inavyoendelea kila wakati. Hali hii humhitaji anayeugua kukaa akikumbuka hali yake na ugonjwa unaomtatiza. Hata baadaya ya kupata nafuu na kupona, aliyeugua hukumbuka hali aliyokumbana nayo alipokuwa ameugua. Hali hiyo inaweza kumlemaza kufanya mambo mengine muhimu katika maisha ama akaogopa kufanya mambo mengine ambayo yanaweza kumweka katika hali ngumu aliyokuwa nayo ya kuugua. Kwa hivyo kila wakati yeye huchukuwa tahadhari asijipate katika hali kama ile tena. Wakati kama huu mtu kama yule ndipo hupewa tumaini katika maisha ama katika hali fulani ambayo humbidi asahau madhila aliyopitia katika ugonjwa aliokuwa nao na kuweza kuendelea mbele na maisha.

#### 4.3.2.2 Uwajibikaji

Mtu hupata magonjwa kwa njia tofauti kama vile ajali, kuambukizwa pasipokujua ama kutochukua tahadhari wakati wa hatari ya mlipiko wa ugonjwa fulani. Methali hizi zinaashiria mchango wa mtu kupata ugonjwa.

**36.** *a) Agunduaye ndwele ndiye mganga*
*b) Aendaye kwa mganga hakosi jambo*

Kulingana na ujumbe wa methali hizi ina maana kuwa sio magonjwa yote ambayo humpata mwanajamii pasipo yeye kuchangia. Kuna yale magonjwa ambayo mtu hawezi jikinga na kuna yale ambayo hutokana na utepetevu wa mtu binafsi. Magonjwa kama vile malaria, kisukari, kiharusi hutokana na mtu kutokuwa mwangalifu pahali anapokaa, kile anachokula ama kunywa. Ili mtu ajikinge na ugonjwa wa malaria anahitaji kununua neti na kulala ndani

yake ili asiumwe na mbu. Ugonjwa wa kisukari unatokana na hali ya maisha ya mtu anavyoishi hususan anachokula, ndivyo ajikinge noa anahitaji kuwa mwangalifu wa kile anachokula. Ugonjwa wa Ukimwi huambukizwa kwa watu wengi kwa kutotumia kinga wakati wa kujamiiana, kama mtu anaweza kuwa mwangalifu na kutumia mipira ya kinga hawezi ambukizwa kwa urahisi. Hivyo basi kama mtu angekuwa mwangalifu magonjwa kama haya hayangemuathiri. Methali hizi zinasisitiza kuwa ni jukumu la kila mwanajamii kujukumika ili kuhifadhi afya yake kwa kuwa mwangalifu kwa kile alacho na afanyacho.

**4.3.2.3 Utamaushi**

Methali hizi zinabeba ujumbe unaoleta athari inayoashiria kutamauka kwa kurejelea uuguzi.

**37.** *a) Chendacho kwa mganga hakirudi*
*b) Donda ndugu laisha dawa*
*c) Sikio la kufa halisikii dawa*
*d) Wanja ya manga si dawa ya chongo*

Mtu anapougua huwa na matumaini makubwa ya kuwa akimuona muuguzi atapata kuuguzwa na kupata tiba ya ugonjwa unaomwathiri. Ni jambo la kuatua moyo baada ya mtu kufanya juhudi za kutafuta tiba na kulipia gharama hatimaye anakosa kupona ugonjwa unaomwathiri. Vilivile sio magojwa yote ambayo hupona, kuna magonjwa ambayo hata mtu akitia bidii kwa njia gani magonjwa yale huwa hayaponi bali mtu huishi katika hali ile maishani mwake.

**4.3.2.4 Ushirikiano na Umoja**

Athari zingine zinazotokana na magonjwa mengineo huleta dhana ya ushirikiano na umoja katika jamii.

**38.** *a) Usipouguza mwele una koo la ujuko.*
*b) Ukiona ambari na zinduna i papo*
*c) Ukiona zabadi na ziduna i papo*

Methali hizi zinaashiria ushirikiano na umoja katika jamii kwa kutumia tiba katika methali teule. Mtu anapougua huhitaji msaada kwa dharura ili kuokoa maisha yake. Mtu aliyekaribu hata kama sio ya jamii ya anayeugua huhitajika na kaida za jamii kumsaidia muwele. Mtu asipomsaidia aliyeugua anaweza kutengwa na jamii na wakati wake ufikapo na pengine ahitaji msaada wa wanajamii, kutokana na hulka yake ya kutosaidia wengine, pia naye hatasaidiwa na wengine.

Magonjwa mengine yanapomwathiri mtu huwa yanaandamana na kuyatenganisha huwa ni vigumu hivi kwamba mtu hufahamu kuwa anapougua ugonjwa fulani baada ya muda fulana, ataandamwa na ugonjwa mwingine pia. Ugonjwa na kisukari mara nyingi huandama na ugonjwa wa msukumo wa damu.

#### 4.3.2.5 Kiwewe nu Makovu Yasiyosahaulika

Athari zingine zinazotokana na magonjwa mengine zinaweza kubaki katika maisha ya mtu daima kama inavyodhihirisha methali hii.

**39.** *a) Adhihakiye kovu hajaona jeraha.*

Mtu anapougua ugonjwa fulani hupitia wakati mgumu na magonjwa mengine huacha ishara zisizoisha au kusahaulika milele katika mwili wa binadamu maishani mwake. Ishara hizi huwa ni ukumbusho wa ugonjwa ule kila wakati. Ishara hizi huwa na athari mbalimbali katika maisha ya mgonjwa na wakati mwingine katika maisha ya walio karibu na yeye ama hata kuathiri jamii nzima kwa ujumla. Aliye uugua anaweza kuadhirika kiafya na asipate kurudia hali yake ya kawaida tena. Kuna magonjwa ambayo huwa hayaponi mtu anapougua kama vile saratani, ugonjwa wa kisukari, Ukimwi na usonji huachia anayeugua ishara za

kiafya zisizofutika daima. Kuna ajali zingine ambazo mtu anaweza pata maishani na kuathiri viungo vya mwili na kumuachia ishara zisizosahaulika maishani kama vile kukatwa viongo vya mwili kama mguu, mkono, kutolewa figo moja, kupoteza uwezo wa kuona ama kupoteza uwezo wa kusikia.

Magonjwa kama haya huathiri maisha ya mgonjwa moja kwa moja na hubidi mgonjwa kuachwa na ishara hizi zisizosahaulika na kujifunza kuishi na ishara hizi hata kama hazipendezi. Ishara hizi huathiri maisha ya mwathiriwa kwani hawezi kufanya kazi zake kama ilivyo kuwa hapo mbeleni na huhitaji msaada wa mtu au watu wengi au hata kutumia mkongojo au kiti cha magurudumu.

Jeraha lile huathiri hata familia yake kwa njia moja au ingine haswa kama ndiye aliyekuwa tegemeo lao kiuchumi kwani hawezi kujimudu yeye mweyewe wala jamaa yake wa karibu. Jamaa yake inaishi kuliona lile jeraha linaloletwa na ugonjwa anaougua yule mtu. Jamii kwa ujumla inaweza kuathirika kutokana na jeraha la mtu kwa kuwa pengine alikuwa kiongozi katika jamii, alikuwa anafanya kazi muhimu katika jamii kama vile mwalimu, daktari au mhubiri au hata mwanabiashara mashuhuri. Yale aliyokuwa anatendea jamii hataweza kuyatenda tena kutokana na athari ya ugonjwa uliomwathiri.

### 4.3.3 Athari za Matumizi ya Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe

Methali teule za kiswahili zinatumika kusheheni ujumbe unaosawiri tiba kama vile majuto, mapenzi kutahadharisha, sio magonjwa yote hupona kama vile utafiti huu unavyothibitisha.

Matumizi ya tiba kufasiri ujumbe katika methali teule za Kiswahili inaleta athari chanya za mapenzi, unyumbukaji, uwezo wa kimaarifa ya kibinadamu, na athari hasi ya utamaushi katika jamii.

**Jedwali 4.8: Athari za Matumizi ya Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe**

| Na | Ujumbe | Mdafao (fx) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| (1) | Mapenzi ya dhati | 2 | 22.2 |
| (2) | Unyumbuaji au mnepo maishani | 1 | 11.1 |
| (3) | Uwezo na maarifa ya kibinadamu | 2 | 22.2 |
| (4) | Utamaushi | 4 | 44.5 |
| | **Jumla** | **9** | **100** |

**Chanzo: Data Uwandani, 2023**

Kutokana na jedwali 4.8 inabainika kuwa ujumbe wa utamaushi unachukua asilimia kubwa, 44.5, ukifuatwa wa ujumbe wa mapenzi ya dhati na uwezo wa maarifa ya kibinadamu kwa asilimia 22.2 kila kipengele na hatimaye ujumbe wa mnepo maishani unabeba asilimia 11.1 ya methali zote teule katika sehemu hii.

### 4.3.3.1 Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni zile hisia nzuri na za ukweli ambazo huibuka moyoni mwa mtu kuhusu mtu au kitu fulani. Mapenzi yanatumika kama tiba la moyo wakati mtu anapatwa na changamoto za maisha.

**40.** *a) Kipendacho roho ni dawa*
*b) Penzi la moyo ni dawa*

Neno dawa linatumiwa kuonyesha tiba kwa roho au moyo wa mtu ambaye anakabiliwa na hali ya mtanziko wa kuchagua kati ya mambo mawili au zaidi. Ili mtu aweze kujinasua kwa hali hii inayomkanganya hufuata hisia za ndani ya moyo wake. Hili huwa ni penzi la moyo wake na ndio huwa tiba pia. Sio changamoto za kiafya zinazoweza kutatuliwa kwa matumizi ya dawa, kunazile shinda ambazo mtu akifuata mapenzi ya roho yake, afya yake huimalika.

Mount Kenya University

Mtu anaweza kuuguwa na kupatwa na msongo wa mawazo kutokana na mapenzi yake na mtu ampendaye iwapo atakataliwa, lakini anapokubalika na kupewa penzi afya yake ya kiakili inaimalika na hata kupona.

**4.3.3.2 Unyumbukaji au Mnepo Maishani**

Mnepo au unyumbukaji ni uthabiti mtu anaofaa kuwa nao katika maisha. Mtu anaweza kubwa na hali ngumu za maisha ambazo hustahili uthabiti wa kiwango cha juu ili waweze kufaulu. Hali hii ya mnepo huwa haiji katika maisha ya mtu mara moja mbali huwa ni safari ya muda mrefu ambayo hujenga pole pole kupitia mapito tofauti tofauti yaliyo na changamoto kama za maradhi.

**41.** *a) Maradhi huja shoti yakitoka ni mtambao wa nyoka*

Magonjwa mengine yanapomwathiri mtu, huhitaji kuuguzwa kwa muda mrefu ili yapone. Magonjwa mengine athari zake hasi huthibitiwa kwa matumizi ya madawa kwani hayawezi kupona kwa mfano saratani, Ukimwi na kisukari. Mgonjwa anayeugua magonjwa haya huhitaji uvumilivu wa kiwango cha juu na kukubali hali yake ili asije akapatwa na msongo wa akili anapokabiliana na magonjwa kama yale.

**4.3.3.3 Uwezo na Maarifa ya Kibinadamu**

Mganga huwa na ujuzi na kwa uwezo wake wa kugangua magonjwa na huwa anawatamalaki wagonjwa katika hali zao hoi. Hata hivyo ujuzi wake wakati mwingine hugonga mwamba kama vile hizi methali zinavyoashiria.

**42.** *a) Tabibu hakingi ajali*
*b) Uzee hauna dawa.*

Mount Kenya University

Mganga huwa na uwezo wa hali ya juu na tajriba kuu ya kuuguza wagonjwa. Kutokana na dalili fulani za ugonjwa, anauwezo wa kufahamu ugonjwa anaougua mtu na hatimaye kumtibu mgonjwa. Kuna magonjwa ambayo huwa yanazidi uwezo wake na kumwacha mgonjwa katika hali ya tahadhari hivi kwamba anaweza kupoteza maisha yake. Vilevile mtu anapozeeka hali ile ya uzee haiwezi badilika hata mtu akiamue anywe dawa zozote.

**4.3.3.4 Utamaushi**

Mtu anapougua awe na fedha ama asiwe nazo huhitaji kugharamia matibabu. Methali hizi zinaubeba ujumbe unaoashiria hasara iletwayo na ugonjwa.

**43.** *a) Sikio la kufa haliskii dawa.*
*b) Donda ndugu laisha dawa*
*c) Kutaataa sio dawa ya kufa.*
*d) Kiendacho kwa mganga hakina marejeo*

Mtu anapougua hubidi atafute huduma ya uuguzi kutoka kwa mganga. Ili kupata huduma hii kutoka kwa mganga, mgonjwa humbidi aende na malipo. Malipo haya huwa ndio faida ya kazi afanyayo ya kuuguza na kutibu wagonjwa. Ujuzi huu mganga alionao wa kuuguza ndio huwa shibe yake. Mgonjwa anapo uguzwa na pengine akose kupata nafuu ama kwa bahati mbaya afe, malipo yale aliyotoa kwa mganga hayawezi kurudishwa. Malipo haya yanaweza kuwa ghali mno na pengine hubidi mgonjwa amtembelee mganga kwa muda mrefu kulingana na maradhi ya mgonjwa. Sio lazima aliyeugua kuwa na mali na hubidi wanajamii kumchangia ili aweze kupatiwa tiba. Hali hii ya kutoa mali kwa mganga yaweza kumuacha mgonjwa katika hali duni kiuchumi.

Kuna aina nyingine za magonjwa ambazo humuuathiri mtu katika maisha yake yote. Magonjwa mengine huwapata watoto wadogo kwa kiwango kikubwa, mengine huwapata vijana na magonjwa mengine huwapata wazee na kuna magonjwa mengine ambayo

hayabagui. Kulingana na sayansi kuna magonjwa yale ambayo husababishwa na bakteria na mengine virusi na mengine mashetani au mizimu kulingana na imani na itikadi za Waswahili.

Methali hizi zinadhihirisha ukweli kuwa japo mtu huugua na kwenda kumuona mganga ili aweze kuuguzwa au kutibiwa sio lazima apate nafuu na kuna uwezekano ya mgonjwa kutopona. Kuna yale magonjwa ambayo huwa ni rahisi kutibiwa mtu anapougua kama vile malaria, homa na kiharusi ilhali kuna yale ambayo mtu akiugua hapati tiba na hubidi kuishi katika hali ile katika maisha yake hadi kufa.

Mtu anapougua na kukosa kupata matibabu au ikiwa kwamba ugonjwa alio ugua hawezi kupona, huwa anahangaika huku na kule kabla ya kukata roho. Ata akihangaika aje kama wakati wake wa kufa kutokana na athari ya ugonjwa fulani umefika hana budi kukata roho. Sito (2015) akichunguza athari zinazotokana na mazingira katika uteuzi wa msamiati, anaonyesha jinsi mazingira huathiri matumizi ya msamiati. Anaonyesha jinsi miktadha ya kijamii na mazingira ilivyo muhimu katika uchambuzi na ufasiri wa maana na ujumbe unaowasilishwa na methali zinazohusika. Katika uchunguzi huu wa Sito unasaidia kuweka msingi dhabiti tunapochanganua athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe.

Katika utafiti huu ugonjwa unatumika kuwasilisha ujumbe maalum katika jamii ya Waswahili. Ugonjwa unatumika kwani ni hali ambayo humkumba mwanajamii yeyote na kwa hivyo ujumbe unawafikia wanajamii wengi na kuweza kutafsiri ujumbe uliobebwa na methali zinazohusika kwa urahisi. Baadhi ya jumbe ambazo zinatokana na athari ya usawiri wa ugonjwa katika methali zinazochunguzwa ni kufanya mambo kwa utararibu ni muhimu, uhusiano wa ukaribu unaoletwa na ugonjwa, usawiri wa kukata shauri ni athari nyingine inajitokeza katika matumizi ya ugonjwa,usiri mtu anapougua, ugonjwa vilevile unatumiwa

kuleta athari ya usawiri wa ustahamilivu katika maisha ya mwanajamii, ugonjwa pia unatumika kuleta athari katika usawiri wa kuleta ubaguzi katika maisha ya wanajamii, ugonjwa kuleta athari ua usawiri wa kuacha ishara ambazo haziwezi kusahaulika katika maisha ya anayeugua.

Asha na Fatma (2012) ambao wanatazama athari zinazoletwa na uchawi katika jamii ya Wazanzibari ili kutoa tiba inayoweza kuuguza magonjwa yanayosababishwa na uchawi wanagundua kuwa, mgonjwa anahitaji kufanyiwa matambiko na mganga ili mizimu inayosababisha magojwa iweze kutolewa katika mwili wa mgonjwa na basi akapata nafuu. Kazii hii haijafaidi utafiti huu kwani watafiti hawa waliangazia athari za uchawi katika jamii ilhali utafiti wetu unajikita katika kuchunguza methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Ali (2016) katika Jarida la *Africa studies Review* akitoa maelezo kuhusu nyimbo za uganga za Wazigua na Wazaramo, anaeleza umuhimu wa nyimbo katika matambiko na uganga wa jamii hizi na jinsi wagonjwa wanapopewa huduma za uuguzi na tiba huhitajika kurudia maneno ya nyimbo mbalimbali ziibwazo na muuguzi. Utafiti huu haukufaidi utafiti wetu kwani mtafiti huyu alichunguza uhusiano uliopo kati ya nyimbo na matambiko na uganga wa jamii za Wazigua na Wazaramo ilhali utafiti wetu naejikita katika kuchunguza methali teule za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Anapochambua jamii ya Waswahili na itikadi zilizo katika jamii hiyo, Sengo (2011) anaeleza kuwa uganga wa kale ni taasisi iliyo hai katika maisha yao. Anasema kuwa wawele huweza kuimbiwa nyimbo kama sehemu ya tiba ili wapone. Kazi hii inazamia katika kuchunguza nyimbo na dhima zake katika taaluma ya uganga katika jamii ya Waswahili. Ali(2016) pia naye katika uchunguzi wake anaangazia nyimbo za uganga katika jamii ua Waswahili na

Wapemba na kugundua kuwa nyimbo za uganga huwa na siri kubwa katika jamii ambayo huhusiana na utoaji wa tiba. Kazi hii inajikita katika uchunguzi wa nyimbo na umuhimu wake katika uganga. Hata kama inasaidia welewa wa tiba katika taaluma ya uganga, haifaidi utafiti wetu kwani utafiti huu wetu unachunguza athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe. Natalia (2019) anachunguza jinsi nyimbo hutumika kama tiba ya kisaikolojia kwa anayeugua. Pia nyimbo hutumiwa kurekebisha upotovu wa mihemko na kupotoka kwa tabia. Utafiti huu haujafaidi utafiti tunaofanya kwa sababu utafiti wetu unajikita katika methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

### 4.4 Hitimisho

Kuyafikia malengo mahususi ya utafiri huu, sura hii imechambua data ya methali za Kiswahili zilizokusanywa na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yenyewe unatekelezwa kwa mwongozo wa madhumuni mahususi pamoja na mihimili ya nadharia ya utafiti. Kwanza, matumizi ya vipengele vya fani katika methali za Kiswahili kubainishia ugonjwa, uuguzi na tiba yanaangaziwa. Inathibitika kwamba vipengele vya fani kama vile taswira, takriri, tashibihi, kejeli, sitiari, kweli-kinzani na kinaya vinatumika kuwasilishia ujumbe unaohusika. Matokeo ya uchunguzi huu yanabaini kuwa vipengele hivi vya fani vinatumika kusisitiza ujumbe, husaidia kukumbukika kwa ujumbe kwa urahisi, huleta mvuto katika maongezi, huficha ujumbe na pia hupunguza ukali wa ujumbe unaobebwa na methali teule. Hili ni dhihirisho kuwa vipengele hivi vya kifani pia ni muhimu kwa kuelekeza mkondo wa ujumbe katika kueleweka kwa ujumbe uliobanwa nazo kwa urahisi. Aidha, mbinu katika methali hizi unadhihirisha ufundi ulioko katika utunzi wa methali hizi. Pili, matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili kuwasilishia ujumbe yanaangaziwa. Matokea ya utafiti huu yanabaini kuwa methali hizi teule

zinatumika kuwasilisha jumbe tofauti kama vile kuchukua tahadhari kabla ya hatari, umuhimu ya kizazi cha kesho, kuwapa wanajamii matumaini, umuhimu wa kuvumilia, ushirikiano na umoja katika jamii, kuwa na subra maishani, viumbe wanatumiwa kuwasilisha ujumbe, dawa inatumiwa ikilinganishwa na suluhu na matumizi mingineo. Lengo la tatu na la mwisho, linaisilisha kwa kuangazia athari zinazotokana na usawiri wa ugonjwa, uguzi na tiba katika ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili. Baada ya kupitia vipengele mbalimbali ambavyo vinatumika katika methali tunazochunguza, inabainika wazi kuwa methali hizi zinaakisi hali chanya na hali hasi katika kuwasilisha ujumbe wake. Hata hivyo methali teule nyingi zinaakisi hali chanya kwa mfano zinaleta athari zinazobeba ujumbe wa kujenga na kuleta matumaini, ni bora kufanya mambo kwa utaratibu, ni vyema kuchukua tahadhari kabla ya hatari, kukuza uhusiano mwema, umoja na ushirikiano, kuchora umuhimu wa kustahimili na pia mapenzi. Baadhi ya athari hasi ni kuleta utamaushi, ubaguzi na unyanyapaa, makovu ambayo huachwa na baadhi ya magonjwa na vilevile hadaa itokanayo na vitu vipya.

Mount Kenya University

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii ya mwisho ya utafiti inawasilisha muhtasari wa uchunguzi uliokamilika. Muhtasari wa tasnifu nzima pamoja na muhtasari wa matokeo ya utafiti unawasilishwa mtawalia kabla ya kuwasilisha hitimisho la utafiti wenyewe. Hatimaye, mapendekezo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye yanawasilishwa.

### 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu unabeba sura tano zilizo na mada kuu na chini ya mada kuu kuna zingine ndogondogo. Sura ya kwanza katika uchunguzi huu inanuia kutoa mwongozo unaotumika katika utafiti huu. Vipengele muhimu katika utafiti huu vinajadiliwa ili kuelewesha na kuliibua tatizo la utafiti. Vipengele hivi ni usuli wa tatizo, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, vikwazo vya utafiti, mipaka ya utafiti na uteuzi wa sampuli.

Katika sura ya pili nayo, dhana mbalimbali zilizo na umuhimu mkubwa kwenye utafiti huu zinaelezewa kwa kina kirefu. Umuhimu wa methali na matumizi yake kwa watu unabainika wazi kutokana na tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa na wanaparemiolijia mbalimbali waliokusanya methali na kuziainisha kwa njia tofautitofauti na wengine kuzieleza kwa kina kimatumizi na sifa zake mabalimbali. Mapitio ya kazi tangulizi yanaonyesha kuwa hakuna mtafiti mwingine aliyefanyia utafiti kipengele hiki cha usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Utafiti huu unaangazia methali mbalimbali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba.

Ili kufukia malengo ya utafiti huu, vipengele mbalimbali vinavyohusiana na ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti vinaelezewa katika sura ya tatu ya utafiti huu. Vipengele vyenyewe ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa ya utafiti, sampuli na usampulishaji, njia za kukusanyia data, vifaa vinakavyotumika katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data inayokusanywa na hatimaye mazingatio ya maadili na miiko ya utafiti.

Ili madhumuni mahususi ya utafiti huu wetu yakamilike, katika sura ya nne tunajibidiisha kufanya uwasilishaji wa data tunayokusanya na kuichambua data ile kwa kina. Ili utafiti huu ufuate mfumo maalum, katika uwasilishaji na uchambuzi data madhumuni mahususi yote matatu ya yanaangaziwa tukianza na madhumuni ya kwanza, harafu ya pili na hatimaye yale ya tatu. Kwanza tunaangazia jinsi vipengele vya fani vinavyotumika kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za kiswahili. Vipengele hivyo ni takriri, tashibihi, sitiari, kweli kinzani, kejeli na kinaya.

Kisha katika madhumuni yanayofuata, ambayo ni ya pili tunaangazia ni kwa njia gani ugonjwa, uuguzi na tiba hutumika ili kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili. Madhumuni haya ynaangaziwa kwa kuongozwa na msamiati mkuu katika utafiti huu ambapo tunachambua jinsi ugonjwa huwasilishia ujumbe, jinsi uuguzi huwasilishia ujumbe na hatimaye jinsi tiba huwasilishia ujumbe katika methali teule za Kiswahili. Madhumuni ya tatu na ya mwisho, yanaisilisha kwa kuangazia athari zinazotokana na usawiri wa ugonjwa, uguzi na tiba katika ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu unafanywa kwa makusudio ya kutimiza madhumuni mahususi matatu na ili kupitia kwa hayo madhumuni, lengo kuu la utafiti litimizwe.

### 5.2.1 Vipengele vya Fani Vitumikavyo Kubainishia Ugonjwa, Uuguzi na Tiba

Madhumuni mahususi ya kwanza katika utafiti huu ni kuangazia jinsi vipengele vya fani vinavyotumika kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali teule za Kiswahili. Vipengele hivyo ni takriri, tashihisi/uhuishi, taswira, sitiari, kweli-kinzani, kejeli na kinaya. Matokea ya utafiti huu yanaashiria kwamba, methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumia vipengele mbali mbali vya kifani. Hata hivyo, ili kufanikisha malengo ya utafiti huu, vipengele vichache tu vinachunguzwa. Kipengele cha kwanza ni takriri. Inatumika katika methali husika kutoa msisitizo kwa kurejelea ugonjwa, uuguzi na tiba. Msisitizo unaoletwa na takriri huonyesha umuhimu wa jambo linalorejelewa. Kupitia msisitizo huu tunaona umuhimu wa kutafuta matibabu wakati unaofaa, kutilia mkazo juhudi na umuhimu za waganga katika kuuguza na pia umuhimu wa kutumia tiba na dawa anazopewa mgonjwa hata kama wakati mwingine huwa chungu na zisizopendeza kwa mtu. Kipengele cha pili ni tashihisi au uhuishaji. Hiki nacho pia kinatumika katika methali hizi teule. Kinaonyesha jinsi ugonjwa unavyohuishwa ili kutoa ujumbe unaoeleweka kama vile ugonjwa huwa si rafiki ya mtu, yafaa utibiwe, na kuvumilia kutumia dawa hata kama ni chungu mtu anapougua. Taswira pia inatumika kutoa ujumbe na kujenga picha kuhusiana na ugonjwa na athari zake kwa mwanadamu. Kipengele cha kejeli kinatumika kuwasilisha ujumbe kwa kutumia dhihaka ili kukebehi tabia hasi katika jamii. Kwelikinzani inatumiwa kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kulinganisha hali mbili kinzani ili kufikirisha mtu kufahamu ujumbe kwa kina. Sitiari inatumika kulinganisha hali mbili au hali na vitu vinavyofahamika na jamii ili kurahisisha uelewa wa ujumbe, vilevile kipengele hiki husaidia mtu kufikiria zaidi na kwa undani ujumbe wa methali teule.

### 5.2.2 Matumizi ya Ugonjwa, Uuguzi na Tiba Kuwasilishia Ujumbe

Madhumuni ya pili ambayo ni matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilisha ujumbe yanafanyiwa uchunguzi. Katika matokeo ya utafiti huu inabainika vyema kuwa ugonjwa ndicho kipengele cha maudhui ambacho kinabeba asilimia kubwa katika kutoa ujumbe pale ambapo ugonjwa unafananishwa na viumbe tofauti ili kukamilisha ujumbe, ujumbe wa kuchukua tahadhari kabla ya hatari,umuhimu wa kuendeleza kizazi katika jamii, ugonjwa kutumika kuashiria tatizo na jumbe zinginezo. Vile vile uuguzi na tiba zinatumika kuwasilisha ujumbe kama vile dawa inalinganishwa na suluhu, dawa kulinganishwa na hali fulani na ujumbe wa kutegemeana. Uuguzi unawasilisha ujumbe wa utamaushi na pia wa kujali au kutunza, na manufaa ya ujuzi katika jamii.

### 5.2.3 Athari ya Usawiri wa Ugonjwa, Uuguzi na Tiba kwa Ufasiri wa Ujumbe

Madhumuni ya tatu yalikuwa kutafiti athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika kufasiri ujumbe ambako matokea yanabaini methali hizi zinaleta athari chanya na hasi katika ufasiri wa ujumbe kama vile, mambo yanahitaji kufanywa kwa utaratibu, uhusiano unaoletwa na magonjwa, kukata shauri ni jambo la muhimu, usiri unaokuwepo mtu anapougua ugonjwa fulani, ustahamilivu na wakati mwingine ugonjwa huleta ubaguzi.

## 5.3 Hitimisho

Katika utafiti huu, tunaangazia jinsi methali teule za Kiswahili zinavyotumika kusawiri ugonjwa, uuguzi na tiba. Azma kuu ya uchunguzi huu imekuwa kuchunguza jinsi methali za Kiswahili zinatumika kusawiri ugonjwa, uuguzi na tiba ambayo inachomozwa na malengo mahususi matatu; kufafanua matumizi ya vipengele vya fani kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili, kudadavua matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba

kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili na kutathmini athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili.

Matokeo ya uchunguzi huu yanabaini kuwa vipengele hivi vya fani vinatumika kusisitiza ujumbe, husaidia kukumbukika kwa ujumbe kwa urahisi, huleta mvuto katika maongezi, huficha ujumbe na pia hupunguza ukali wa ujumbe unaobebwa na methali teule. Haya yanadhihirisha kuwa vipengele hivi vya kifani pia ni muhimu kwa kuelekeza mkondo wa ujumbe katika kueleweka kwa ujumbe unaobanwa nazo kwa urahisi. Aidha, mbinu katika methali hizi zinadhihirisha ufundi ulioko katika utunzi wa methali hizi.

Pili, matokea ya utafiti huu ynaebaini kuwa methali hizi teule znaetumika kuwasilisha jumbe tofauti kama vile kuchukua tahadhari kabla ya hatari, umuhimu ya kizazi cha kesho, kuwapa wanajamii matumaini, umuhimu wa kuvumilia, ushirikiano na umoja katika jamii, kuwa na subra maishani, viumbe wanatumiwa kuwasilisha ujumbe, dawa inatumiwa ikilinganishwa na suluhu na matumizi mingineo.

Katika lengo la tatu linaangazia athari zinazotokana na usawiri wa ugonjwa, uguzi na tiba katika ufasiri wa ujumbe katika methali za Kiswahili na kubainika wazi kuwa methali hizi zinaakisi hali chanya na hali hasi katika kuwasilisha ujumbe wake. Kama vile ujumbe wa kujenga na kuleta matumaini, ni bora kufanya mambo kwa utaratibu, ni vyema kuchukua tahadhari kabla ya hatari, kukuza uhusiano mwema, umoja na ushirikiano, kuchora umuhimu wa kustahimili na pia mapenzi,kuleta utamaushi, ubaguzi na unyanyapaa, makovu ambayo huachwa na baadhi ya magonjwa na vilevile hadaa itokanayo na vitu vipya. Utafiti huu umeweza kuthibitisha malengo yote matatu kutokana na matokeo yake.

### 5.4 Mapendekezo

Sehemu hii ina hitimisha utafiti huu kwa kutoa mapendekezo ya utafiti huu na mapendekezo mengine ya baadaye ambayo yanaweza kufanywa na watafiti wengine wa siku za usoni kuendeleza utafiti kwa kujaza pengo au mapengo ambayo utafiti huu unayaacha.

#### 5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni matatu ambapo lengo la kwanza ni kufafanua matumizi ya vipengele vya fani kubainisha ugonjwa, uuguzi na tiba katika methali za Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba, methali za Kiswhili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumia vipengele vya fani kama vile takriri, kinaya, taswira, kejeli, tashihisi, kwelikinzani na sitiari kuwasilishia ujumbe wake. Vipengele hivi vya fani ndivyo vitumikavyo kuufumba na kuukoleza ujumbe wake.

Lengo la pili lilikuwa kudadavua matumizi ya ugonjwa, uuguzi na tiba kuwasilishia ujumbe katika methali za Kiswahili. Inathibitika kwamba methali za Kiswahili zinazosawiri ugonjwa, uuguzi na tiba zinatumika kuwasilisha ujumbe maalum kama vile matumaini, utamaushi, tahadhari, subira pamoja na kuhamasisha upendo, umoja na ushikamano katika jamii ya Waswahili.

Nalo lengo la tatu lilikuwa kutathmini athari ya usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba kwa ufasiri wa ujumbe wa methali za Kiswahili. Matokeo haya yanabainisha kuna athari chanya na hasi katika methali teule. Athari zinazotokana na ufasiri wa ujumbe katika methali hizi ni kama vile: umuhimu wa kufanya mambo kwa utaratibu, uhusiano wa ukaribu uletwao na ugonjwa, ukataji shauri, usiri mtu anapougua badhi ya magonjwa, ustahamilivu, ubaguzi na

Mount Kenya University

unyanyapaa, makovu ya ugonjwa maishani, msaada, matumaini pamoja na usugu wa baaadhi ya magonjwa umedhihirishwa.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadaye

Fasihi simulizi huwa na tanzu na vipera vingi, utafiti unaweza kufanywa katika vipera vingine kuchunguza jinsi usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba unavyothihirika katika vipera hivi.

Utafiti huu unajikita katika methali za Kiswahili tu, kwa hivyo utafiti kama huu unaweza kufanywa na watafiti wengine katika methali nyingine za makabila mengine barani Afrika au ulimwenguni kote. Nadharia tofauti inaweza kutumiwa katika tafiti za baadaye.

Uchunguzi wa viumbe na wanyama waliotumika kuunda methali za Kiswahili unaweza fanywa kubaini kwa nini viumbe na wanyama hao wakatumiwa katika muundo wake.

Utafiti wa tamathali za lugha katika methali za Kiswahili kwa ujumla unaweza fanywa vilevile kubaini tamathali zinazotumika na zinasaidia kutoa maana gani za methali hizo.

Uchunguzi wa usawiri wa ugonjwa, uuguzi na tiba katika tanzu zingine za kifasihi unaweza fanywa kama vile katika tamthilia, riwaya ama ushairi.

Mount Kenya University

# MAREJELEO


Ali, M. (2016). *Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Uganda katika jamii za Waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Andambi, A. na Murono, E. (2005). *Muundo Mpya wa Methali za Kiswahili.* Nairobi: Mvule Africa Publishers.

Arege, T. na Nyonje, M. (2011). *Kamusi Fafanuzi ya Methali.* Nairobi: Target Publications.

Awhida, H. (2021). *Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello.* Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Sabha: Chuo Kikuu cha Sebha.

Baker, C., Wuest, J. na Stern, P. (2010). *Method Slurring: The Grounded Theory/ Phenomenology Example*. *Journal of Advanced Nursing 17*(1), 1355-1360.

Baldrick, C. (2001). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York: Oxford University Press.

Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA). (2010). *Kamusi la Kswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Bathers, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.

El-jetlawiy, R. (2013). *Kufanana na Kutofautiana kwa Maudhui na Fani kati ya Methali za Kitanzania n na Kilibya: Utafiti Linganishi*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Farida, H. (2018). *Kuchunguza Sanaa na Dhima za Methali za Wahaya.* Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Finnegan, R. (1984). *Oral Tradition and the Verbal Arts*. New York: Routledge.

Haji, G. (2018). *Mbinu za Utunzi wa Nyimbo za Uganga wa Pepo Zanzibar: Mifano kutoka Jamii ya Watumbatu, Zanzibar*. Kioo cha Lugha

Hatibu, S. (2017). *Kuchunguza Dhima za Methali zinavyoendeleza Elimu ya Jadi*: Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa: Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Tanzania

Ibrahim, M. (2020). *Nafasi ya Mwingiliano Fani katika Kukuza Fasihi ya Watoto:*Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Rongo: Chuo Kikuu ch Rongo.

Jilala, H. (2008). *The Artistic Uses of Metaphores in Constructing Meanings and Messages in New Generations Songs in Tanzania. MA Dissertation (unpublished)*, University of Dar es Salaam.

Karama, S. na Saidi, S. (1983). *Maelezo ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Khatibu, T. (2017). *Dhamira Zijengwazo na Taswira Katika Methali za Wapemba*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

King'ei, K. na Ndalu, A. (2009). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Kingei, K. na Ndalu, A. (2008). *Kamusi ya Methali, Toleo Jipya*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Kitetu, W. (2003). *Ethical Issues in Data Collection. In Social Science Research: Getting into the Field. Katika Wawasi*, *AICAD/Department of Languages and Linguistics, Egerton University Juz. 2*. Kur. 30-46.

Kitundu, G. (2018). *Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha: Uchunguzi Kifani kutoka katika Matini Teule za Kiswahili.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Klarer, M. (2004). *An Introduction to Literary Studies*, *Toleo la 2*. New York: Routledge.

Kombo, D. and Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kombo, O. (2014). *Uchunguzi Kifani wa Mashairi ya Ukimwi katika Magazeti ya Kiswahili* Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa: Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*, *Toleo la 2*. New Delhi: New Age International Publishers.

Kothari, C. (2008). *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques*. New Delhi: New Age Internationl Publising.

Kyando, L. (2013). *Majina Sadfa ya Wahusika katika Kusadikika* na *Kichwamaji*. *Mulika 31(1)*, 37-50.

M'Ngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Madumulla, J. (2005). *Proverb and Saying: Theory and Practice*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Phoenix Publishers.

Maitaria, J. (2012). *Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali:* Tasinifu ya Ph.D Isiyochaoishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mark, G. (1995). *Postmodern Semiotics*: *Material Culture and the Forms of Postmodern Life*. Oxford: Basil Blackwell.

Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mauya, A. (2008). *Semi: Maana na Umuhimu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Ltd.

Mbonde, J. (2005). *Methali za Kiutandawazi. Makala ya Kongamano la Miaka 75 ya TUKI*. Dar es Salaam: TUKI.

Mkota, A. (2009). *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi*. Nairobi: Vide~Muwa.

Mohamed, S. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mphande, D. (2001). *Tonga Proverbs from Malawi*. New York: Philadelphia.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salam University Press.

Msokile, M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Kifasihi*. Dar es Salaam: East Africa Education Publishers.

Mtesigwa, P. (1989). *Methali ni Nini? Kiswahili 56(1)*, 1-9.

Mugenda, O. na Mugenda, J. (2003). *Reseach Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: ACTS Press.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Hria cha Tanzania.

Murono, S. (2005). *Tadubiri za Insha*. Dar es Salaam: Longhorn.

Mutembei, A. (2009). *Ukimwi katika fasihi ya kiswahili 1982-2006*. Dar es salam: TATAKI.

Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziyya.* Dar es Salaam: TUKI.

Mwakio, W. (2016). *Matumizi ya Tashibiha, Sitiari na Taashira Katika Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwangi, I. na Wamalwa, K. (2016). *Miali ya Ushairi: Shule za Upili na Vyuo Vya Elimu*. Nairobi: East African Educational Publishers

Nazarova, T. (1996). *Linguistics and Literary Semiotics*. Moscow: Moscow State University Press.

Ndalu, A. (1989). *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mount Kenya University

Nsookwa, C. (2011). *Dokezo za Sitiari katika Methali za Kiswahili na Kigadnda.* Tasnifu ya Uzamifu Isiyochapishwa. Kampala: Chuo Kikuu cha Makerere.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Oyinda, P. (2016). *Ulinganishi na Ulinganuzi wa Tasfida za Matibabu katika Kiswahili Kimarachi*: Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa: Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oyaro, C. (2019). *Tafsiri za Methali na Misemo Katika Mshale wa Mungu.* Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa: Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi

Raymond, N. (2016). *Usawiri wa Mwamamume katika Methali za Kimeru Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Kilifi: Chuo Kikuu cha Pwani.

Robson, C. (2007). *How to do a Research Project*: *A Guide for Undergraduate Students*. Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Samwel, M na wenzake (2013). *Ushairi wa Kiswahili, Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea.* Dar es-Salaam: Meveli Publishers.

Sengo, T. (2009). *Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AER Kiswahili Researched Products.

Sengo, T. (2016). *Falsafa ya Maisha*. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Researched Products.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Shemweta, G. ( 2015) *Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo*: Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Simiyu, W. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*: Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mount Kenya University

Sito, S. (2015). *Athari za Mazingira katika Uteuzi wa Msamiati*: *Mfano wa Methali za Kiswahili Zinazorejelea Viumbe wa Majini*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Smith, B. (2016). *What was "close reading"? A Century of Method in Literary Studies. The Minnesota Review 87*(1), 57-75.

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4.* Dar es Salaam: TUKI.

Timanywa, F. (2017). *Kuchunguza Ujinsia na Matumizi ya Lugha katika Methali za Wakurya*. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wamitila, K. (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longman.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phonex Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia:* Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide~Muwa.

Wamitila, K. (2011). *Kamusi ya Methali*: Naiobi: Longhorn Publishers.

Waterman, C. (2009). *African Music Microsoft student 2009: DVD.* Redmon W.A.: Microsoft Cooporation.

Mount Kenya University

Yego, K. (2013). *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar. Tasinifu ya Uzamili Isiyochapishwa*, Chuo Kikuu Cha Nairobi

Yin, R. (1994). *Case Study Research: Design and Methods, Toleo la 2.* California: SAGE Publishers.

Mount Kenya University

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO I: METHALI ZIHUSUZO UGONJWA, UUGUZI NA TIBA

(1) *Adhihakiye kovu hajaona jeraha.*

(2) *Aendaye kwa mganga hakosi jambo.*

(3) *Afichaye ugonjwa hazai.*

(4) *Agunduaye ndwele ndiye mganga.*

(5) *Auguaye huanguliwa.*

(6) *Baada ya donda msumari moto*

(7) *Baada ya kifi ni tabibu*

(8) *Baada ya kuingiwa na mwiba ndipo walambuka kiatu.*

(9) *Baniani mbaya kiatu chake dawa*

(10) *Buyu kali ni dawa ya mwana mimba.*

(11) *Chendacho kwa mganga hakirudi.*

(12) *Dawa inayowasha inakupenda.*

(13) *Daawa si dawa.*

(14) *Dawa si chungu, chungu ni maradhi.*

(15) *Dawa ya deni ni kulipa.*

(16) *Dawa ya hasira ni kicho.*

(17) *Dawa ya jipu kulipasua.*

(18) *Dawa ya moto ni moto.*

(19) *Donda ndugu laisha dawa*

(20) *Ganga ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini.*

(21) *Hapana jeraha bila silaha.*

(22) *Hapana uchungu usiotulia.*

(23) *Heri kunjikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi.*

(24) *Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha.*

Mount Kenya University

(25) *Ila ya kikwapa kunuka pasipo kidonda.*

(26) *Iliyopita si ndwele ganga ijayo.*

(27) *Ituuzayo tia hiyo isiyokuwako si dawa.*

(28) *Jino la pembe si dawa ya pengo.*

(29) *Jino liumalo hung'olewa.*

(30) *Kidole kimoja kikiumia chenzake chapwita.*

(31) *Kiendacho kwa mganga hakina marejeo.*

(32) *Kinga ni bora kuliko tiba.*

(33) *Kipendacho moyo ni dawa.*

(34) *Kipya kinyemi ingawa kidonda.*

(35) *Kufanya gaga si kupoa donda.*

(36) *Kufanyika gaga sio kupona kwa donda.*

(37) *Kuna kufa na kupona, na kuliwa na kingugwa.*

(38) *Kutaataa sio dawa ya kufa.*

(39) *Kuzuia ni bora kuliko kuponya.*

(40) *Kuzunguka mbuyu si dawa ya shetani.*

(41) *Kwa mdogo pumu kwa mkubwa mafua.*

(42) *Kwa mkunga haziishi nyimbo*

(43) *Mali ya mgonjwa faida ya mfumu.*

(44) *Maneno mengi maradhi.*

(45) *Mapenzi kikohozi hayawezi fichika.*

(46) *Maradhi huja shoti yakitoka, ni mtambao wa kinyonga.*

(47) *Mficha ndwele hapati dawa.*

(48) *Mganga hajigangi.*

(49) *Mgonjwa haulizwi dawa.*

(50) *Mgonjwa ni mwenzi wa kitanda.*

(51) *Mkimbilia sheria hujiponya.*

(52) *Mwana kidonda, mjukuu kovu.*

Mount Kenya University

*(53) Mtambua ndwele ndiye mganga*

*(54) Mwana mui dawa ya mlango.*

*(55) Mwenda mbio hujikwaa dole*

*(56) Mwenda pole hajikwai.*

*(57) Mwenye kovu haliwai na kidonda.*

*(58) Mwenye kuficha kidonda,kilio kitamfichua.*

*(59) Mwenye kovu asidhani kapoa.*

*(60) Mwenye matende hana mapaja.*

*(61) Mzaha mzaha hutumbuka usaha.*

*(62) Nduli na mchimba dawa shauri lao ni moja.*

*(63) Neno jiwi ni jeraha la moyo.*

*(64) Neno ovu ni jeraha la moyo.*

*(65) Ngoja ngoja huumiza matumbo.*

*(66) Ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini akasaidiwe.*

*(67) Ng'ombe mteua jani ni mgonjwa.*

*(68) Nia njema tabibu,nia mbaya harabu.*

*(69) Nzi kufa juu ya kidonda si haramu.*

*(70) Pembe si dawa ya kuku.*

*(71) Penzi la moyo ni dawa.*

*(72) Pumu zimepata kikohozi.*

*(73) Sahau ni dawa ya waja.*

*(74) Shibe ya waganga hutoka kwa wagonjwa.*

*(75) Shino ya kuitikiza sio chungu.*

*(76) Shomvi mbaya kiatu chake dawa.*

*(77) Si hasara nzi kufa juu ya kidonda.*

*(78) Sikio la kufa haliskii dawa.*

*(79) Sitafuga ndwele na waganga tele.*

*(80) Tabibu hakingi ajali.*

Mount Kenya University

(81) *Ugonjwa ni suna, kufa ni faradhi.*

(82) *Ukiona ambari na zinduna ipapo.*

(83) *Ukiona zabadi na zinduna i papo.*

(84) *Ukiwaa uwe na subira.*

(85) *Umeingiwa mti.*

(86) *Usipouguza mwele una koo la ujuko.*

(87) *Utamu wa kidonda umemwua nzi.*

(88) *Uzee hauna dawa*

(89) *Wanja wa Manga si dawa ya chongo.*

(90) *Yaliyopita si ndwele, ganga yajayo.*

Mount Kenya University

## KIAMBATISHO II: CHETI CHA UZINGATIFU WA MAADILI

**Mount Kenya University**

REF: **MKU/ISERC/3304**
TO: **JOSEPH GIKONYO MWANGI**

Date: 27 October 2023

REG: **MAKI/2022/44670**

Dear Sir/Madam,

**RE: USAWIRI WA UGONJWA, UUGUZI NA TIBA KATIKA METHALI ZA KISWAHILI**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **2348.** The approval period is **27/10/2023 - 26/10/2024.**

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used
ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

The Chairman
Mount Kenya University
Ethics Review Committee
P. O. Box 342 - 0100, Thika

Yours sincerely

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika. Tel: +254 67 2820 000,
Cell: +254 720 790 796, 0709 153 000
Email:info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.
Unlocking Infinite Possibilities

**KIAMBATISHO III: BARUA YA UTAMBULISHO KWA NACOSTI**

# Mount Kenya University

## DIRECTORATE OF GRADUATE STUDIES

**MAKI/2022/44670**

3rd November, 2023

***National Commission for Science Technology & Innovation (NACOSTI)***
***Off Waiyaki Way, Upper Kabete,***
***P.O Box 30623- 00100***
***NAIROBI, KENYA***

Dear Sir/Madam,

**RE: JOSEPH GIKONYO MWANGI – REGISTRATION NO. MAKI/2022/44670**

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Master of Arts in Kiswahili** in the Department of **Psychology, Languages and Humanities** in the School **of Social Sciences.**

The title of the research is **"Usawiri wa Ugonjwa, Uuguzi na Tiba katika Methali za Kiswahili."**It has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data between **November, 2023 and January, 2024.**

Any assistance accorded to the student will be highly appreciated.

Thank you.

Mount Kenya University
P. O. Box 342 - 01000,THIKA
Office of the Director,
Graduate Studies

**Dr. Samuel M. Karenga, Ph.D**
**Director, Graduate Studies**
**Enc.**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 / +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.
Unlocking Infinite Possibilities

## KIAMBATISHO IV: KIBALI CHA CHA UTAFITI NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **403200**

Date of Issue: **09/December/2023**

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. JOSEPH GIKONYO MWANGI of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kiambu on the topic: USAWIRI WA UGONJWA, UUGUZI NA TIBA KATIKA METHALI ZA KISWAHILI for the period ending : 09/December/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/31647**

**403200**
Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commision for Science, Technology and Innovation -